ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 5 Julai, 2011

(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika *order paper* naona kuna makosa kidogo, imeandikwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Sasa nilifanya marekebisho ya haraka haraka, lakini mwenyewe hasa ni huyu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 182

Msamaha kwa Wafungwa

Mhe. Asha Bakari Makame (Kny: Mhe. Wanu Hafidh Ameir) - Aliuliza:-

Kwa kuwa masuala ya Magereza sio miongoni mwa mambo ya Muungano.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazofanya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa msamaha kwa wafungwa wakati wa Sherehe za Muungano; tena kwa upande wa Tanzania Bara tu.

(b) Kwa nini msamaha huo usifanywe wakati wa Sherehe za Uhuru wa Tanganyika kwa kuwa wafungwa wanaopata msamaha huo ni wa Tanzania Bara pekee.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika , kwanza napenda nimpongeze Mhe. Wanu Hafidh kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Na. 182 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

a). Mhe. Spika, ni kweli kabisa masuala ya Magereza si mambo ya Muungano, Magereza yapo Tanzania Bara. Aidha, kwa upande wa Zanzibar tunavyo Vyuo vya Mafunzo na kutokana na sababu hiyo, ndio maana Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 45(1)(a) na Ibara ya 45(3) zinampa uwezo rais kutoa msamaha kwa wafungwa waliopo magerezani Tanzania Bara pamoja na wafungwa waliohukumiwa kwa adhabu zilizotolewa Zanzibar kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayotumika Zanzibar.

Aidha, Rais wa Zanzibar hutoa msamaha kwa wanafunzi walioko katika Vyuo vya Mafunzo viliopo Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Ibara ya 59.

b). Mhe. Spika, sababu za kutolewa msamaha huo kwa upande wa Tanzania Bara katika sherehe za Muungano ni utaratibu aliojipangia mwenyewe Rais wa Tanzania. Naomba ifahamike kuwa Mhe. Rais anao uwezo wa kutoa msamaha kwa wafungwa wakati wowote hata kama hakuna sherehe za kitaifa.

Nam. 152

Serikali ya Mitaa

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Kwa kuwa sasa serikali yetu inaamini mamlaka ya uongozi yapo mikononi mwa wananchi na maendeleo ya kweli yataletwa na wananchi na kuna Asasi za Kiraia hivi karibuni zilikuja kutuomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuishauri serikali kuboresha Sera ya Kuimarisha Serikali za Mitaa hapa Zanzibar.

Je, serikali hadi sasa imelifanyia kazi kwa kiasi gani wazo la kuwepo mipango imara na yenye nia ya kuanzisha Serikali za Mitaa zilizo imara kwa kuchaguliwa na wananchi kama ilivyo kwa Tanzania Bara.

Mhe. Waziri Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 152 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyuokwishasema awali na ninakumbuka wiki iliyopita nilijibu swali kama hili kwamba, Katiba ya Zanzibar kifungu Nam. 128 kinaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa ambazo uchaguzi wake, madaraka na kazi zake zitakuwa kama zitakavyoelezwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi lilitunga Sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 na Sheria Nam. 4 ya Mwaka 1995 kwa ajili ya kuanzisha kazi na kuweka utaratibu wa utendaji wa Baraza la Mapispaa, Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji ya Wete, Mkoani na Chake-Chake. Hatua hii imewezesha serikali kuanzisha Serikali za Mitaa hadi katika ngazi ya Wadi.

Mhe. Spika, serikali hivi sasa inakamilisha mchakato ambao utaweka mkakati wa kuimarisha Serikali za Mitaa kwa kutayarisha mpango wa mageuzi ya Serikali za Mitaa ambao pia umeainishwa katika Mpango wa Mageuzi wa Utumishi wa Umma. Pia serikali imo katika hatua za mwisho za matayarisho ya Sera ya Serikali za Mitaa.

Nakiri kwamba sera hii imechelewa lakini kwa uzito wake na ugumu nahisi bora twende taratibu na hatimaye tutakamilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa wadau wakubwa wa kuunda hizi serikali za mitaa ni madiwani mpaka katika ngazi ya wadi kama alivyosema Mhe. Waziri, na kwa kuwa serikali bado haijataka kuwatambua vizuri hawa madiwani. Haoni kuwa hiki ndio kikwazo cha kuanzishwa hizo serikali za mitaa kwama madiwani bado hawajataka kutambuliwa kazi zao na serikali na bado kuna kusuasua kuhusu kazi za madiwani na kazi za masheha.

(b) Kama kuna mchakato ambao unaendelea, Mhe. Waziri anaweza akatupa tarehe ya kuanzishwa kwa hizo serikali za mitaa kama inavyotakiwa na Serikali Kuu.

Mhe. Waziri Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza naomba nimjulishe Mhe. Rashid Seif kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatambua rasmi madiwani. Wao ni waheshimiwa, wamechaguliwa kama tulivyochaguliwa sisi wawakilishi, lakini wao wamechaguliwa katika ngazi ya Wadi. Kwa hvyo, inawatambua rasmi na kama nilivyosema wapo kikatiba na kazi zao kwenye sheria hii niliyoizungumza zimeainishwa wazi, kazi za masheha pia zimeainishwa wazi.

Tatizo alilozungumza kwamba labda kuainisha mishahara hilo tunasema ni moja katiak hizo *reforms* tunazokujanazo tutakuja na mapendekezo walipwe vipi. Hivi sasa tunashukuru kila Halmashauri au Baraza la Mji wanawalipa maposho kwa mujibu wa uwezo wao, lakini kwa kweli tunawatambua rasmi.

Swali la pili aliuliza itakuja lini? Kama nilivyokwishaeleza awali kwamba tunatarajia ile rasimu ya Sera kamili na Sheria ya mwaka huu wa fedha tutaileta hapa Barazani baada ya mchakato mzima wa masemina na kupita kwenye kamati.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa alipokuwa akijibu swali amekubali kuwa Madiwani wanachaguliwa kwa kura za wananchi kama vile Mbunge, Mwakilishi na viongozi wengine wa kuchaguliwa, na kwa kuwa kakiri kuwa Masheha ziko sheria zinazoainisha kazi zao na kazi za Madiwani. Lakini atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba Masheha wanaingilia kazi za Madiwani na Madiwani pengine wanaingia kazi za Masheha. Kwa hivyo, atakubaliana na mimi kama kuna haja ya kuwafanyia semina ya pamoja na ofisi yake ikawaelimisha wazi wazi kila mmoja kwa pamoja akajua nafasi yake aliyonayo.

Mhe. Waziri Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakiri kwamba kuna migongano ya kazi kati ya Waheshimiwa Madiwani na Masheha, migongano hiyo ipo na kazi zao kwenye sheria zimeainishwa kwa uwazi kabisa, kazi za diwani ziko hizi na kazi za sheha ziko hizi. Lakini kutokana na matatizo ya kiutendaji na kibinadamu yanatokea hayo.

Mhe. Spika, naomba nimjulishe Mhe. Mwakilishi kwamba tuna wadi 141 Unguja na Pemba, Unguja ziko 75 na Pemba ziko 66. shehia zote ni 332 na tumejitahidi kupitia Idara yetu hii ya Uratibu ya Serikali za Mitaa kuwafanyia semina ya masheha peke yao na madiwani peke yao, lakini pia semina ya wote pamoja ili wajuane zile kazi zao na kuepusha migongano. Sasa tutazidi kuwaelimisha tuwafahamishe nini kazi zao na vipi wende.

Nam. 194

Uuzaji wa Jengo la Mambo Msiige

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba nifanye marekebisho madogo sana . kwenye swali (b) pale ambapo tumeandika sheria Nam. 8 isomeke Nam. 9 ya mwaka 2005. baada ya marekebisho hayo naomba kujibiwa swali langu. Mapema mwezi wa Mei, 2011 alipokuwa anarejea safari yake ya Uturuki, Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Moh'd Shein alipata fursa ya kuzungumza na Waandishi wa Habari katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar. Pamoja na Mhe. Rais kuelezea mafanikio ya ziara hiyo, Waandishi wa Habari walipata nafasi ya kumuuliza Mhe. Rais juu ya uuzaji wa jengo la serikali la Mambo Msiige ambapo sehemu hiyo imekusudiwa kujengwa Hoteli ya Nyota Tano (*Five Star Hotel*) ndani ya eneo la urithi wa kimataifa la Mji Mkongwe.

(a) Naomba kujua ni njia zipi alizotumia Mwekezaji huyo kulipata eneo hilo nyeti la serikali.

(b) Mwaka 2005, Baraza la Wawakilishi lilipitisha Sheria Nam. 8 ya 2005 inayohusu masuala ya uuzaji, ukodishaji na uhaulishaji wa mali za umma. Je, ni kwa kiasi gani sheria hiyo ilifuatwa.

(c) Kama eneo hilo limeuzwa au kukodishwa. Je, serikali imepata kiasi gani cha pesa.

Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima yako naomba kwanza kumshukuru sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, Mwakilishi wa Wananzhi Jimbo la Kiwani alinipa kazi kubwa sana Mhe. Spika, ya kuzisoma sheria hizo zote ikiwemo Sheria Nam. 8 nikiitazama haihusiani na suala hili, nikajua huyu amekusudia Sheria Nam. 9. Kwa hivyo, namshukuru sana alinifanya na Sheria Nam. 9 nayo niisome.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 194 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, taratibu za kupatiwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara, jengo la huduma au makaazi ni kama zifuatazo:-

(i) Muombaji hutakiwa kutuma barua yake ya maombi kwa Katibu Mkuu mwenye dhamana ya ardhi.

(ii) Kuelezea dhamira au madhumuni ya matumizi ya eneo linaloombwa.

(iii) Kama eneo hilo halijapangwa kutumiwa na mtu au taasisi nyengine na Wizara ya Ardhi imeridhika na madhumuni ya matumizi ya ardhi yaliyoombewa, muombaji atapatiwa eneo hilo kwa ajili ya kuliendeleza kwa faida ya nchi na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ni matarajio yangu basi, kuwa Mwekezaji aliyeomba eneo la Mambo Msiige amepitia njia hizo.

(b) Mhe. Spika, ni kweli mwaka 2005 Baraza lako tukufu limepitisha sheria Nam. 8 lakini sheria hiyo haihusiani na masuala ya uuzaji, ukodishaji au uhaulishaji wa mali za uuma bali inahusiana na usalama kazini. Aidha, Sheria Nam. 9 ya mwaka 2005 pia haihusiani na masuala ya uuzaji, ukodishaji na uhaulishaji wa mali za umma bali inahusiana na masuala ya manunuzi ya mali za umma. Kwa maana hiyo, sheria zote mbili hazihusiana na upatikanaji wa eneo hili, bali sheria iliyotumika ni Sheria ya Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2003 halafu ikafanyiwa tena marekebisho mwaka 2010.

(c) Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya ardhi, ardhi ni mali ya umma hivyo serikali wakati wote huwa inakodisha eneo na sio kuuza eneo. Kwa maana hiyo, eneo la Mambo Msiige la mita za mraba 0.42 limekodishwa kwa dola za kimarekani elfu 10 kwa mwaka.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyongeza.

(a) Kwa kuwa serikali imetoa kibali hicho cha ukodishwaji wa eneo kwa muda mrefu sana, na kwa kuwa malengo ya serikali na wananchi ni mradi huu kuendelezwa ili maendeleo ya Wazanzibari yapatikane. Ni kwa nini hadi sasa mradi huo haujaendelea.

(b) Katika eneo hilo mbali ya jengo la Mambo Msiige pia lipo jengo la *Starehe Club*. Naomba kujua yamekodishwa pamoja kwa mkataba huo.

(c) Kwa kuwa hii ni mali ya wananchi, kwa nini wananchi wanapohoji inaonekana wanafanya kero.

Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli hadi hivi sasa mradi bado haujaanza, na haujaanza kwa sababu moja kubwa sana. Jengo la Mambo Msiige ni jengo ambalo liko katika majengo ya kale na lazima tufuate taratibu zote ili tuweze kusema sasa mradi unaanza. Tumewasiliana na wenzetu wa *UNESCO* ili kuweza kupata taratibu za kuweza kuliendeleza jengo lile, vyenginevyo tutakuja kuliendeleza na tutatolewa katika majengo ya kale. Kwa hivyo, tunafuata taratibu zote tunahakikisha kwamba tukianza mradi tuanze bila ya kuwa na matatizo. Lakini wajenzi wako tayari wameshaeleza kila kitu, michoro yao iko tayari wanatusubiri sisi na sisi tunakamilisha taratibu zetu ndio tutoe kibali ili tuweze kuanza.

Mhe. Spika, swali lake la pili nataka kumahakikishia kwamba eneo la kiwanja limehusisha eneo la *Starehe Club.*

Swali la tatu Mhe. Spika, wananchi wanapoiuliza serikali yao ni wajibu wao kuihoji na kuiuliza serikali yao. Sisi mawaziri ni wajibu wetu kuwajibu wananchi pale wanapotaka kujua kinachoendelea ndani ya serikali yao. Mimi nathubutu kusema pamoja na mawaziri wenzangu tunapohojiwa na wananchi hatuoni kama ni kero, lakini utaratibu wa kuhoji sasa ndio *some time* unaonekana kama ni kero. Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi waendelee kutuhoji tu na sisi tutawajibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba wananchi ni wajibu wao kuhoji na mawaziri wako tayari kujibu, kwa hivyo, naamini kwamba kwa kuwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi, naomba nimuulize hivi.

Je, katika utaratibu wa ukodishaji kuna wakodishwaji wangapi ambao waliomba kukodishwa eneo hili? Na je, ni taratibu gani zilifuatwa katika kumpata yule aliyekuwa bora katika kuweza kumpa mradi huu.

Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mwanzo taratibu za kuomba eneo ziko wazi na madhumuni yake yako wazi. Sina uhakika kwamba waliyoomba ni wangapi, lakini inategemeana na madhumuni uliyoombea. Nitatoa mfano Mhe. Spika.

Kama waliyoomba ni wawili wote wanataka kufanya hoteli mmoja ya nyota tatu na mmooja ya nyota tano, kwa dhamira yetu ya uwekezaji tutampa wa nyota tano. Kwa hivyo, sina uhakika wangapi waliyoomba lakini nasema taratibu za kuomba ziko wazi na kama mwekezaji kazifuata na dhamira

imekubalika basi amepewa hilo eneo. Lakini namhakikishia Mhe. Mwakilishi nitamtafutia kupitia wizara husika halafu nitamkabidhi wangapi waliyoomba na kila mmoja na sababu zake halafu ataridhika yeye mwenyewe kwa nini tumempa huyu.

Mhe. Spika, suala la pili kuhusu utaratibu uliofuatwa wa kumpatia eneo huyo aliyeomba nimeshaueleza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii na nitajitahidi nifupishe swali langu. Mhe. Spika, katika kufuatilia katika vyombo vya habari hili linaloitwa hivi sasa sakata, kwa sababu watu wameligeuza kama ni sakata, suala zima la ukodishaji wa eneo hili la Mambo Msiige, kulitajwa kwamba kulikuwa na washindani wawili, Kampuni iliyokuwa ikiendesha Hoteli ya Zanziba zamani ya Kempinski ambayo tunaambiwa sasa imehamishiwa kwa Uongozi wa *For Season Hotel* na Taasisi ya Aghakan ambayo inamiliki Hoteli ya *Serena Inn*.

Sasa kwa sababu ya kuonekana malumbano baina yao ya kibiashara ambayo yanataka kuiingiza nchi nzima, hebu Mhe. Waziri atusaidie ili wananchi waweze kuelewa na kujua uwezo na hali halisi ya wote wawekezaji wote wawili katika lile eneo la jirani katika Hoteli ya Serena. Huyu Aghakan Foundation amekodishwa kwa kiasi gani kwa mwaka na kiasi gani amekuwa akifuata taratibu ili wananchi waweze kuridhika kuwa uamuzi uliofanywa ulikuwa ni sahihi.

Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa amekuja na masuala mawili, lakini la pili nitaomba nimtafutie majibu kwa sababu sina jibu Aghakan amekodishwa kwa kiasi gani, itabidi nimtafutie halafu nimpe.

Mhe. Spika, uwezo wa Kempinski na uwezo wa Aghakan katika *investing* za Zanzibar sisi tunaangalia dhamira yako, unataka kuwekeza kitu gani hapa Zanzibar. Mhe. Spika, labda niseme tu kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Serena kama Aghakan aliliomba eneo hili kwa dhamira ya ku-*a stand* Hoteli ya Serena, Hoteli ya Serena ni Hoteli ya Daraja la Tatu. Kempinski anataka kujenga hoteli ya daraja la tano. Kwa dhamira hiyo ninaamini kwamba utoaji wa eneo hili umeona ni vyema kuwekeza katika hoteli ya daraja la tano kuliko la tatu hasa tukizingatia kwamba katika Mji wa Zanzibar hatuna hoteli ya daraja la tano. Sasa ukitizama uwezo wao siwezi nikaulinganisha uwezo wao kwa sababu sijaona *accounts* zao, kwa hivyo siwezi nikaulinganisha uwezo wao.

Lakini ninachokiangalia mimi nitafaidika vipi kama ni Mzanzibari, yule atakayenifaidisha kama ni Mzanzibari ndiye mwekezaji ambaye mimi nitamkaribisha kuwekeza Zanzibar.

Suala lake la pili Mhe. Spika, ni kwamba Serena amekodishwa kiasi gani nadhani nitamtafutia majibu kwa sababu toka amekodishwa Serena ni miaka mingi sasa kwa hivyo sina jibu la haraka haraka, wacha nimtafutie halafu nitampatia kupitia kwa taasisi husika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo naomba niongezee pale aliposema uwezo wa Aghakan kwa Zanzibar ambaye kweli ndiye anayeendesha Hoteli ya Serena alileta ombi lake la kukodishwa eneo la jengo lilokuwa la Wizara ya Elimu, jengo la Mambomsige pamoja na *Starehe Club.*

Pale alitaka apewe vitu vitatu vyote serikali ikasema ata jamani tumekupa eneo la Mangapwani zaidi ya miaka 25 sasa hivi, eneo umelizuia wananchi walinyanganywa kule wasilime, wasiokote nazi wasifanye chochote kile na mpaka leo hajaliendeleza. Mhe. Spika, eneo hilo mpaka leo amelikalia tu sasa hivi akaja na ombi hili serikali kupitia Baraza la Mapinduzi ikasema hapana nenda kaliendeleze lile kwanza. Mhe. Spika, naunga mkono majibu kwamba kiuwezo wake kwa Zanzibar ni mdogo alidharau sana.

Nam. 159

Uchimbaji wa Visima Katika Mabonde ya Mpunga

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Maeneo mengi ya mabonde ambayo hupita maji ya mito yameanza kuwa na upungufu mkubwa wa maji na kuifanya baadhi ya mito kukauka kabisa. Hii inatokana na maeneo hayo kuchimbwa visima kama ni vianzio vya maji ya matumizi vijijini na majumbani.

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba jambo hili linachangia kwa kiasi kikubwa cha upungufu wa mavuno ya mpunga.

(b) Katika uchimbaji wa visima hivyo kuna mchango wa kitaalamu unaopatikana katika pande zote mbili, yaani Wizara ya Kilimo na Wizara inayohusika na Maji.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 159 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa kufuatilia kwa karibu hali ya mazingira ya upatikanaji wa maji katika mabonde ya mpunga. Vile vile napenda kumfahamisha kwamba hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa kukauka kwa maji ya mito na uchimbaji wa visima kama vianzio vya maji ya matumizi ya majumbani.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba upungufu mkubwa na ukaukaji wa maji uliojitokeza katika maeneo mengi ya mabonde umechangiwa na uharibufu wa vianzio vya mito na chem chem. Uliotokana na shughuli za kibinadamu ikiwemo ujenzi wa nyumba za kuishi, ukataji wa miti kwa uchomaji wa makaa na kuni kwa lengo la kujipatia kipato na hata kazi za kilimo ambapo huchangia kuharibu kivuli cha njia za mito. Hata hivyo, mabadiliko ya tabia ya nchi yamechangia kupungua kwa upatikanaji wa mvua ambao una mahusiano makubwa na ukaukaji wa mito.

Mhe. Spika, nakiri ya kwamba zao la mpunga kwa kawaida huwa linahitaji maji mengi sana kwa hivyo hali ya upungufu wa maji inachangia kiasi kikubwa cha upungufu wa mavuno ya mpunga.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako kwamba wizara yangu inamashirikano makubwa ya kitaalamu na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Maendeleo ya Makaazi. Kimsingi huwa tunawasiliana na Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) katika hatua za awali za uchunguzi wa upatikanaji wa maji pamoja na kushauriana namna ya kufanikisha kazi za uchimbaji kwa ujumla.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa vile nia ya serikali ni kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kwa kuwa vianzio vingi vya vimekauka. Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kilimo kwa njia ya umwagiliaji maji kinafanikiwa hapa kwetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ni sahihi kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga na kujidhatiti katika kuendeleza kilimo kwa kauli mbiu yetu ya Mapinduzi ya Kilimo ikiwemo umwagiliaji maji, kwa maana kilimo bila ya maji hakiwezi kuendelea tunahitaji maji kwa ajili ya kumwagilia zao letu la mpunga, tunahitaji maji kwa ajili ya viungo, mboga mboga na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wizara yangu pia inasimamia masuala ya maliasili, hivyo tumedhamiria kuendeleza na kuimarisha misitu yetu. Pia kuendeleza upandaji wa miti katika maeneo nje ya misitu ambapo vianzio vingi vya maji vinapoanzia. Hivyo tutaendelea pia na jitihada ya kuwaelimisha wananchi na pia kudhibiti matumizi mabaya ya misumeno ya moto na uvunaji kiholela wa rasilimali zisizorejesheka hasa za misitu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa nchi yetu ya Zanzibar inatakiwa angalau iwe na vipindi viwili vya mvua na kwa kuwa mvua zinazonyesha maji yake huwa yanapotea bure hayatumiki zaidi kwa kilimo. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kukuza hii taaluma ya kuvuna maji ya mvua ili yaweze kutusaidia katika siku za baadae.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kama nilivyokwishaeleza kilimo bila ya maji hakiwezekani, miongoni mwa mipango yetu ni kuyasimamia mageuzi makubwa ya kilimo ni uvunaji wa maji ya mvua ili yasipotee. Kwa bahati nzuri pia nimemsikia mara kadhaa hapa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba na wao kwa upande wao wanautaratibu ambao wanakuja nao wa uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya majumbani pamoja na kusaidia sekta ya kilimo. Kwa hivyo, naamini wizara hizi mbili kwa mashirikiano ya karibu tuliyokuwanayo na mipango ambayo tuaanza nayo katika mwaka huu wa fedha, tutaanza kuelekea katika hatua za awali za kuanza kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya sekta ya kilimo na sekta nyenginezo.

Nam. 5

Wanafunzi wa Wazee Wasio na Uwezo
Kurudishwa Nyumbani kwa Kukosa Ada

(Mheshimiwa aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 87

Bei Ndogo ya Mwani

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Katika maeneo mengi yaliyo karibu na bahari , wakaazi wengi waliokaribu na bahari hasa wanawake wajajishughulisha na kazi za ukulima wa mwani ikiwa ni kazi yao ya kujipatia riziki za halali. Kazi hii ni ngumu sana na malipo yake

ni madogo kulingana na kazi yenyewe. Hivi sasa kilo moja ya mwani mkavu inauzwa kati ya shilingi 250/= hadi 300/= bei ambayo ni ndogo sana na inavunja moyo. Pamoja na hali hiyo ngumu wananchi inawalazimu kuifanya kazi hiyo kwani hawana kazi nyengine mbadala.

(a) Je, Mhe Waziri ni sababu zipi zinazopelekea kuweko kwa bei ndogo ya zao hili.

(b) Bei halisi ya kilo moja ya mwani mkavu ni ipi katika soko la dunia.

(c) Wenye makampuni ya mwani wanadai kuwa bei ndogo ya mwani inasababibishwa na ushuru mkubwa wanaolipia serikalini wanapoingiza vifaa vya kilimo hicho. Je, Serikali haioni ulazima wa kupunguza au kuondosha kabisa ushuru wa vifaa vya ukulima wa mwani ili wakulima wapate bei nzuri kwa kazi yao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba ukulima wa mwani ni moja kati ya shughuli muhimu ya kiuchumi hapa Zanzibar inayochangia katika pato la Taifa, takwimu sasa zinaonesha uzalishaji wa mwani hapa Zanzibar umefikia tani 12.5 elfu kiwango ambacho kikubwa kuliko nchi nyengine nyingi katika Bahari ya Hindi. Na pia sasa ubora wa mwani wetu ni wa kiwango kikubwa kuliko mwani wa nchi nyengine nyingi. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wakulima wa mwani hapa Zanzibar hasa wanawake kwa jitihada zao za kuzalisha mwani katika kiwango bora. Wizara yangu kupitia Idara ya Mazao ya Baharini imemteua Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Mwani hapa Zanzibar akiwa ni Mwanamke, na jitihada zake za kuwakomboa wanawake wenzake wanaolima mwani zimeanza kuzaa matunda mazuri.

a) Sababu kubwa inayopelekea kuweko kwa bei ndogo ya zao la mwani hapa Zanzibar ni:

i) Mwenendo na uhalisi wa thamani za bei ya bidhaa ambayo ni mahitaji ya bidhaa na kuwepo kwa bidhaa katika soko yaani *supply and demand theory*.
ii) Kuuza mwani ambao haujafanyiwa usarifu.
iii) Kuuza mwani kupitia soko dogo.

(b) Bei halisi ya kilo mmoja ya mwani mkavu katika Soko la Dunia hutegemea aina ya mwani, kwani kuna zaidi ya aina tano ya mwani unaouzwa katika Soko la Dunia mwani aina ya *Spinosum* ambao unazalishwa kwa wingi hapa Zanzibar ndio mwani wenye bei ndogo ambao utafiti uliofanywa na idara yangu, bei ya mwani ya *Spinosum* ni baina ya shs. 800 hadi 900 katika Soko la Dunia.

© Sio kweli kwamba bei ndogo ya mwani inasababishwa na ushuru mkubwa wanaoilipia Serikali wanapoingiza vifaa vya ukulima wa mwani. Wazo la kupunguza ushuru au kusamehe kabisa ushuru tumelipokea na tumeanza kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo utekelezaji wake utakua na ufanisi mkubwa ikiwa lile lengo la wizara yangu ya kuwahimiza wakulima wa mwani wajiundie jumuiya zenye nguvu za ukulima wa mwani nchini ambazo zitashughulikia, vifaa vya ukulima wa mwani ikiwezekana kueka maduka ya jumuiya zao.

- Teknolojia ya ukulima wa mwani, ukaushaji wake na ubora wake
- Usarifu wa mwani, bei na soko lake.

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko tayari kushirikiana na jumuiya hizo pindi zitakapoanzishwa na kuimarishwa kwa maslahi ya wakulima wa mwani hapa nchini.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Hivi karibuni katika kijiji cha Jambiani alikuja tajiri alikuwa ananunua bei ya mwani kilo shilingi mia nne badala ya mia mbili na hamsini, na tajiri huyo nasikia kwamba wizara yako imempigia marufuku kununua mwani huo. Je, hili suala ni kweli na ikiwa ni kweli ni kwa sababu gani mkamzuia.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nataka nimpongeze kwa kuniuliza hili swali kwa sababu nilitegemea kama litakuja. Mhe. Spika, mwishoni mwa mwezi wa 5 na mwanzoni mwa mwezi wa 6 wizara yangu ilikuwa ikipokea simu mbali mbali kutoka kwa wananchi kuhusiana na suala hili. Mhe. Spika, kwa uzito wa suala hilo imebidi tufanye kazi kubwa ya kulifuatilia na kwa sababu nilitegemea ama litakuja katika suala hili au katika bajeti yangu naomba unipe nafasi kidogo nimuelezee kwa kina Mhe. Mwakilishi suala hili.

Mhe. Spika, mnamo siku ya Jumapili ya tarehe 22, Mei wizara ilipata taarifa ya kutokea mnunuzi wa mwani katika kijiji cha Jambiani kwa bei ya shilingi 400 kwa kilo badala ya shilingi 250. Wakulima wa mwani wamefurahia sana kutokea kwa mnunuzi huyo kutokana na bei yake nzuri, taarifa za mnunuzi huyo hazikuwa zinajuulikana katika ngazi yoyote ya utendaji wa serikali, jambo ambalo lilileta wasi wasi kwa watendaji na hata kutoa picha mbaya kwa hatima ya kilimo cha mwani nchini. Baada ya taarifa hii Idara ya Mazao ya Baharini ilifuatilia katika eneo husika ili kuthibitisha taarifa hiyo.

Mhe. Spika, madhumuni au lengo la ufuatiliaji huu ni kutaka kujua taarifa za kampuni inayonunua mwani katika maeneo ya Jambiani kuhusu jina la kampuni kujua kama imesajiliwa au laa, kama imesajiliwa kuona waraka wa usajili wao, kama haijasajiliwa kuelimisha taratibu zilivyo kuhakikisha kuwa bei wanayoitangaza ndio wanayonunulia.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 24, Mei mwaka huu timu ya watendaji wa Idara ya Mazao Baharini ilikwenda Jambiani kuonana na kufanya mazungumzo na Sheha wa Shehia ya Jambiani Bwana Ali Mtumwa ambaye kwa wakati huo shughuli za ununuzi wa mwani zilikuwa zinaendelea katika shehia yake. Alieleza kuwa ni kweli kwa bahati yeye amewaona watu wala hawajui wala hajasikia taarifa zao ambao wananunua mwani kwa bei hiyo. Mhe. Spika, watu hao walianza kununua kuanzia tarehe 15, Mei 2011 katika Shehia ya Jambiani Kikadini.

Mhe. Spika, Sheha wa Shehia ya Kibigija alizipokea taarifa hizi kutoka kwa Bwana Haji Vuaa ambaye ni mnunuzi wa mwani wa Kampuni ya Zanzibar Shell pia msaidizi wa Sheha ya Kikadini vile vile ni Katibu wa Kamati ya Wakulima wa Mwani wa Jambiani. Sheha aliendelea kueleza kwamba siku ya Jumapili ya tarehe 22 Mei, 2011 alipokea simu kutoka kwa Sheha mwenzake wa Shehia ya Kikadini kwamba hawa wanunuzi watakwenda kununua mwani Kibigija siku ya Jumanne ya tarehe 24, Mei.

Mhe. Spika, baada ya kuonana nao aliwauliza kuhusu vibali alivyowaruhusu akawa hana kibali na hili ni tatizo. Kwa hivyo, idara yangu kazi iliyofanya iliwaambia kwamba lazima wafuate utaratibu kama wenzao wanaofanya. Mhe. Spika, utaratibu wameufuata na sasa wameanza kununua kwa bei ya shilingi 400 Unguja na Pemba. Kwa hivyo, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mnunuzi huyo hakuzuiliwa lakini alifuatwa ili afuate utaratibu kama wenzake wanaofuata na kwa sababu utaratibu ameshaufuata sasa mwani unanunuliwa kwa shilingi 400 nchi nzima badala ya shilingi 250 ongezeko la asilimia 90 hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wizara yangu nawaomba sana wakulima wa mwani bei nzuri waliyoipata waitumie kwanza kwa kuhakikisha kwamba wanaendeleza ukulima kwa kiwango bora. Lakini pia wahakikishe kwamba sasa wanaanza kujinunulia vile vifaa ambavyo vinatokana na ukulima wa mwani badala ya kuwategemea makampuni.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huoni sasa wizara yako ina haja ya kuwanunulia hawa walimaji wa mwani machine ya kukaushia na wakaweza kwenda kuuza wenyewe kwa kuondoa umasikini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kwamba wazo lake ni zuri lakini wizara yangu hivi sasa haijuilishi moja kwa moja na ukulima wa mwani. Hilo ni suala la wananchi na jumuiya zao na kupitia pia kwa makampuni ambayo yanajishirikisha katika ukulima na ununuzi wa mwani. Kwa hivyo, wazo lake zuri tutalichukua na tutawashauri wote wanaohusika kushughulikia katika suala la kutafuta machine za kukaushia mwani ili liwe na kiwango bora.

Nam 33

Utaratibu wa Kuchangia Huduma za Uzazi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna utaratibu wa kinamama waja wazito wanaokwenda kujifungua kuchangia huduma kwa kutakiwa kununua baadhi ya vifaa vinavyotumika wakati wa kujifungua. Ingawa utaratibu huu sio mbaya sana.

(a) Je, Mhe. Waziri, inakuwaje ikiwa mjamzito alieletwa kujifungua hana uwezo wa kujipatia vifaa hivyo.

(b) Kwa kuwaondoshea usumbufu kinamama wajawazito katika wakati mgumu wa kujifungua, kwa nini serikali isichukue hatua muafaka za kuwaondolea ulazima wa kuchangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama nilivyo tangulia kujibu suala kama hilo katika vikao vya Baraza hili vilivyopita kwamba hakuna mtu atakae kosa au kunyimwa huduma kwa kuwa hana uwezo. Iwapo atatokea mjamzito kama huyo ambaye hana uwezo wa kujipatia vifaa wakati wa kujifungua, basi mzazi huyo atahudumiwa kwa kutumia vifaa vya dharura.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu imo mbioni kutayarisha mpango madhubuti wa kutafuta vyanzo vya upatikanaji wa rasilmali ikiwemo nyenzo na vifaa vya kutolea huduma. Hali ikiruhusu uwezekano wa akinamama hao na wengine wasio na uwezo hawatachangishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Dada yangu Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kuwa bado hilo tatizo linaendelea kuhusu wazazi wetu na wanafika kuweka vitu vyao rehani kwa kupata huduma hiyo. Mhe. Spika, kama hana taarifa hiyo basi nakupa hiyo taarifa kwamba hali bado inaendelea na wazazi wetu wanapata shida.

b) Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri anatwambia yuko mbioni kwa muda mrefu katika majawabu yako, mbio hizo zinaanzia wapi na zitamalizikia wapi kama Hospitali ya Makunduchi inatoa huduma bure kwa matibabu yote. Je, hatuwezi kufuata mfano huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hiyo taarifa ya rehani ndio kwanza naisikia leo nitaifanyia kazi niulizie nijue kama hicho kinaendelea na hao utapoa amewapa nani ruhusa kuweka rehani wakati nchi hii hairuhusu rehani. Mhe. Spika, mbio zangu zitaishia pale serikali itakapokuwa na uwezo na pale nitakapozipata nyenzo kama nilivyosema. Moja ya mbio kuishia ikiwa kesho tukijaaliwa mtaipitisha bajeti bila ya kikwazo tutapata nguvu za kutafuta fedha ili kuyaondosha yote hayo.

Mhe. Spika, kuhusu Hospitali ya Makunduchi kutoa huduma bure mimi nakubaliana na yeye sio tu kuzalisha inawafuata wagonjwa mpaka majumbani, imetoa mpaka namba za simu. Mhe. Spika, kinachoendelea pale ni kwamba pana wafadhili ambao Wizara ya Afya imewatafuta na wako pale kwa ajili ya kutoa huduma zile kama majaribio kwa sababu tunataka Hospitali za Wilaya zifuate utaratibu ule. Kwa hilo ile ni *pilot projective* na ni *pilot* nzuri na ikiwa itafanikiwa na kwengine kote nchini itafanikiwa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika Hospitali ya Chake Chake Pemba huwa kinamama hao baada ya kujifungua wanadaiwa shilingi 1000 kwa ajili ya kulipia kitanda. Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako inalijua hilo na kama analijua malipo hayo huwa yanaingia kwenye kifungu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kitanda hakiko katika sehemu ya kuchangiwa tunachochangisha ni vifaa vya huduma ya kuzalia. Kwa hivyo, kama hospitali hiyo wanachangisha hilo katika *list* niliyoikuta katika wodi ya Chake-Chake hiyo haikuwepo. Kwa hivyo, mimi sina uhakika kama suala hilo lipo, lakini nitalifuatilia niwe na uhakika ikisha niwaulize wanazitia katika mfuko upi na nani kawapa ruhusa kuchangisha kitanda.

Mhe. Ali Salim Haji: Ahsante Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la uzazi ni suala nyeti sana ambalo linapelekea watu wanapopeleka wajawazito kutokuondoka kutokana nakusubiri hali ya mazingira ya wajawazito wao, suala ambalo limepelekea wanaowapeleka watu wale hualala mpaka chini ya ngazi na chini ya milango jambo hilo linaleta usumbufu kwa watu ambao wanahitaji kupeleka wagonjwa juu. Kwa kuwa hospitali yetu ilijenga eneo maalum la kukaa watu kwa ajili ya dharura za wagonjwa kupitia mlango mkuu.

Je, wizara haioni kuna haja ya kufungua mlango ule na watu kukaa katika kibanda kile maalum.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, anayoyasema Mhe. Mwakilishi ni kweli na ukizungumza habari ya kuzaa nafikiri mimi naumwa kwa sababu naujua uchungu. Sehemu unayoizungumza haikufungwa isipokuwa imebadilishwa matumizi yake, pale sasa hivi utaratibu ulikuwa ni wakuanzisha ma-*file* kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, sehemu ile kama unavyoifahamu Mnazi Mmoja sehemu zilizopo kila siku tunabadilisha hiki lakini pakupanua hamna na ma-*file* yanahitaji kuwekwa.

Mhe. Spika, utaratibu unatakiwa kuanzishwa kwa hiyo sehemu ile itakubalika kwamba ibadilishwe matumizi yake ili yawekwe ma-*file.* Lakini hata hivyo tuko mbioni na tumeshapewa ruhusa na Manispaa kujenga sehemu ya dharura ambayo haitokuwa ya kukaa pale watakapohitaji tuondoshe mbele ya hospitali katika bustani. Kwa hivyo, tumetafuta wafadhili tofauti na wako waliokwishakuahidi kwamba watatupa ili tujenge halafu tuweze kuwaondoa watu mle wanamokaa ili waweze kusubiri nje.

Nam. 148

Kuwawezesha Wananchi wa Micheweni

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Je, serikali haioni kwamba iko haja ya kuwawezesha zaidi wananchi waliomo ndani ya Wilaya ya Micheweni ambayo hali ya kijiografia na kiuchumi ni ngumu zaidi kati ya Wilaya 10 za Zanzibar kwa mujibu wa ripoti mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 148 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ripoti za Mapato na Matumizi ya Kaya zimeonesha katika vipindi tofauti kuwa kwa ujumla kuna kiwango kikubwa cha umaskini hapa Zanzibar, na hali hiyo ni mbaya zaidi katika Wilaya ya Micheweni ukilinganisha na Wilaya nyengine.

Mhe. Spika, juhudi mbali mbali zimechukuliwa na hasa juhudi za makusudi zilielekezwa Wilaya ya Michezweni ili kupunguza tatizo hilo kiuchumi na umaskini. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imekuwa ikitekeleza programu ya pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa (JP.5) kupitia programu ya Mpango Maalum wa kuiendeleza Wilaya ya Micheweni kiuchumi na kijamii.

Mambo mengi ya maendeleo yametelekezwa ndani ya Wilaya ya Micheweni katika kipindi hicho ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi watoa huduma na Kituo cha Afya Maziwa Ng'ombe, ujenzi wa Skuli ya Chekechea na kuanzisha mpango wa kuwapatia chakula hapo hapo skuli, mradi wa maji safi na salama, ujenzi wa vyoo, kusaidia zaidi ya familia 93 na kuanzisha Radio Jamii ya Mcheweni.

Mhe. Spika, aidha katika jitihada za kuwawezesha wananchi wa Micheweni vikundi mbali mbali vimesaidiwa kuanzisha shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kilimo na ufugaji. Kisima kimechimbwa katika bonde la Saninga ili kuimarisha umwagiliaji na kuongeza uzalishaji. Hayo yote yametekelezwa kupitia programu moja tu ya JP.5, yako mengi yanayo endelea lengo hilo hilo la kuwawezesha wananchi wa Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali kama ambavyo imeona umuhimu wa kuwawezesha wananchi wa Wilaya zote za hapa na hasa Wilaya ya Micheweni, itaendelea na juhudi hizo na kwamba wananchi wa Wilaya hiyo ni miongoni mwa walengwa wakuu wa mipango yote ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, hivi karibuni Mhe. Rais aliagiza wizara tatu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayoongozwa na Mhe. Said Ali Mbarouk, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaongozwa na Mhe. Omar Yussuf Mzee na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inaongozwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman kwenda kuona hali kwa lengo la kuishauri ipasavyo Wilaya hiyo. Naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi hizo za serikali yetu inalengo la kuwaondolea matatizo wananchi na hali ngumu ya kimaisha.

Serikali ya awamu ya saba inayoongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein, inajali wananchi wake. Tutaendelea kuwasaidia wananchi popote pale walipo kwa lengo la kuwaondolea umasikini

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba ni mpango wa serikali kusaidia Wilaya yote katika masuala ya kujipatia kipato na kuinua uchumi. Kwa kuwa Wilaya ya Chake-Chake hususan katika vijiji vya Kibokoni, Wawi, Vitongoji na Furaha, tayari wameanzisha miradi midogo midogo kama vile ufugaji, nyuki, ufugaji wa samaki, pamoja na kufungua *SACCOs* mbali mbali.

Je, Wizara yake ina mpango gani wa kutembelea vijiji hivi kufudi kwenda kuona jitihada za wananchi katika suala zima la kuinua kipato chao.

Mhe: Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi, Kiuchumi na Ushirika: Mher. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu mama, tunakusudia kuwawezesha wananchi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na tumejipanga vizuri. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi wakae mkao wa kuondokana na umasikini Ishallah.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba uniruhusu kumuuliza Mwalimu wangu Mhe. Waziri wa Uwezeshaji swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atusaidie katika hiyo Ripoti ya Uchunguzi wa Kaya kama inavyoitwa ya Zanzibar. Ni asilimia ngapi ya wananchi wa Zanzibar wanaoishi chini ya kiwango cha dola moja kwa siku. Yaani waliokuwepo chini ya *property line*.

Katika kuwasaidia hao kutokana na majibu yake kwamba sasa serikali itaumaliza umasikini na Wawakilishi tukae mkao wa kupunguza umasikini au kuuondoa. Serikali imepanga mwaka huu kutumia kiasi gani katika fungu la kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuufuta umasikini huu uliotajwa katika ripoti.

Mhe: Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi, Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, takwimu halisi nitamletea kwa maandishi suala lake la mwanzo.

Kuhusu bajeti katika upande wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, wizara yangu imetenga kwa ujumla karibu shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya suala hiko. Lakini pia kupitia mabenki kwa utaratibu wa mikopo ya AK na JK kuna kiasi cha bilioni 2 ambazo sasa hivi zimeanza kutolewa na zitaendelea kutolewa.

Pia napenda nihakikishie Mhe. Mwakilishi Ismail Jussa pamoja na Wawakilishi wengine. Serikali hii ya awamu ya saba itaendelea kutafuta njia mbali mbali kuptia mabenki na kwa washirika wengine wa maendeleo ili kuweka mfuko maalum ambao unakusudia katika kipindi cha miaka mitano kupunguza kwa asilimia kubwa tatizo kubwa la umasikini katika nchi yetu.

Nam. 27

Barabara ya Kichangani-madungu

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kichangani hadi Madungu iliyopo Jimbo la Wawi, haizidi Kilomita mbili. Na kwa kuwa ni miongoni mwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami mara baada ya Mapinduzi ya 1964, kwa hivyo kubakia kama barabara ya kihistoria. Barabara hiyo kwa sasa haipitiki na kusababisha usumbufu mkubwa wa usafiri na usafirishaji baina ya maeneo ya Wawi na Soko kuu la Chake-Chake.

Je, ni lini Serikali itafikiria kufanya matengenezo makubwa ya barabara hiyo badala ya kuendelea kuitelekeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli barabara ya Kichangani – Madungu iliyopo Jimbo la Wawi haizidi kilomita mbili, na ni kweli barabara hiyo ni miongoni mwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatumbua kwamba barabara hiyo kwa sasa iko katika hali mbaya na inawaletea usumbufu watumiaji wa barabara hiyo. Hata hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako Tukufu kuwa Wizara yangu itaifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo hapo hali ya fedha itakapo ruhusu.

Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti na mahitaji yalivyo makubwa kwa wananchi wetu hasa kwa huduma ya barabara kwa wananchi wanaoishi eneo la Wawi, Wizara yangu kwa kupitia mfuko wa barabara imepanga kufanya matengenezo na ukarabati mkubwa wa kiwango cha kifusi kutoka eneo la Wawi hadi eneo la Mgogoni kwa kuikarabati barabara hiyo ili iweze kupitika na watu wote. Hii ni kutokana na idadi na matumizi makubwa na umuhimu kwa maeneo hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nashukuru kwa kufanya matengenezo barabara ya Wawi mpaka kufikia Mgogoni. Lakini suala la msingi lilikuwa ni barabara ya kihistoria ya kutoka Kichangani mpaka Madungu.

Kwa kuwa barabara hii ilijengwa kwa ule utaratibu wa Afroshirazi wa kujitolea tena chini ya usimamizi mkali wa Mhe. Rashid Abdalla Mamba na kwa kuwa sasa hivi serikali yetu haina uwezo wa kuchonga masanamu wala kujenga minara ya kumbukumbu kwa viongozi wetu hawa waasisi. Je, ni lini barabara hii itajengwa katika kiwango cha lami pamoja na kuwekwa taa za barabarani na hatimaye kupewa jina la biti Fehemu road ili kuwaenzi wazee wetu pamoja na jitihada za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, dhamina na malengo ya mapinduzi ni kuboresha huduma na maisha ya wananchi wa Zanzibari. Dhamira na lengo la Mhe. Mwakilishi ni zuri la

kutunza na kuendeleza waasisi na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu mama kikwazo hapa ni uwezo lakini dhamira ya serikali ni kutengeneza mipango yote ili kurahisisha huduma na kuboresha maisha ya watu wa Zanzibar. Imani yangu kwamba Serikali ikipata uwezo basi tutatekeleza na tutafanya barabara hiyo kwa lami kama hali itakavyoruhusu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda nimuulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa tulipata taarifa kwamba kuna utaratibu wa upimaji wa maeneo yanayopita barabara Unguja na Pemba ili kujulikana zile barabara zilizopo na zile zinazo hitaji matengenezo. Kutokana na uchache wa viunganishi vya njia kwa njia za Pemba ni chache na sasa mafuta ni ghali. Je, katika kujiondolea umasikini utaratibu huu unaendelea kwa Pemba katika kupimwa njia ambazo zingewarahisishia watu katika maeneo mbali mbali kupata njia nyepesi na rahisi kama mtandao ulivyojengwa hapa sasa hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli alivyoeleza Mhe. Mwakilishi dhamira ya kuongeza. huduma ya *feeder roads* kwa ajili ya kuondoa usumbufu dhamira hiyo tunayo na tumekuwa tukifanya hivyo kadiri ya upatikanaji wa fedha kwa kushirikiana na wenzetu wa mfuko wa barabara. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kadri ya bajeti ya Wizara yetu pamoja na wenzetu wa mfuko wa barabara itakavyoweza kuruhusu basi ndivyo tutakavyoweza kuwasaidia wananchi wetu katika kupata huduma hii muhimu na adhimu.

Nam. 154
Kuporomoka kwa Maadili

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar tunayo maadili yetu ambayo ni kinga tosha dhidi ya maradhi ya ukimwi na zinaa, mimba za utotoni na ukahaba. Lakini kwa kuwa Serikali hailisimamii vya kutosha suala la maadili kwa kisingizio cha uhuru binafsi, leo hii athari zake zinaonekana wazi wazi.

(a) Kwanini Serikali hailifatilii na kuchukua hatua ya kudhibiti maeneo yanayoendesha biashara ya ukahaba na kuwachukulia hatua washiriki

wa vitendo hivyo au na hili ni haki yao hata kama ni kinyume cha maadili yetu.

(b) Kwanini Serikali haiweki muongozo wa mavazi yanayoendana na utamaduni na maadili yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 154 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe Spika, kwa upande wetu tunawajibika kuwaelimisha watu juu ya kufuata maadili ya Mzanzibari kupitia Kamisheni yetu ya Utamaduni na Michezo na vitengo vyake kwa kutumia vikundi mbali mbali vya sanaa ngoma na maigizo na vikundi vya Taarab, pamoja na vyombo vya Habari. Hata hivyo, Mhe. Spika bado Wizara yangu haina mamlaka kamili juu ya udhibiti wa jambo hili kwa kuwa kuna mamlaka nyengine zinazoweza kusimamia maadili ya Mzanzibari vikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama. Halmashauri ya Mikoa na Wilaya pamoja na taasisi zinazosimamia malezi ya wanajamii.

(b) Mhe. Spika, miongozo kuhusu mavazi yanayoendana na utamaduni na maadili ya Mzanzibari yapo kisheria lililobaki ni jukumu la vyombo vinavyohusika kusimamia sheria ya nchi. Mfano: Muongozo wa kutokuvaa nguo fupi kwa wenyeji na wageni wanaoingia nchini, katika viwanja vya ndege.

(c) Bandari kulikuwa na maafisa maalumu ambao walikuwa wanatoa maelekezo kuhusu mavazi yanayoendana na muongozo mwengine mzuri wa mavazi Zanzibar unaotokana na mwenendo mzuri wa jamii unaoathiriwa kutoka kizazi hadi kizazi tangu mtoto anapozaliwa hadi anapokuwa mkubwa na kujitegemea mwenyewe, muongozo huu wa kivazi haufungamani na matoleo au makatazo ya Serikali bali inatokana na mafunzo tunayopata kwa wazee wetu na kwa dini zetu.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika jibu lake mama amesema zamani kulikuwa kuna maafisa maalum bandarini ambao wanaelimisha mavazi yetu ya kizanzibari. Je, Mhe. Waziri huoni ipo haja ya maafisa wale warejee tena bandarini ili watoe elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli kwenye suali mama nimesema kuwa suala hili lilikuwepo zamani lakini Wizara yangu kwa kushirikiana na serikali pamoja na vyombo vya sheria tualifuatilia ili kulirudisha hapo hapo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, katika uongozi wake muasisi wa taifa hili Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alikuwa jasiri na alithubutu kupiga marufuku uvaaji wa buga, suruwali za chupa na kufuga manywele marefu kwa maana ya afro, hata kupiga marufuku uganga wa kienyeji. Kwa nini viongozi wa leo wanashindwa kuwazuia wanawake kuvaa nguo fupi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mimi nina historia fupi kwa sababu miaka hiyo na mimi nilikuwa mwanafunzi, kweli serikali ilikataza lakini sasa hivi kama unavyojua utandawazi ndio unaotupelekea kuvaa mavazi ya sasa. Kama unavyojua huwezi kukosa utandawazi. Wewe Mhe. Mwakilishi mwenyewe ndio unaetakiwa ili uwaelimishe jamii wavae kivazi ambacho kinatakiwa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa mavazi ni miongoni mwa utamaduni uliozoewa sana hapa Zanzibar. Na kwa kuwa kuna baadhi ya wizara inawafanyakazi wafanyakazi wao wapunguzi baadhi ya mavazi ambayo wameyazoea kwa mfano Wizara ya Elimu. Je, unatoa wito gani kwa kuwa suala la mavazi ni miongoni mwa utamaduni na Wizara yako ni miongoni kwa kusimamia masuala haya. Unatoa wito gani kwa wafanyakazi hawa na viongozi wao katika wizara zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli serikali pamoja na Wizara zetu zimepanga utaratibu mzuri wa kuhusu mavazi hasa sisi wanawake. Kama unavyotuona Baraza la Wawakilishi basi na ofisini kwetu huwa tunavaa mavazi haya haya mazuri na yenye kutustiri sisi wanawake. Na upande wa wanaume na wao vile vile wana mavazi yao kama hivyo Mheshimiwa ulivyo na wanaume huwa wanavaa hivyo hivyo.

Nam. 69
Ukosefu wa Maji Safi Mjini/Magharibi

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Licha ya kukamilika kwa Mradi mkubwa wa Maji katika Mkoa wa Mjini na Magharibi uliogharimu mabilioni ya shilingi, wananchi wa Shehia ya Sogea,

Nyerere na Kwawazee katika Jimbo la Magomeni hadi leo hawajaweza kupata huduma ya maji katika maeneo yao.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea wananchi hawa kukosa maji katika maeneo yao licha ya mradi huu kukamilika.

(b) Huoni kwamba kuendelea kukosa maji kwa wananchi hawa huku wenzao wa maeneo mengine wakipata huduma hii kunawatia unyonge.

(c) Ni lini Serikali yao, itawaondoshea unyonge huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba matarajio ya wananchi wengi ni kwamba, kukamilika kwa Mradi mkubwa wa Maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi kungeliondosha kabisa tatizo la maji katika Mkoa huu. Lakini kutokana na uchakavu wa mtandao wa maji, kuharibika kwa mitambo ya kusukumia maji pamoja na kuchafuliwa kwa vianzio vya maji ni miongoni mwa sababu za kuwa na pupungufu wa maji baadhi ya maeneo ya Mkoa huo na hasa katika eneo la Jimbo la Magomeni.

Mhe. Spika, ni kweli kukosekana kwa maji kunatia unyonge mkubwa lakini serikali kupitia wizara yangu tayari imeshachimba kisima kipya karibu na nyumba za wazee Sebleni ili kuongeza nguvu za maji katika maeneo ya Semiso.

Mhe. Spika, tatizo hilo litaondoka baada ya kumalizika kwa matengeneo ya kisima hicho.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nishukuru kupata nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na nimshukuru ndugu yangu Mhe. Salmini kwa kuanza kuuliza alipomalizia herufi ya mwisho So, Sogea kwa jimbo lake lakini mradi huu umeanzia na Semuso (Sebleni, Muungano Jimbo la Kwahani) na kwa fida yangu wanchi wa jimbo la Kwahani kwa sababu tunakabiliwa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani niishukuru serikali kwa jitihada yake. Lakini namuomba Mhe. Naibu Waziri atuhakikishie je, zoezi hili linaweza kukamilika hivi karibuni ili wananchi ukifika mwezi wa Ramadhani waweze kuondosha matatizo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Wizara yangu iko katika matengenezo, siwezi nikasema lini lakini namuomba Mhe. Mwakilishi awaweke sawa wananchi wake na wajitayarishe kuyatumia maji haya. Jitihada za wizara yangu zinaonekana na tutajitahidi ndani ya kipindi hichi cha karibuni tuweze kukamilisha zoezi hilo.

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Katiba na Sheria
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizira ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2011/2012)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyowaomba jana kwamba asubuhi ya leo tupate michango ya Muheshimiwa Mwanasheria Mkuu na kuna mchango wa Mhe. Waziri wa Masuala ya Fedha. Niwaombe radhi sana wale ambao wameomba nafasi za kuchangia ambao ni kama hawa wafuatao:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Salim Abdalla Hamad
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Hamza Hassan Juma

Marejeo yalikuwa ni mengi na wasaa mwengine kidogo utakuwa mgumu kama wataweza kupeleka kwa maandishi basi itasaidia vile vile. Lakini naomba radhi sana kwamba hatutoweza kupata nafasi. Basi sasa nimkaribishe Mhe. Othman Masoud ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nikushukuru na wewe binafsi kwa kunipa wasaa wa kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Kwanza na mimi niseme kuna wajumbe wengi ambao.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuelewe kwamba mchango wa Waheshimiwa hawa ni sehemu ya majumuisho. Wakati mwengine huwa inaleta tabu waheshimiwa wakiwa hawapo au hawakusikia hatimaye inabidi Waziri arejee wakati tayari maelezo yamekwisha kutolewa ya kutosha. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba wajumbe wengi wamenipa pongezi kwa kazi niliyoifanya huko nyuma kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Afisi ya Mashtaka na pia kwa uteuzi katika nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu.

Mimi naomba niwaahidi kwamba shukurani zao, pongezi zao ni deni na naomba niwaahidi Mhe. Spika, kwamba nitalilipa na faida na sio na riba. Na Ishallah Mungu ataniwezesha kufanya hivyo.

Suala jengine nizungumzie kuna hoja baadhi baadhi ya taasisi ambazo zimezungumzwa. Nianze na suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa wengi kidogo kuhusu Mahakama katika suala la ucheleweshaji wa kesi.

Mhe. Spika, niseme kwamba kweli hili bado ni tatizo. Suala la ucheleweshaji wa kesi ni kama mkufu. Bado nakumbuka maneno ya Mhe. Iddi Pandu aliyekuwa Mwanasheria Mkuu mara nyingi alikuwa akilieleza suala hili. Kwamba katika kesi kama ni ya jinai kwanza kuna upelelezi, na upelelezi una hatua nyingi. Kuna suala la kupata mashahidi, mara nyingi linaleta matatizo. Kuna suala la mshtakiwa mwenyewe nalo wakati mwengine linachelewesha. Kuna suala la kesi kama ina mawakili nalo pia ni tatizo. Juhuzi zimechukuliwa katika kupunguza hili .

Mhe. Spika, wengi naamini watakubaliana na mimi kwamba hili tatizo kama tungekuwa tunafanya tathmini kina basi tungegundua kama limepungua. Mara nyingi kunapokuwa kuna mashirikiana ya wote hao basi unakuta kesi inakwenda kwa haraka zaidi.

Mfano mzuri Mhe. Spika, kesi tuliyokuwa nayo ya kuchomwa kwa msahafu. Kesi ile haikufika miezi mitatu, tokea ilipoanza kusikilizwa mpaka ilipotolewa hukumu. Kwa sababu wote hawa walishirikiana kuanzia upelelezi, mashahidi kuna watu walijitolea wenyewe kwenda kufuata baadhi ya mashahidi waliokuwa Morogoro na kesi ikaweza kusikilizwa ndani ya miezi mitatu ikatolewa hukumu.

Kwa hivyo ni ushahidi kwamba panapokuwa na mashirikiano ya karibu basi kesi haina sababu ya kuchukua muda mrefu. Mara nyingi tatizo linakuwa katika mkufu huu hivi vipande kukaa pamoja.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa Mhe. Ali Salim alisema kuhusu suala la mahabusu kuwa wengi. Nalo tutakubaliana kwamba hili tatizo limepungua kwa kiasi kikubwa. Limechangiwa kuendelea kwa sababu tuna tatizo, wengi utakaowakuta Mahabusu wapo ndani. Siku hizi dhamana ukenda mara nyingi

mtu anapata kama anao wadhamini. Wengi utakaowakuta wapo ndani ni watu ambao au ni washtakiwa ambao hata jamaa zao wamewasusa, kwamba sisi tumeshindwa. Kwa hivyo hayupo mtu wa kumchukulia dhamana. Mara nyingi hawa wakipewa dhamana wanakuwa hawarudi na hawapatikani tena. Hii ni katika kuweka sawa baina ya kumpata mshtakiwa aje Mahakamani na pia kumpa haki yake ya dhamana.

Mara nyingi tatizo linatokea kwamba wengi hawana mtu wa kumchukulia dhamana. Pia wengi utawakuta ni watu ambao ni wageni kwa hapa Zanzibar. Hili tatizo litaendelea kuwepo kwa sababu hiyo na halina jibu la rahisi. Juhudi zimechukuliwa mbali mbali za kisheria. Kwa mfano kuweka muda maalum wa upelelezi na kupunguza masharti ya dhamana. Linapotokea kwa mfano limetokea Pemba Mahakama wenyewe wamekaa wakaambizana na hili tatizo kweli wakalipunguza lakini tatizo bado kubwa lipo huko. Hili linahitaji msaada wa jamii yote kwa ujumla kwa sababu uhalifu unatokana humu tunamoishi.

Mhe. Spika, suala jengine ni malalamiko ya kuchelewa rufaa. Mhe. Spika, Idara ya Mahakama imejitahidi katika suala hili lakini bado wakati mwengine tunapochelewa ni kwa sababu ya ukosefu wa nyenzo katika kuchapisha zile *proceedings*. Lakini utakuta kwamba mahabusu wanalalamika wakisubiri rufaa wengi wao mara nyingi wanasubiri kesi ama kusikilizwa au hukumu. Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa Mahakama wamejitahidi katika kutatua tatizo hili na walioko ndani mara nyingi wanapewa kipaumbele hata kuliko wale walioko nje ya magereza.

Mhe. Spika, jengine ni suala la kuchelewa kwa miswada ambalo limezungumzwa na waheshimiwa wengi kuhusiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, tunaelewa kwamba hili ni tatizo, inapendeza sheria zetu zitakuwa nzuri katika zitapata kujadiliwa kwa uwazi na kwa muda ambao unafaa na kuwashirikisha watu wengi zaidi.

Lakini kwenye hili Mhe. Spika, tuna mipango ya muda mfupi nayo ni kuhimizana kuhakikisha kwamba miswada inayokuja inafika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa wakati. Lakini hili pia tumelizungumza serikali kwamba kuna haja ya kubadilisha utaratibu wa miswada kwa kusoma mara ya kwanza na mara zinazofuata katika vikao tofauti. Hili litahitaji marekebisho ya kanuni, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja atalieleza vizuri zaidi mipango ambayo inaandaliwa lakini tunakusudia kupendekeza kubadilisha utaratibu na kanuni zetu ili hili liwezekane. Kwa kweli litatusaidia sana hata sisi kutuondolea hii *pressure* ya kwamba hatulali ikifika wakati wa miswada usiku na mchana unahangaika. Kwa hivyo, tuna mipango ya muda mfupi lakini pia tuna mipango ya muda mrefu ya kuliondoa tatizo hili moja kwa moja.

Mhe. Spika, suala jengine ni lile alilozungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu mchango wa maendeleo kwa upande wa serikali katika bajeti ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, nadhani Mhe. Jussa akiangalia vizuri atakuta kwamba bajeti ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika *recurrent* imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Bajeti ya mwaka uliopita wa fedha ilikuwa shilingi milioni 472, bajeti inayokuja ya *recurrent* ni milioni 612. Wakati ule bajeti hiyo ilikuwa ni tuko pamoja na *Law Review Commission* kwa hivyo kuna ongezeko la karibu shilingi milioni 140 katika bajeti ya *recurrent* ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo, ule mchango wa serikali tuliomba uingizwe katika *recurrent* kwa sababu kuna mambo ya msingi ya kuweza kuifanyia *improvement* Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo inahitaji kuongeza bajeti ya *recurrent*. Tuna mambo mengi ya haraka ya kuweza kuyafanya na ingekuwa vizuri kwamba bajeti ile ya *recurrent* ikaongezeka. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie kwamba serikali imetupa mchango lakini mchango huu umeingizwa katika bajeti ya *recurrent* ili kuweza kuiimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Pengine mwakani anaweza akaona hiyo *capital budget* ikaingizwa katika *capital* ya kawaida baada ya kurekebisha yale mambo ya msingi, ili ikija hata hiyo bajeti ya maendeleo tuweze kuifanyia kazi kwa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, mipango hiyo ni kama tulivyosema katika hotuba ya bajeti lakini pia kuweza kuimarisha miundombinu ya mle ndani katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, suala jengine ni uchapishaji wa Katiba. Hili pia tuna mipango ya muda mfupi kwamba tunategemea tutapata fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kuchapisha nakala za ziada karibu 2,000 lakini tunategemea kufanya pia suluhisho la muda mrefu. Kwa sababu utaratibu huu wa kuchapisha machapisho ya kisheria, sheria, matangazo ya kisheria na kanuni. Hizo katiba na *document* nyengine muhimu hatuwezi kuendelea nayo hii kwa njia endelevu kama tunaomba pesa Hazina halafu tunazitumia tunagawa.

Lakini tumesema kwa kushauriana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo basi tuanzishe Mfuko Maalum *(Revolving Fund)* kwa ajili ya machapisho ya kisheria. Hii itatufanya tuwe na mpango endelevu wa kuweza kuchapisha na kuweza ku-*recover* zile gharama ili kuendelea kuchapisha haya machapisho. Kwa sababu ni vizuri yakawepo na naamini wananchi wapo tayari kuchangia kwa kiasi fulani ili ituwezeshe kuendelea kuchapisha.

Lakini jengine Mhe. Spika, nilizungumza kuhusiana na ada, nayo ni ile ada ya tirka kwamba labda ni kubwa sana ya asilimia 5 kwa sasa hivi. Mhe. Spika, naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwanza kodi au ada za mirathi nadhani kwa kiwango kilichopo Zanzibar basi ndio pahala pazuri kwa mtu kufa na kurithiwa kwa sababu ni cha chini kuliko katika nchi takriban zote duniani. Kwa sababu hata hapa Zanzibar ilikuwa ni asilimia 18 na ikashushwa mpaka ikafikia hii asilimia 5. Kusema kweli ni asilimia 3 kwa sababu asilimia 2 ni *administration fee.* Kwa hivyo, hii inasaidia katika usimamizi wa tirka zenyewe.

Mhe. Spika, pia naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba sio tu ile ada yenyewe lakini serikali pia imeondoa na gharama nyengine. Kabla ya Sheria hii ya Kamisheni ya Wakfu ya mwaka 2007 kulikuwa na ada za dalali ambazo zilikuwa ni kubwa kwa sababu ilikuwa lazima thamani ya mali itiwe na dalali ambapo nae alikuwa na mgao wake. Sheria hii imeiondoa hiyo mpaka labda wenyewe warithi walazimishe.

Lakini jengine ambalo limeondolewa ni ada ya kufungua kesi kwa ajili ya tirka *(administration of asset)* kupata ile *letter of administration* ambayo nayo pia ni gharama imeondolewa kwa utaratibu wa sasa. Kwa hivyo, mimi naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa kweli serikali katika eneo hili imejitahidi kuondoa gharama nyingi za usimamizi wa mali maiti.

Mhe. Spika, jengine kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambalo alizungumza Mhe. Abdulla Juma Abdulla kuhusiana ni suala la upelelezi. Mhe. Spika, hili suala linaendelezwa lakini bado kutakuwa na vikwazo katika baadhi kesi hasa kwa wale ambao ni wageni na makosa mengi makubwa makubwa. Uzoefu umeonesha kwamba ama ni wananchi wa Zanzibar kushirikiana na wageni au ni wageni. Kwa hivyo, hili bado linakwamisha lakini mpango huu ni endelevu na unaendelezwa katika kuusimamia.

Lakini naomba nimkumbushe Mhe. Abdulla Juma Abdulla kwamba hata sheria yenyewe katika hili imeweka vikomo. Upelelezi kwa makosa ambayo hayana dhamana mwisho ni miezi tisa na yenye dhamana mwisho ni miezi minne na yote hii ni kupunguza muda wa upelelezi wa kesi ili kuharakisha mwenendo wa kesi.

Mhe. Spika, ni lile ambalo amezungumza kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ijitahidi kuhakikisha kwamba inapeleka wanasheria kuweza kusimamia kesi katika Mahakama zote. Naomba nimhakikishie Mhe. Abdulla Juma Abdulla kwamba nia ni kupeleka katika Mahakama zote za Wilaya. Nadhani mwaka huu baada ya kukamilisha katika Mahakama ya Wilaya

Mfenesini na Mwera na Mahakama ya Wilaya ya Chake Chake na Wete kwa Pemba tutabakiwa na Mahakama ya Mkokotoni na Makunduchi kwa Unguja na Mahakama ya Konde na Mkoani kwa Pemba ambayo inatayarishiwa miundombinu.

Hili halikuweza kukamilishwa kwa sababu unahitaji kwa utaratibu wa sasa hivi kwa kila hakimu mmoja lazima uwe na mwanasheria au mwendesha mashtaka 1.6, yaani kwa kila mahakimu 10 uwe na wanasheria 16 ndio utaweza kuendesha bila ya matatizo. Kwa sababu hakimu anaweza akenda Mahakamani, anaweza asiende Mahakamani lakini mwanasheria au mwendesha mashtaka hata kama hakimu yupo Mahakamani au hayupo lazima aende. Kwa hivyo, hakuna dharura yupo likizo, kapata safari, yupo kwenye semina.

Mhe. Spika, sasa hivi ile ofisi ina wanasheria 32, ili kukamilisha hao mpaka Mahakama zote za Wilaya ni lazima iwe na wanasheria 39 kwa idadi ya sasa ya mahakimu. Sasa kuwaajiri hao wengine tulikuwa na tatizo la mshahara ambalo nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameliona vizuri na namshukuru kulieleza hilo. Mhe. Spika, tunategemea kwamba tatizo hili litaondoka katika mwaka huu wa fedha. Kwa sababu kama tungeajiri kwa upungufu wa sasa hivi ina maana tungekula bajeti ya *recurrent* na sisi kipindi chote tulikusudia ku-*maintain* ile *ratio* ya kwamba bajeti ya mishahara isizidi asilimia 45 na bajeti ya kufanya kazi iwe ni asilimia 55. Ukipungua hapo lazima utapata matatizo katika kuendesha afisi ambayo ina kazi za kila siku kama hii Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, suala la wanasheria maalum kwa kesi za watoto namshukuru Mhe. Mwakilishi aliyezungumza hili kwa sababu ni kweli kuna tatizo hilo. Lakini hili limeanza kwa kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kuanzisha kituo cha *One Stop Centre.* Kwa sasa hivi kituo kile kina wanasheria watatu ambao wamepangiwa mafunzo maalum na kwa hivyo kitatanua huduma zake kuhusisha kesi maalum za watoto.

Mhe. Spika, pia kwa upande wa Mahakama kama tunavyojua kwamba kuna Mahakama maalum ya watoto inapotokea mtoto ni mtuhumiwa. Kwa hivyo, kwa kupitia hiki kituo cha *One Stop Centre* huduma hizi zitaendelea na ninahakika kwamba tutafika huko ambako Mhe. Mwakilishi alikuzungumza.

Mhe. Spika, jengine ni lile alilozungumza Mhe. Abdulla Juma Abdulla vile vile kuhusu sheria ya vileo ya mwaka 1928. Labda niseme tu kwa ujumla kwamba suala la ulevi kwa Zanzibar lipo muda mrefu. Kwa kweli ukiangalia historia ya

sheria zetu Sheria ya Kupiga Marufuku Tembo Kali maana yake ndio lililoanza kupigwa marufuku kwanza mwaka 1907. Hii Sheria Nam. 7 ya mwaka 1928 ilikuja kuweka masharti kuwazuia zaidi raia wa Kiingereza kwamba wasilewe wanavyotaka wao. Iliweka masharti ambayo unaweza ukasema yalileta staha katika starehe hizi. Yalileta staha kwa sababu kwanza ni watu maalum ndio walioruhusiwa ilikuwa lazima uwe na kibali cha kulewa, kwanza ukate kibali cha wewe kulewa ndio unaweza ukalewa na kuna masharti yake ya kupewa kibali.

Mhe. Spika, pia sheria hii iliweka masharti magumu sana ya kuuza huo ulevi wenyewe. Lakini bahati mbaya kila mambo yalivyoendelea mwaka 1958 hii sheria ikafanyiwa marekebisho makubwa ambayo yaliingiza mambo haya yanayotupa shida hivi sasa.

Lakini katika sheria moja iliyorekebishwa mwaka 1964 ni hii ambayo iliondoa ile ya kwamba watu maalum ndio walewe ikawa ni sehemu ya uhuru. Kwa hivyo, hilo ni moja katika tatizo ambalo limekuwepo na sijui leo kama tunaweza tukarudi kule kule kwamba walewe watu maalum. Maana unajiuliza mwaka 1964 shughuli yote iliyokuwepo lakini moja katika sheria iliyoonekana ya kurekebisha ni hii.

Kwa hivyo, mimi nashukuru kwamba Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais imeliona hili tatizo na kuna kamati ambayo tutashirikiana nayo sisi kuifanyia mapitio. Lakini nadhani hii sheria ya mwaka 1928 basi ndio hiyo sheria ambayo ilikuwa na staha zaidi katika suala hili. Mhe. Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali hili inalishughulikia na nategemea kwamba litapata suluhisho katika muda mfupi ujao.

Lakini ndio nasema wale waje hawatoki nje, kwa hivyo nalo hilo tuliangalie kwa upande wetu wa kijamii vile vile. Mhe. Spika, ni jambo ambalo kwa upande wa serikali tutafanya yale yanayotuwajibikia kwa upande wa serikali ili sheria tuiweke katika mazingira ambayo hayatowapa shida wananchi. Kwa sababu hakuna sababu uweke baa mtaani hiyo zamani haikuruhusiwa, lazima uwe na hoteli ya daraja fulani ndio uweze kupewa kibali cha kuuza pombe. Waliokuwa wakiruhusiwa ni hao tu ama uwe na *police mass* na wanajeshi *(club licence).*

Kwa mfano, kule Tibirinzi wenyewe zamani wakiita *Tea Breeze* tukaibadilisha tukaiita Tibirinzi ilikuwa ni moja katika iliyokuwa na leseni kwa Pemba nzima kwa sababu walikuwa wakitumia wenyewe tu. Lakini sasa ziko mitaani naelewa hilo tatizo na serikali inalielewa na tunalifanyia kazi.

Mhe. Spika, labda nimalizie kwa suala alilozungumzia Mhe. Hija Hassan Hija kwamba kuna utafiti uliofanywa wa kuwa Zanzibar kuna tatizo la kakapoa na dadapoa. Mhe. Spika, nadhani Waheshimiwa Wawakilishi watakumbuka kwamba mwaka 2004 tulifanya marekebisho makubwa ya Sheria ya Jinai na hili likarekebishwa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria yetu sasa kwa upande wa kina dada wao wenyewe kwa wenyewe kifungu cha 153 hilo ni kosa la jinai, kwa upande wa kinakaka wenyewe kwa wenyewe kifungu cha 157 hilo ni kosa la jinai.

Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan Hija akiwapata awapeleke tu sheria ipo tena madhubuti kweli kweli lakini mambo haya kwa usiri wake tunajua sote kwamba ni shida kupata huo ushahidi. Utamuona mtu mtaani kwamba alivyokukalia sio sawa lakini hatumhukumu mtu kwa anavyotembea, anavyocheka wala anavyoongea ushahidi ndio unaotakiwa.

Sasa kama Mhe. Hija atakuwa nao huo basi naomba nimhakikishie kwamba sheria ipo. Mhe. Spika, naomba nimhakikishie pia kwamba sheria yetu ni *advance* zaidi maana yake ukiangalia ni kwamba hata hii teknolojia ya siku hizi ya hawa kinadadapoa wenyewe kwa wenyewe wanatumia mpaka mashine za kisasa inavyosemekana.

Sasa sheria yetu pia hilo ililiona mwaka 2004 ikasema hata kutumia hizo mashine pia kama ni wenyewe kwa wenyewe ni kosa, haijazungumzia kama ni mwanamke na mwanamme. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie tu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba sheria yetu tuliirekebisha.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo naamini Mhe. Waziri atakuja kulizungumza kwa uzuri maana huo ndio uwanja wake ni hili suala la Katiba. Naomba nisiyatoe ladha yale ambayo najua yeye atayaeleza vizuri. Lakini mimi labda niseme mambo mawili tu kwenye hili.

La kwanza ni vizuri tukafahamu kinachoendelea kwamba sasa hivi Waheshimiwa Wajumbe hatujafika katika marekebisho ya Katiba. Mchakato wa sasa hivi na ambacho mmetuamini tukifanye ni kuandaa kanuni, ni kuandaa uwanja, mechi yenyewe bado. Tulichokabidhiwa ni kuandaa uwanja wa hiyo mechi yenyewe na kanuni zenyewe za mchezo, lakini itakapofika wakati wachezaji ndio nyinyi Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote kwa kila mtu na uwezo wake.

Mhe. Spika, tunajua kwenye hili haiwezekani kwamba sisi wawili au hata tuliomo humu ndani tutaweza kulisimamia jambo hili kwa sababu si letu ni la wananchi wote kwa jumla. Mhe. Spika, kinachofanyika sasa ingekuwa ni

uganga tungesema ni kuandaa chano, lakini itakapofika wakati mimi nakubaliana na yote aliyosema Mhe. Hija Hassan Hija na wengine kama mengine tuliyokuwa hatuwezi kuyasema basi wapo wasemaji.

Mhe. Spika, mimi naamini hilo watalifanya na huu ni ukweli kwamba wakati mwengine hata unapotaka kupandisha shetani wanasema kule kwetu shetani haimbiwi kimji. Maneno inawezekana ndio yale yale lakini mpaka umpate Mhe. Hija Hassan Hija au Mhe. Subeit Khamis Faki aimbe vile anavyotaka kwa maneno yale yale basi ndio atapanda. Lakini pengine ukimpa sahibu yangu hapa Mhe. Omar Yussuf Mzee akaimba kimji hapandi shetani. Kwa hivyo, kwa kuelewa hilo tunajua kwamba utakapofika wakati kama ni la kupandisha basi wapo waimbaji watakaoweza kuimba na akapanda na akatoa jina na akachukuliwa. Kwa hivyo, tunachofanya sasa naomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu astahamili.

Mhe. Spika, naomba ninukuu maneno yako uliwahi kusema hapa kwamba hamu ina matatizo yake, lakini mmoja katika ku-*comment* haya maneno yako akasema hamu ndio inayoleta uhai. Kwa hivyo, ni suala la ku-*balance* naomba hizi hamu zetu tuzisubiri itakapofika siku yake *inshaallah* tutapata uwanja mzuri wa kuweza kuzitumia na zikazaa matunda. Mimi labda ilikuwa niseme hilo kwenye uwanja wa suala hili la Katiba. Ungeniruhusu Mhe. Spika, kama neno zuri ningewaambia tu kwamba labda Waheshimiwa Wajumbe taireni kwanza tusubiri yatakapokamilika basi haya mtapata fursa. Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha hotuba yake ambayo kwa kweli ni nzuri na imejaa kila kitu. Vile vile nataka niwapongeze sana watendaji wake waliomsaidia Mhe. Waziri kwa kufanikisha majukumu haya. Halikadhalika nataka nimpongeze sana Mhe. Jaji Mkuu kwa kuteuliwa na Mhe. Rais. Pia nataka nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu kwa kuteuliwa na Mhe. Rais na hasa kwa mchango wake ambao amemalizia.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu amenukuu maneno yako ya hamu akayaoanisha na Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Sasa na mimi Mhe. Spika, nitakuwa nina maelezo machache tu ambayo hamu hiyo hiyo alikuwa nayo Mhe. Jussa akanigusa katika michango yake. Kwa hivyo, naomba kidogo kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nitoe ufafanuzi katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, moja ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa na wasi wasi na pengine Waheshimiwa Wawakilishi wengi walikuwa na wasi wasi na

inawezekana wafanyakazi vile vile wa Wizara hii ya Katiba na Sheria wana wasi wasi upungufu wa kasma ya mishahara. Mhe. Spika, Mhe. Jussa alikuwa na wasi wasi kwamba huenda katika kipindi fulani katika mwaka huu wafanyakazi pengine wasipate mishahara kwa sababu mishahara iliyoainishwa pale ni kidogo.

Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hakuna mfanyakazi wa Utumishi wa Umma atakayekosa mshahara katika kipindi cha mwaka 2011/20112. Kwa sababu katika utaratibu wetu wa kutumia *first charge* ni mshahara, kwa hivyo kwanza tunatoa mishahara na baadae ndio tunatoa mambo mengine.

Lakini pia nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hata katika bajeti hii iliyomalizika mwaka jana tulitenga fedha bilioni 2.6 tukaziweka katika mfuko mkuu wa serikali kwa ajili ya mishahara, yaani *shock absorber* pale ambapo patahitajika nyongeza za mishahara. Huwezi ukaliepuka hili Mhe. Spika, kwa sababu kati kati unaweza ukasikia JKU imepandisha vyeo, KMKM wamepandisha vyeo, unapompandishia mtu cheo maana yake kiendane na mshahara wake. Watazitoa wapi kwenye bajeti ile uliyofanyia *allocation* katika bajeti ambayo mliyoitangaza, lazima tutoe fedha katika mfuko mkuu wa serikali ili tuweze kuwapatia wenzetu.

Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba zoezi la kurekebisha mishahara tumelimaliza hivi karibuni hakuna mfanyakazi wa serikali atakayekosa mshahara wake.

Lakini la pili Mhe. Spika, liliulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk suala zima la fedha za Mambo Msiige kutokuwekwa katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa madhumuni ya ujenzi wa jengo la wizara.

Mhe. Spika, nataka nimwambie tu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Waheshimiwa Wawakilishi wengine wote kwamba lengo la serikali ni zuri sana. Katika kikao cha Baraza la Mapinduzi tumekubaliana kwamba majengo tunayotumia wizara mengi sasa hivi ni mabovu, hata lile la kwangu mimi ninalotumia Wizara ya Fedha ni bovu. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora hana jengo nimemuazima jengo la *ZRB*, Waziri wa Katiba na Sheria jengo lake bovu na mawaziri wengine wote humu ndani. Labda Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ana jengo zuri, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ameanza kujenga jengo lake zuri, lakini wengi majengo yao ni mabovu.

Tukakubaliana Mhe. Spika, kila mmoja atatazama peke yake na katika bajeti hii kila wizara itakuja na kifungu cha ujenzi lakini kweli hawataweza kujenga kwa kutumia fedha hizi watakazoziweka, kila mmoja ataweka milioni 200 ambazo huwezi ukajenga jengo. Tunaweza tukachukua miaka na miaka hatujamaliza jengo hata moja, sasa tukafanya uamuzi wa makusudi kwamba hebu tuanzeni kujenga kwa pamoja majengo mawili mawili lakini kila jengo wakae wizara mbili mbili, twende ghorofa sita au saba itategemea na pahala penyewe palivyo. Tukasema tuwe na vote ya pamoja ya ujenzi wa majengo ya serikali na hii isimamiwe na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Uzuri wake ni nini Mhe. Spika. Uzuri wake ni kwamba huyu akichelewa basi huyu aliyekuwa yuko tayari unampa huyu, anaanza kujenga na yule akiwa tayari na yeye unampa kujenga mna *rollover* mnakwenda mwaka wa pili mnamaliza kwa kipindi kifupi sana kuliko hata mlivyotarajia.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Makame Mshimba kwamba lengo ni kuwapatia Wizara ya Katiba na Sheria jengo jipya ndio lengo. Nathubutu kusema tayari tumeshatoa kazi ya michoro kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, tumewaomba watafute mtaalamu, mshauri mwelekezi ili waanze kazi hiyo na tunatarajia katika kipindi kifupi kazi hiyo wataanza. Analolitaka Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Makame Mshimba kusikia ni kwamba hii ni wizara ya kwanza ndio itakayoanza kujenga na hilo nataka nikuhakikishie, hii ndio itakayokuwa wizara ya kwanza. Tumetenga 5.3 bilioni.

Wizara ya pili tutakayoanza kujenga, watu wanasema kwamba aah! Hata sijui niseme vipi.

Mhe. Haroun Ali Suleiman: *Charity begins at home.*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Haroun Ali anasema *charity begins at home.* Lakini mimi sitoanza kwangu nitahakikisha kwamba kuna wanzangu kwa kweli hali zao ziko mbaya. Kama wewe mgonjwa wako yuko wodini mwengine wake yuko *ICU*. Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hali zao kimajengo ni mbaya. Mimi nitahakikisha kwamba hawa wenzangu waanziwe mwanzo mimi nitasubiri.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Ismail Jussa kwamba nia ya serikali ni nzuri, tumeziweka pamoja hizi fedha ili tukianza tuanze kwa *speed* tumalize, kuliko kuanza kuzigawa kidogo kidogo, tutatumia miaka mingine kumi au kumi na tano hatujamaliza jengo hata moja. Tutaanza na jengo hili na

nataka nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa na Waheshimiwa Wawakilishi wengine kwamba fedha za Mambo Msiige ambazo tulizonazo kiasi cha 2.2 bilioni hazitoweza kumaliza jengo la Mambo Msiige au jengo la Katiba wanalotaka. Tunataka jengo, tutatumia zaidi ya 2.2 bilioni ndio lengo letu la kuweka hapa. *out of* 5.3 tunatarajia wao watatumia zaidi ya nusu. Tutawapa pesa hizo tutajenga hilo jengo na tayari kiwanja chao wanacho na tayari kazi ya kuanza michoro tumeshawaagiza nadhani Mhe. Waziri atakaa na Katibu Mkuu wake kuona kwamba wamefikia wapi ile kazi, lakini sisi tumeshazungumza nao asubuhi hii ya leo kwa kwali wanakwenda vizuri sana na watakapomaliza tu ujenzi utaanza mara moja.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hotuba hii, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kujumuisha maelezo yote na michango yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyatoa katika kuchangia hotuba ya wizara yangu.

Mhe. Spika, katika uchangiaji huu nathubutu kusema kwamba nimefarijika sana na Waheshimiwa Wajumbe ambao walitoa michango yao. Kwa ujumla ni wajumbe 32 ambao wamechangia. Kati ya hao 32 wajumbe 21 wamezungumza na wajumbe 11 walichangia kwa maandishi.

Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba kuwataja wajumbe wote waliochangia na walioleta kwa maandishi. Wajumbe waliochangia wa kwanza ni:

Mhe. Ali Abdalla Ali Mwenyekiti,
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Abdalla Juma Abdalla
Mhe. Omar Ali Shehe
Mhe. Asha Bakar Makame
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Mohammed Haji Khalid
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Ussi Jecha Simai
Mhe. Rashid Seif Suleiman
Mhe. Ali Salum Haji
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Mussa Ali Hassan
Mhe. Abdalla Mohammed Ali

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Othman Masoud Othman
Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

Waheshimiwa Wajumbe walioleta kwa maandishi ni 11 kama ifuatavyo:

Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Kazija Khamis Kona
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Rafai Said Rufai
Mhe. Amina Iddi Mabrouk
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Ashura Sharif Ali

Mhe. Spika, wajumbe hawa wote napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa, kwa sababu michango yao yote waliyoitoa imesaidia na itasaidia wizara yetu katika kuimarisha zaidi shughuli za utendaji katika wizara hii.

Mhe. Spika, wajumbe wote hawa michango yao ilikuwa katika maeneo muhimu ambayo ni kama hivi ifuatavyo. Kwanza kulikuwa na mchango mkubwa sana katika Idara ya Mahakama.

Pili kulikuwa na mchango mkubwa sana katika Idara ya Mrajis Mkuu wa Serikali, vile vile michango kwa Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakfu na Mali ya Amana pamoja na Mufti na Haki Miliki.

Mhe. Spika, kwa sababu wajumbe wengi walichangia katika maeneo haya na kwa sababu michango yao ilikuwa takriban inafanana. Kwa hivyo, mimi kwa ruhusa yako naomba nizungumzie idara moja moja pamoja na wale Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia.

Kwa upande wa mahakama Mhe. Spika, michango ilikuwa kwa waheshimiwa wengi kama vile Mhe. Mohammed Ali, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Hija Hassan, Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Rifai Said Rifai, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Abdalla Juma

Abdalla, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Asha Bakar Makame, Mhe. Suleiman Hemed, Mhe. Mohamme Haji Khalid, Ismail Jussa, Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Mahammed Mbwana Hamad, Mhe. Salma Mohammed Ali na wengi wengineo.

Mhe. Spika, katika eneo la mahakama mambo kadhaa yalizungumzwa. Kwanza kulikuwa na suala la uhaba wa mahakimu. Mhe. Spika, ni kweli hapo mwanzo tulikuwa na uhaba wa mahakimu, lakini nashukuru serikali na namshukuru Mhe. Rais kwamba kilio chetu hiki cha matatizo ya mahakama, tumepata nafasi ya kuajiri mahakimu pamoja na majaji. Hivi sasa nathubutu kusema kwamba uhaba huo wa mahakimu katika mahakama zetu umepungua sana tena sana.

Hivi sasa Mhe. Spika, kwa mfano katika Mahakama za Wilaya Unguja Mjini Magharibi tuna mahakamu 5, Mfenesini 2, Mwera 2 na Mkokotoni 1 na Pemba kila Wilaya kuna hakimu wake. Kwa hivyo, utaona tumejaza maeneo yote. Lakini katika Mahakimu wa Mkoa Pemba wako 2, kusini 1, kaskazini 1 na Mjini Magharibi 5. Kwa hivyo, pia nalo hili pengo limezibika kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, swali lilikuja hivi, kwa nini mahakimu. Kwa mfano anatoka Chwaka anakwenda Mwera. Hii ni katika utaratibu wa kawaida wa kazi zetu, kwa sababu ukitizama Chwaka hakuna kesi nyingi za kumuweka hakimu pale wakati wote, kwa hivyo badala ya kuipoteza *main power* hii ni vyema tukampangia nafasi pahala pengine kwenda kusaidiana na wenzake.

Mhe. Spika, ni hivyo hivyo kwa Makunduchi kwa mfano, kesi za Makunduchi sio nyingi sana, kwa hivyo hatuwezi kumuweka pale hakimu kwa wiki nzima pale, itakuwa tunapoteza *main power* na hilo sio lengo. Lengo ni kuwasaidia wananchi, sasa katika kuwasaidia wananchi hawa tunajua angalau.

Kwa mfano kesi za Makunduchi kwa siku mbili au tatu zinaweza zikakamilika. Kwa maana hiyo ndio tunaweza tukampeleka Makunduchi, lakini pia hakimu yule yule anaondoka Makunduchi anakwenda katika eneo jengine. Kwa hivyo hayo ndio madhumuni makubwa ya kwa nini hakimu hakai pale moja kwa moja, kwa sababu maeneo mengine huwa hayana kesi nyingi za kushughulikia. Katika maeneo ambayo kesi zipo hatuwezi kufanya hivyo na hatujafanya hivyo. Tunamuweka pale na kuna wengine tunawaongezea ili kusaidiana na kesi hizo. Kwa hivyo, wakauliza kwa nini basi tukawa tuna *delays* nyingi. Mimi nashukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumza na akasema kwamba suala la hizi *delays* za kesi haitokani na kitu kimoja tu, sio hakimu tu, lakini ni mtiririko wa mambo mengi ambayo yote kwa pamoja yanaweza yakachelewesha kesi.

Kwa mfano kesi ili iende ni lazima uwe na hakimu, lazima uwe na wanasheria, uwe na mashahidi na uwe na polisi waliochunguza ile kesi. Sasa mmoja wao akikosekana basi kesi ile ni lazima iahirishwe. Kwa hivyo utaratibu huu ndio unaofanya kuwe na *delays*. Lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe tutajitahidi kukaa nao pamoja hawa wadau wote wa kesi ili tuhakikishe kwamba ucheleweshaji huo unapungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni suala la Makadhi pamoja na Mufti. Kwanza napenda niseme kuwa kweli tuna upungufu wa Makadhi na kweli kwamba tokea pale alipohitajika Mufti wetu bado hajateuliwa mwengine. Utaratibu wa Makadhi pamoja na Kadhi Mkuu ni lazima tufuate sheria zilivyo na sheria ya kuteuwa Makadhi, kwa sababu wao ni mahakimu ni kwamba lazima *judiciary service commission* ikae na iwa *vote*.

Tulikuwa na tatizo la kukaa kwa *judiciary service commission.* Kama mnavyojua kuwa kulikuwa kuna tatizo la kumpata Jaji Mkuu kwa sababu yeye ndiye mwenyekiti wa *judiciary service commission.* Kwa hivyo, tulichelewa kidogo, lakini mara tu baada ya kuteuliwa Jaji Mkuu mpya kazi hiyo tumeshaifanya, tumeshawaita wale watu ambao tunahisi wangefaa kuwa Makadhi, tumeshatoa maoni.

Mhe. Spika, napenda niseme kuwa katika kuwazingatia, tumezingatia mambo mengi. Tumezingatia elimu yao ya kidini, tumezingatia elimu yao ya duniani na tumezingatia umri wao. Kwa sababu wakati mwengine umri nao ni matatizo. Anakuja mzee ni mzuri katika dini, anaelewa kila kitu na anafahamu mambo ya dunia lakini umri wake ni miaka 75 wako ambao wameomba, lakini sasa unamuajiri mtu wa miaka 75, kwa kweli itakuwa sivyo. Kwa hivyo, tulichelewa kidogo kwa sababu tulikuwa tunajaribu kupata angalau watu wenye umri mdogo na ambao wana elimu zote ya dunia na ya akhera.

Hiyo tumeshafanya na ushauri tumeshaupata na Mhe. Rais tumeshamuarifu na hili suala analijua na naamini kwamba kwa busara zake hatua anazichukua na ni karibuni tu kwa imani yangu kwamba tutapata uteuzi wa Makadhi, Kadhi Mkuu pamoja na Mufti. Maoni hayo tumeshayawasilisha na sasa tumpe nafasi yeye, kwa sababu hata sisi tukishamaliza ni lazima na yeye kwa kutumia vyombo vyake aweze angalau kutafuta *vote* ya utaratibu wake ambao anaupata. Naamini suala hili halitochukua muda mkubwa sana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lilizungumzwa katika michango ya wajumbe ni suala la utaratibu wa Mahakama za Kadhi. Sisi tulisema hapa katika hotuba yetu, tulisema kwamba tuna azma ya kurekebisha sheria ya Makadhi. Hii ni kwa lengo moja kubwa, kwa sababu sheria ya Makadhi ya

wakati ule au hii ya sasa iliopo, kwa kweli yote inazungumzia suala la sheria ile kama kwamba ni kesi ambazo zinatokana na kesi za kawaida za mahakama za kawaida. Lakini tukaona kwamba haiwezekani kwa sababu kuna *technicalities* nyingi katika kesi za aina zile.

Kwa hivyo, lengo la kurekebisha sheria hii ni kupunguza zile *technicalities* za mahakama za kawaida ili hawa mahakimu wetu au Makadhi waweze kuwa na utaratibu wao na waweze kuwa na mwenendo wao ambao utawapunguzia zile *technicalities* ambazo zipo hivi sasa. Kwa hivyo, suala hili Mhe. Spika, tunalifanya na naamini kwamba tutalifanya haraka haraka ili wenzetu hawa waweze kufanya kazi zao vilivyo.

Mhe. Spika, jengine kuhusu mahakama ni suala la majengo ya mahakama. Mimi napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe hapa kwamba mimi binafsi baada ya kuteuliwa katika nafasi hii, nimetembelea mahakama zote za Unguja na Pemba. Mhe. Jaji Mkuu na yeye ameshatembelea mahakama zote za Unguja na Pemba. Tumeshakaa pamoja mimi na Mhe. Jaji Mkuu ili kutafuta njia gani mahakama zetu tunaweza kuzisaidia. Hapa napenda nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa kwamba haitofika hata miaka 2, seuze miaka 22 ya kwenda kutembelea vyombo vyetu hivi.

Sasa tumeshakaa, lakini tujuwe. Hivi karibuni mimi nilikuwa na wageni ofisini kwangu. Katika jambo moja ambalo tulizungumza nao ni suala la kutusaidia majengo ya mahakama. Lakini wenzetu wafadhili siku hizi, misaada kama hii hawatoi, suala la majengo hawatoi. Kwa hivyo, ni vigumu kwa kweli kusema kwamba tunaweza tukajenga mahakama zote kwa mara moja.

Fedha ambazo tunazipata kwa kupitia serikali hizo ndio zitasaidia kujenga mahakama zetu. Kwa maana hiyo mahakama zetu tutazishughulikia na tutazijenga lakini hatua kwa hatua, kwa sababu hatuna uwezo wa kuzijenga mahakama zote kwa mara moja. Hivi sasa ndio maana ukaona kuwa mahakama ya Konde tumeshaitengeneza, Mahakama ya Chwaka tayari na tunaendelea na mahakama ya Vuga. Mahakama ya Mwera tumeshajenga na mahakama ya Mkoani na kila tutakapopata fedha *Inshaallah* tutaendelea kuzikarabati ili angalau ziwe na sura mpya ya mahakama.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mahakama ya Mkokotoni. Kweli Mahakama ya Mkokotoni ni mbaya sana, lakini jengo lile la Mkokotoni mwanzo lilikuwa ni jengo la mudir hapo zamani na jengo lile mudir walikuwa ni mahakimu na wao. Kwa hivyo, lile ni jengo letu, lakini tena baadae tukaruhusu Mkuu wa Mkoa kuingia mule, sasa akageuka ngamia, maana sote mahakama tukatolewa, tukapewa vyumba viwili vidogo na vyumba vile ndivyo tulivyokuwa

tukiendelea navyo. Sasa kule juu ambako Mkuu wa Mkoa yuko vyoo viko na utaratibu uko, lakini vile vya chini tulivyopata sisi hakuna vyoo. Tumelazimika sisi angalau kutafuta pahala kuwasitiri wale wenzetu, tunajua kwamba ni mbali kidogo, lakini hiyo ndio hadithi ilivyokuwa.

Hivi sasa kwa sababu tunaamini kwamba Mkuu wa Mkoa ataondoka katika jengo lile hivi karibuni, basi hivi sasa tuko katika kuzungumza na serikali ili jengo lote lile lirejee tena kuwa ni jengo la mahakama. Sasa tukifanya hivyo tunaweza kulitengeneza kwa sababu ni letu na pia ile hali ya matatizo ya vyoo tunaweza tukairejesha.

Mhe. Spika, suala la mishahara, napenda nizungumze kwamba mishahara kama ilivyozungumzwa kweli ni midogo, lakini naamini serikali yetu kwa kuona umuhimu wa watu kama hao pamoja na madaktari wamepewa kipaumbele maalum, ili kuweza kuwasaidia. Kwa hivyo, naamini kwamba mishahara kwa kadi kama hizi yamezingatiwa na mambo kidogo yatakuwa ni mazuri kulinganisha na nyuma.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la *CAG* kwamba Mrajis wa Mahakama alitumia pesa vibaya. Kwa hapa napenda niseme tu kwamba kwa mujibu wa ripoti ile ya *CAG*, ni kweli kwamba kuna fedha kiasi ya Shs.640,000/= ambazo hazikuambatanishwa na viambatisho vyake vya matumizi. Lakini baada ya kupata hivyo tukafuatilia na tumeshapeleka viambatisho vile na suala hili limeshamalizika. Ninechopenda niseme tu kwamba hata kama kulikuwa na tatizo hili lakini haina maana kwamba mahakimu wetu au majaji wetu ni wabadhirifu, kwa sababu suala hili la *Administration* ni tofauti na suala la uendeshaji wa kesi.

Administration iko upande mwengine na suala la la kesi liko upande mwengine. Ndio maana hivi sasa tuko katika harakati za kuweka angalau Afisi ambaye anashughulika moja kwa moja na mambo ya *Administration* katika mahakama ili kuondoa dhana kama hizi ambazo hazitokuwana msingi wowote.

Mhe. Spika, nakubaliana na wajumbe wengi ambao walizungumzia kwamba mahakama nayo iwe na fungu lake kama Baraza la Wawakilishi. ni kweli kwa sababu mahakama ni nguzo moja katika nguzo za serikali, ukiacha Baraza la Wawakilishi ni mahakama na *executive*. Hizi zote katika ile *principle* ya *separations of powers* basi ni vyema kuwa na fungu lake.

Naishukuru serikali kwamba baada ya kuwapelekea kilio hicho kwamba mahakama nayo ni lazima iwe na fungu lake, wamesaidia kidogo na ndio maana katika bajeti yetu safari hii mishahara yote ya majaji itatokana na

consolidated fund kitu ambacho zamani kilikuwa hakipo. Sasa hii ni hatua moja, lakini tunawahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba hili tutaliendeleza ili hatimaye na mahakama iwe na fungu lake kama lilivyo Baraza la Wawakilishi.

Kuna suala la sheria hizi ndogo ndogo ambazo walilaumiwa pengine mahakimu. Mimi naamini kwamba mahakimu kwa utaratibu huu hawawezi kulaumika. Kwa sababu kwa mfano ulitolewa mfano, kuna kesi za *traffic* kwa mfano au kesi ya ulevi.

Nashukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumza vizuri. Kesi za *traffic* kwamba mtu akiendesha baskeli hana kengele au hana *break*. Ni kweli hapo zamani sheria nafikiria sura ya 135 adhabu zake zilikuwa ni ndogo, lakini sheria hii naamini imefanyiwa marekebisho au ilikuwa *amended*, kwa sheria ya mwaka 2003 ni *road traffic art*. Sasa hiyo *traffic art* imezidisha adhabu hizi. Kuna matatizo madogo ambayo baada ya kufuatilia ni kwamba yapo na hayo tutayafuatilia. Kuna baadhi ya kanuni katika hii *road traffic art* hazijatungwa. Kwa hivyo, mimi ninawahakikishieni Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutashirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tuwakumbushe jukumu hili, ili kanuni hizi tuzirekebishe na adhabu ziweze kutumika ipasavyo.

Mhe. Spika, haya ni baadhi ya mambo ambayo yalizungumzwa katika suala la mahakama. Suala la mwisho lilizozungumzwa ni kwamba Mhe. Salma aliuliza kuhusu Jaji Mkaazi Pemba. Mhe. Spika, wewe ni shahidi na baadhi ya wawakilishi waliomo katika Baraza hili wa zamani ni mashahidi, kwamba mimi ndio kilichokuwa kilio changu kikubwa sana katika suala hili. Nakumbuka hata alipokuwepo Mhe. Ali Juma Shamuhuna alipokuwa Waziri wa Katiba kwa muda ule aliokabidhiwa, mimi nili-*offer* nyumba yangu ili akae Jaji Mkaazi Pemba. Kwa bahati mbaya na waswahili wanasema, ukiamba vyako na Mwenyezi Mungu huamba vyake.

Mhe. Spika, tulikuwa tumeshafanya matayarisho nyumba ya Jaji tayari na ipo Tibirinzi, zamani alikuwa anafikia Waziri Kiongozi nyumba nyengine ya mkono wa kulia. Tumeshaitengeneza hata kwenye bajeti hii ilikuwa haimo, bahati mbaya sana na ni kwa masikitiko. Katika mvua hizi kubwa na upepo nyumba ile iliangukiwa na mwembe, ikawa kwa lugha ya siku hizi, ikawa ni nyang'anyang'a. Kwa hivyo, tumerudia mwanzo kabisa.

Katika kutia tathmini ya maharibiko itagharimu kiasi cha shilingi milioni 50. Ni pigo kubwa kwa wizara yetu, lakini tunawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa kipindi hiki wakati tunatafuta pesa, kwa sababu hata fedha hizi katika bajeti hazipo kwa sababu ilipopigwa na muembe ilikuwa mambo ya

bajeti tayari yameshakamilika. Kwa hivyo, tutajitahidi kutafuta fedha pahala pengine tuitengeneze ili Jaji Mkaazi Pemba tumpeleke

Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Rashid Seif Suleiman na wengineo.

Mhe. Spika, najua katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali tunayo matatizo mengine na hasa yako katika *registration* ya vizazi. Kwa kweli hili ni tatizo na tumeliona tayari tumeshaanza kuchukua hatua, tumewaita Wakuu wa Mikoa, Wilaya pamoja na watendaji, ili kuhakikisha kwamba matatizo haya yanaondoka. Habari nilizonazo ni kuwa kidogo kuna afuweni lakini bado, kwa sababu bado basi Mhe. Spika, nalihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tutaendelea kulichukulia hatua.

Kwa hivyo, hatua ambazo tayari tumeshaanza kuzichukua ni kuwa ofisi yetu bajeti hii ikipita tukijaaliwa, basi tumetenga wafanyakazi 10 na kila mfanyakazi mmoja atakwenda katika wilaya moja, ili kuhakikisha kwamba yale matatizo ya wananchi katika wilaya ile yanaondoka.

Hali hii kwa sababu wafanyakazi wa wilayani walikuwa na matatizo kidogo, kwa sababu mfanyakazi, yaani *typist* wa vyeti anaweza kupewa vyeti, lakini akapewa kazi nyeingine na Mkuu wa Wilaya au akachukua likizo na sisi hatujui. Kutokana na hali hiyo, vile vyeti vinarundikana tu na wakati anaporudi si kama anafanya shughuli ile isipokuwa anafanyakazi nyengine za Ofisi ya Wilaya.

Kwa hivyo, hili ni tatizo ambalo tumeliona na tunahakikisha kwamba katika utaratibu huu mpya, kwa sababu mfanyakazi wetu mmoja ambaye atakuwa anawajibika moja kwa moja na ofisi yetu, basi litapungua kwa kiwango kikubwa sana. Hilo ni moja ambalo tumelifanya.

Jambo jengine ambalo tumelifanya tumesema kwamba ili wananchi wasipate matatizo haya, yule *middle man*, yaani mtu wa katikati naomba asana tumuondoe, yaani Sheha kwa utaratibu huo na tokea hapo nyuma hahusiki, lakini tulikuwa tunamhusisha kikamilifu. Kwa kweli, Sheha jukumu lake yeye ni pale unapopata mtoto kumwambia kwamba umepata mtoto katika eneo lako na yeye anakupa kile cheti cha utambulisho kuwa umeshapata mtoto, ili uende wilayani.

Sasa lililokuwa likifanyika kwa baadhi ya wananchi wetu ni kwamba yeye anaona uvivu kwenda wilayani, kwa hivyo anamuachia Sheha na kumwambia basi niletee na Sheha anachukua zile fedha na kukaa muda na mwengine anampa pia fedha na baadaye zinakusanyika bila ya yeye kwenda na akitizama

Sheha kwenye mfuko anazo fedha nyingi. Kwa hivyo, kibinadamu na yeyote kati yetu sisi ikiwa umepewa fedha basi unaweza kusema unaziamiza kidogo na kuzirejesha ndio matatizo na inachukua muda na wala hawezi kwenda wilayani kama zile fedha za kulipa hana. Kwa hivyo, hilo ndilo lililokuwa tatizo jengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ombi langu kwa Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa ujumla, wakati unapopata kile cheti cha utambulisho kutoka kwa Sheha basi tafadhalini nendeni wilayani na wilayani mkifika mtapewa tarehe ya lini kwenda kuchukua cheti chako. Kwa kuwa sasa tutakuwa na mtu wetu kule, basi atahakikisha kwamba tarehe ile cheti hicho unakipata. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hivi sasa tayari tumeshaanza *process* na tumeshapeleka baadhi ya wafanyakazi wetu katika wilaya, kwa ajili ya kuhakikisha ile *backlog* ya vyeti ambavyo vimo vyote tunavitoa na wala hatuna matatizo ya cheti au vyeti, kwa sababu vyeti kila wilaya vipo na matatizo tuliyonayo ni kwamba bado havijaandikwa. Sasa hilo tutahakikisha katika kipindi hiki kifupi tukijaaliwa vyeti vyote vioko wilayani tutavitoa na mtu wetu atakuwepo, ili kuhakikisha kwamba suala hili linarekebishika. Vile vile kulikuwa na suala jengine kwa nini hivi vyeti, kwa sababu *typewriters* zilizopo ni mbovu tena za zamani na uandikaji wenyewe ni mbovu kwa nini hatutumii *computer*.

Kwa kweli suala hilo tunalo na tayari tumeshaanza kufanya mazoezi, lakini *computer* tunavyojua ina matatizo, kwa sababu tunaweza kutoa vyeti vyetu kwenye *computer*. Lakini kuna huu utundu wa *IT* na mtu akabuni kwenye *computer* yake na kutoa vyeti vingi sana na baadaye ikawa sisi tunapata hasara, kwa sababu vyeti ni thamani, sasa yeye anatoa na pengine anauza na halafu anawapa watu ambao hawahusiki na tatizo litakuwa kubwa.

Kwa hivyo, hivi sasa tunajaribu na tayari tumeshaanza kufanya utafiti namna gani kama tutatumia computer basi tuweze kutumia *computer* na kuwe kuna alama ambazo *computer* ile hawezi mtu mwengine kuzitumia, ili kunusuru kutoa vyeti hivyo kwa watu ambao hawafai. Nadhani suala hili litachukua muda kidogo. Lakini nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kweli kutumia *typewriter* za zamani ni matatizo, basi tutajaribu kuzirekebisha kwa kadri inavyowezekana. Kwa maana hiyo, *computer* matatizo yake ni hayo na kwanza tunatizama namna gani tunaweza kufanya.

Mhe. Spika, kuna suala kuhusu malipo haya ya vyeti. Kwanza kuna suala la *notification*, yaani ile kutoa taarifa kwamba umepata mtoto, *notification* ile unatakiwa uanze tokea siku ile mtoto amezaliwa kwa kipindi cha siku 40 na hicho ndicho kipindi kinachotakiwa.

Registration ni kuanzia siku aliyozaliwa mtoto kwa kipindi cha miezi miwili, sasa ikimaliza hapa kuanzia mwezi wa tatu mpaka miaka miwili, katika kipindi cha ndani ikiwa hujenda kuandikisha na ukenda kuandikisha kwenye kipindi hicho, basi utaangukia kwenye *late registration* katika kipindi hicho na cheti chake ni shilingi 12,000/=

Sasa kuanzia mwaka wa 2 mpaka wa 6 cheti cha late *registration* aina hiyo ni shilingi 22,000/= na kuanzia miaka 6 na kuendelea na shilingi 32,000/=. Mhe. Spika, kilio kimekuja kwamba fedha hizi ni nyingi kwa wananchi wetu. Kwa kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwa asilimia 100, lakini utaratibu huu ndio uliowekwa na serikali ni *fees* na hizi zinakwenda kwenye mapato, sasa hatuwezi kuondosha moja kwa moja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama nilivyoahidi katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia naendelea kuahidi katika Baraza hili kwamba kilio hiki tutakichukua kwa ngazi zinazohusika, ili tupeleke kilio hiki na serikali hapo inapoona kwamba inafaa sasa kupunguzwa kutokana na kilio hicho basi tutarejea na tutawaambia wananchi wetu kutokana na matatizo hayo.

Mhe. Spika, ninachoweza kusema katika ofisi hii mambo muhimu ni hayo, ingawa kuna suala ambalo lilizungumzwa kuhusiana na wizi wa fedha shilingi milioni 2 katika Wilaya ya Kati ambazo ziliibiwa na Afisa mmoja ambaye anashughulika na suala la Vitambulisho.

Kwa kweli kesi hii Mhe. Spika ya zamani kidogo, lakini baada ya sisi kuipata na tulifuatilia. Kwa hivyo, huyu mtu ambaye amefanya kosa hili tayari ameshastaafu, kwamba alichukua fedha *immediately* akastaafu, sasa tumefuatilia zaidi ni kuwa bado hajachukua fedha zake za Kiinua Mgongo katika Wizara ya Fedha. Kutokana na hali hiyo, tayari tumeshaandika barua rasmi, ili fedha hizi za serikali zikatwe kutokana na Kiinua Mgongo chake Wizara ya Fedha na hilo litafanyika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, zaidi ili kukomesha suala hili nishaagiza kufanywe uchunguzi na hatua za kisheria baada ya kupatikana ushahidi wa kisheria basi hapo tutampeleka katika vyombo vya kisheria, ili iwe ni funzo kwamba suala hili hatuwezi kulivumilia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Ofisi ya Mrajis Pemba si ya ghorofa, kwa sababu si ya ghorofa basi si lazima kuwa na ngazi. Sasa kitu ambacho kilichofanyika mwanzo ile ofisi ilikuwa iwe ya ghorofa, lakini mshauri ambaye ni Engineer alisema kwamba pale hatuwezi kujenga nyumba ya ghorofa kutokana na hali ya ardhi

ilivyo. Kwa maana hiyo, hatukujenga tena nyumba ya ghorofa na tulijenga nyumba ya kawaida na hivyo hakuna ngazi yoyote pale. *(Makofi)*

Suala la mwisho katika ofisi hii Mhe. Spika ni kwamba je *late registration* Pemba itafanywa lini, kuna umuhimu wa mtu au watu wa Pemba kuja huku kwa *late registration*. Mhe. Spika, ni kweli wananchi wa Pemba wanapata tabu kwa late registration kuja Unguja.

Lakini ninachokiomba kwa Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, niwaarifu kuwa suala hili tumeliona, isipokuwa kuna utaratibu wake katika masuala ya *late registration*. Kwa hivyo, hivi sasa hatuwezi kusema lini *late registration* itafanywa Pemba.

Hivyo, ninachoweza kuahidi mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba tayari tumeshaanza kufanya utafiti wa namna gani huo utaratibu ambao unafanywa hapa Zanzibar, basi tuweze kuufanya Pemba bila ya kupata matatizo yoyote katika suala zima la *registration*, ili late registration kwa wale walioko Pemba lifanywe huko. Kwa hivyo, ninaahidi kwamba tutalichukulia hatua haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu Wakfu. Kwa kweli suala hili lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi kama vile Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, namshukuru, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Panya Ali Abdalla na wengineo.

Mhe. Spika, Wakfu kweli nako yako matatizo nakiri na ninakubali kwamba matatizo hayo kidogo yanawavunja moyo wananchi wetu. Lakini tatizo ni kwamba watu wenyewe wanaokaa katika nyumba hizi nao wanayo matatizo yao, kwa sababu unapopandisha bei.

Kwa mfano, tulipandisha bei kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lakini tulitoka shilingi 10,000/= tukenda shilingi 20,000/= kwa nyumba nyengine, kwa upande wa nyumba nyenigne tulikwenda mpaka shilingi 200,000/=, yaani inategemea nyumba yenyewe kama vile yenye duka au biashara, yaani inategemea hali ya nyumba ilivyo.

Sasa huyu tuliyempandishia kutoka shilingi 10,000/= mpaka 20,000/= halipi na wala hataki, yaani anayo madeni yanayofika shilingi 300,000/= mpaka 400,000/=. Kwa hivyo, mtu kama huyu anakaa kwenye nyumba na wala halipi na sisi hatutaweza kumtengezea nyumba ile na ukimwambia atengeneze hataki.

Kwa kweli kesi hizi si kwa shilingi 10,000/= mpaka 20,000/=, lakini hata hao wanaolipa shilingi 200,000/= hawalipi na hilo ni tatizo. Kutokana na hali hiyo, wengine tumeshaanza kuwapeleka Mahakamani, ili angalau tupate zile fedha, kwa sababu fedha hizi zinasaidia sana kwenye matengenezo pamoja na mambo mengine. Lakini wananchi wetu nao ni wagumu, yaani wanahisi kama Wakfu ni mali ya bure ya serikali kwa hivyo mtu atumie tu.

Kwa kweli Wakfu si mali ya serikali wala mali ya bure, isipokuwa Wakfu ni mali ya mayatima na lazima tujue na wao kama wananchi wa nchi hii, basi lazima wajue suala hili ili wawasaidie hawa wenzetu ambao wameekewa Wakfu. Sasa hilo ni tatizo ambalo nalo tunalipigia kelele na *Inshallah* tutafanikiwa.

Vile vile kuna matatizo mengine. Kwa mfano, mtu unamkodisha kwa shilingi 200/=, basi yeye anakodisha kwa shilingi 3,000/= au 4,000/= na hayo tumeyapata na hatua tayari tumeshaanza kuzichukua kwa watu wale kuwanyang'anya mara moja na tunamuachia yeye anaende Mahakamani na sio sisi na ikiwa atakwenda Mahakamani basi tutapambana huko kisheria, kwa sababu unapokodishwa hutakiwi u-*sublet* bila ya idhini ya mkodishaji. Kwa hivyo, hayo tumeyakuta na tunayachukulia hatua. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba juzi siku ya Jumamosi tarehe 02/07/2011 tulikuwa na *Workshop* ya Wakfu na Mali ya Amana. Miongoni mwa mambo yetu tuliyokubaliana ni kwamba tumejipa miezi sita, ili masuala hayo yote ya nyumba kuhusu kodi, upangishaji, stokechanging ya nyumba zenyewe zile yawe yameshakamilika.

Kwa hivyo, *Inshaallah* baada ya pindi cha miezi sita tutafika pahala na tutajua ni nyumba ngapi za Wakfu, nani wanaokodi, wapi waliopangishwa zaidi na mambo kama hayo, ambayo naamini yatatusaidia hata sisi ku-*generate funds* ambazo baadaye tutaisaidia serikali, kwa sababu hivi sasa serikali inatupa ruzuku nyingi sana ambapo sisi hatutakiwi tupewe ruzuku. Kwa hivyo, hili tunalifanya, ili tuweze kusaidiana. *(Makofi)*

Suala la mwisho katika Wakfu ni kuhusu mambo ya Hijja. Kwa kweli suala hili ni kuwa fedha zimekuwa nyingi, ni kweli fedha zimekuwa nyingi na zamani ilikuwa dola 1,000/= au 2,000/= unaweza kwenda Hijja, lakini hivi sasa *almost* karibu dola 3,000/= na zaidi.

Lakini utaratibu uliopo hivi sasa Saudia Rabia kidogo umekuwa mgumu si kama ule wa zamani tulipokwenda sisi ukifika Mina unalala chini na utaratibu huo siku hizi haupo. Kwa kweli ukifika Mina siku hizi kuna mahema mazuri

yenye magodoro, *Air Condition* pamoja na chakula chako na kitu ambacho zamani hakikuwepo, sasa yale lazima uyalipie ziada na watu ndio wanayoyataka bila ya shaka zile gharama zitaongezeka pamoja na mambo mengine.

Kwa mfano, bei za ndege sote tunajua kwamba zimepanda, kwa sababu mafuta ya ndege pamoja na mambo mengine yote yamepanda, sasa kama zimepanda, basi huwezi kumchukua Hujjaji na kumpunguzia bei. Mhe. Spika, Mahujjaji wote takribani wanapenda wakae karibu na Misikiti miwili hii, yaani Msikiti wa Makka na Madina. Kwa hivyo, nyumba za sehemu zile zina *market*, yaani gharama zimepanda kwa hiyo lazima na wewe upandishe.

Lakini zaidi Sheria ya Saudia Rabia siku hizi ni kwamba hakuna Hujjaji atakayelala chini katika nyumba. Kwa hivyo, hata hizo nyumba ambazo tulizokuwa tukikaa karibu na Misikiti lazima ziwe na vitanda wakati zamani kulikuwa na magodoro tu na hivi sasa kisheria ni kosa. Kwa maana hiyo, kama kuna vitanda basi wale wenye nyumba wanapandisha bei. Hivyo, yote haya yamefanya gharama za Makka kwa ajili ya kwenda Hijja zipande, lakini zimepanda kwa faida ya wale Mahujjaji.

Mhe. Spika, kweli nakubali kidogo imepanda, lakini tuangalie zile *facilities* ambazo tunapewa wakati tunapofika kule. Mhe. Spika, najua kwamba ni kubwa, lakini *Inshaallah* idara yetu itajaribu kufanya *negotiation* ambazo zinaweza kupunguza kidogo, lakini tujue gharama hizo zimepanda kutokana na mambo hayo. *(Makofi)*

Vile vile suala la Mufti pia lilizungumzwa. Mhe. Spika, hivi sasa tunajaribu kutizama idadi ya vyuo vilivyopo kwa Unguja na Pemba na tukeshakuvijua tuna idadi gani, basi tutakuwa na idadi kamili na tutaweza kuvi-*monitor* shughuli zao na hapo ndipo tunaweza kutoa misaada kwa vyuo hivi kwa kadri hali yetu itakavyokuwa.

Mhe. Spika, pia lilizungumzwa suala la kuteuliwa kwa Mufti naamini tayari nimeshalizungumza hilo. Sambamba na hilo kuna suala jengine ambalo lilizungumzwa kuhusu ile Dua ifanywe kila mwaka na wala si jambo baya. Lakini unapofanya Dua kila mwaka maana yake unaiweka katika *System* ya Serikali, yaani kama ya kitaifa kwa sababu ya kila mwaka.

Kwa hivyo, si jambo baya tutalichukua kwenye serikali na pale tutakapopata kibali basi tutaomba Dua kila mwaka katika tarehe ambayo tutakubaliana.

Mwisho katika suala hili kulikuwa mambo ya migogoro. Mhe. Spika, nafikiri migogoro tuliyopata kama tulivyosema ni 15 na 13 tumejaribu kuitatua na miwili bado inaendelea. Lakini Waheshimiwa Wajumbe wakasema kuna migogoro mingi, ni kweli lakini tatizo lenye ni kwamba migogoro hii bado haijakuwa ripotiwa kwetu. Kwa hivyo, wanaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, tukipata migogoro kama hii basi iripotiwe kwetu, ili tuweze kuitatua.

Mhe. Spika, kuna suala la Hakimiliki. Kwa kweli suala hili kama tulivyosema kwamba tunajaribu kuwaelimisha wananchi wetu kupitia redio na televisheni na tutaendelea kuwaelimisha. Kwa hivyo, Hakimiliki inalindwa kwa sababu ni wajibu wa nchi kulinda kwa dhati ufundi na sanaa unaotokana na watu wetu. Hivyo, tutaendelea kuzilinda pamoja na kuzitetea kwa maslahi ya watu wetu walioonesha vipaji hivyo.

Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alizungumzia kuhusu suala la ujenzi wa ofisi na wala sipendi kulirudia lakini jibu moja tu napenda nimuhakikishie Mhe. Hija Hassan Hija kwamba fedha hizo za mwanzo tumezipata katika bajeti yetu tuliyonayo ambayo tunaimaliza hivi sasa, kuna sehemu nyengine ambazo tulifanya *reallocation* ili kuhakikisha kwamba *phase* ile haikwami njiani. Mhe. Spika, hivi sasa ninayo *blackdown* hii ambayo naweza kumpa baadaye ambayo tumetumia shilingi 11,904,180/= na fedha hizi zote zilikuwemo katika bajeti yetu na kufanya *reallocation* kidogo.

Mhe. Spika, fedha za mishahara na fedha za afisi ya jengo nashukuru Mhe. Waziri amelizungumza kwa urefu, imezungumzwa kidogo lakini wengine walisema kuna katibu tu mbona huyu Mwenyekiti hayupo na wajumbe, napenda niseme tu kwamba Mwenyekiti tunae zamani ambae aliteuliwa katika mwaka wa 2010 mwanzo mwanzo.

Kwa hivyo, mwenyekiti na katibu ndio aliteuliwa hivi karibuni hawa sasa wanashirikiana kwa pamoja kukamilisha utaratibu wa ofisi hii, tumeshapata ofisi kama tulivyosema ya *EACROTANAL*. Kwa hiyo, tayari tumeshaanza kutafuta wafanyakazi wengine na tunaamini baada ya bajeti hii kupitishwa na kupata fedha utaratibu mzima wa shughuli nzima wa *Law Review Commission* utaanza kikamilifu.

Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kuhusu miswada suala hili ni zuri tumelitizama katika Afisi yetu na katika Wizara yetu, kwamba miswada hii sasa tunayoileta katika Baraza yote tunaisoma kwa siku moja, yaani *fast reading, second reading and third reading*. Kwa kweli hii haitupi

nafasi nzuri ya kuwapa wadau pamoja na wananchi wetu wa jimbo na hasa pale miswada inapochelewa, tumeona tatizo hili la ucheleweshwaji wa miswada tutajitahidi tukijaaliwa miswada haitochelewa.

Lakini sisi tukasema ili kuwapa nafasi zaidi wananchi basi suala hili tutalipeleka rasmi kwako wewe Mhe. Spika, ili tubadilishe tukikubaliana na waheshimiwa wawakilishi, tubadilishe kanuni zetu ili mswada unaletwa leo katika kikao hiki tunauweka kwenye Baraza halafu kikao chengine kinachofuata ndio unasomwa na hii itapata nafasi ya kushauriana na wananchi wetu. Mhe. Spika, hilo tutalileta rasmi katika vikao vyetu vya Baraza ili tutizame uwezekano na baadae tunaweza kupata ufumbuzi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa haya niliyoyasema na naamini wajumbe wameridhika na majibu yangu, lakini kuna mambo mawili ya mwisho ninayotaka kuyasema.

La mwanzo ni suala la Mhe. Makame Mbarouk Mshimba, yeye alileta lalamiko lake kama alivyosema na akatoa vielelezo na vielelezo hivi na mimi alinipatiaa na nikweli inasikitisha Mhe. Spika, ingawa hii kesi ni yazamani tokea 1978 na ya mwisho ni mwaka 2007.

Huyu mwananchi wetu sote tunajua zamani alikuwa akifanya kazi kwa Muhindi baada ya yule Muhindi kuondoka akamtunukia ile nyumba kama ni zawadi, wazee wetu hatuwalaumu akaona yeye ameshatunukiwa basi tena ndio zawadi sasa katika *registration* hakufanya chochote anaona yeye ni nyumba yake tu masikini ya mungu.

Sasa mwisho watu wakamwambia nenda kaifanyie *registration* sasa wakati wa kwenda kuifanyia *registration* sijui kilipita kiatu gani Wizara ya Majenzi wakati huo tarehe 30/4/2004 wakamuandikia kwamba nyumba hii imetaifishwa kwa hivyo sio yako tena.

Yule mzee akasema imeshataifishwa kwa hivyo sio yake tena, sasa na mimi nilikwenda nikafanya utafiri ni kweli ilitaifishwa kwa *local Notice No.4* ya mwaka 1978. Kwa hivyo, kisheria ile nyumba sasa hivi ni ya serikali, lakini huyu mtu aliyemtaja hivi sasa kwamba anataka kuinunua akafanya manyago, manyago yenyewe ni kwamba alikwenda Wizara ya Majenzi na akawaambia Wizara ya Majenzi kwamba hii nyumba naitaka, sasa hapa ndio suala langu linapokuja la kisheria, kama hii nyumba ilitaifishwa au ni kweli hatua nyengine zilichukuliwa au hazikuchukuliwa.

Kwa sababu kwa mujibu wa *document* nilizokuwa nazo baada ya kufanya utafiti ni kwamba nyumba hii tarehe 23 April, 2007 aliuziwa tena huyu tuliyesema kwamba nyumba yake imetaifishwa yaani serikali imemuuzia yeye kwa shilingi 5,000,000/= na yeye anasema hajauziwa wala hana habari yoyote ile kwa hivyo hapo pana udanganyifu.

Lakini cha kusikitisha zaidi ni kwamba hii nyumba aliuziwa tarehe 23 April, 2007 lakini tarehe 22 Jun, 2007 huyu mzee akamuuzia huyo bibi aliyetajwa kwa shilingi 15,000,000/=. Sasa anasema mimi sijamuuzia mtu nyumba na kama nimemuuzia hizo milioni kumi na tano zangu mie ziko wapi. Katika wauzaji kuna Juma Ali Kidawa mwenye *ID* No.0300060722 ndiye aliyemuuzia huyo bini kwa shilingi milioni 15, mimi nimemwita huyu Juma Ali Kidawa akaniletea kitambulisho chake ambacho sicho kilichoandikwa humu, kwa hivyo huyu muuzaji sie sahihi aliyotia humu katika fomu ya kuuza siyo, kwa sababu humu kaandika kwa mkono huku kaandika kwa dole na madole haya mawili katika ile siku aliyouziwa yeye kwa Shilingi milioni 5 na siku aliyoiuza kwa Shilingi Milioni 15 madole haya hata mimi niliyekuwa sio *experts* wa *finger print* ni kwamba yanatofautiana.

Sasa ninachotaka kusema Mhe. Spika, ni kwamba uuzaji huu ulipita kinyemela huyu mzee pengine alinyang'anywa haki yake nasema pengine kwa sababu hatuja maliza uchunguzi tukaona, lakini ninachopenda kusema kwamba hili tutalifuatilia na tutahakikisha kwamba huyu mzee ikiwa ni haki yake atapata na hawa maafisa wa Wizara ya Majenzi pamoja na Wizarani kwangu watu wa *registration* kule tukigundua kwamba wao walishiriki katika kufanya matatizo haya nawahakikishieni tutawachukulia hatua, hatua hizo tutazichukua kwa udhati hasa ili iwe ni mfano kwa watu wengine. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makame Mbarouk Mshimba astahamili na hili tutalichukua kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la mwisho ni suala la katiba najua watu walizungumza kwa hamasa kubwa sana katika kujenga nchi yao, mimi nimefurahi na hamasa zile tunazikaribisha na zaidi ya zile tunazikaribisha, ninachotaka kusema kama alivyosema Mwanasheria Mkuu ni kwamba hivi sasa hatujaanza suala la mchakato wa katiba hivi sasa tumo katika mchakato wa kuandaa utaratibu wa namna gani hiyo katiba itafanywa, na utaratibu huu ndio tunaozungumza hivi sasa na kama nilivyowaambia tulivyozungumza Bwawani na Haile Selassie maoni yale tumeyachukua na tumezungumza nao tukakubaliana.

Lakini Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hija wanasema sio *bush layer* lakini ni *Town layer* najua kwamba sheria ina matatizo na sisi hivi sasa ndio mliotupa jukumu hilo Ofisi yangu na Wizara yangu pamoja na ofisi ya

Mwanasheria Mkuu, kwa hivyo lazima sisi tu-*act* kwa niaba yenu. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua namkumbusha kidogo tulipokuwa Bagamoyo tulikuwa tunazungumza kwa Kiswahili katika miafaka tunakwama kwa neno moja tu la Kiswahili na tunakaa siku mbili kila mtu pake, je leo Kiingereza na tena Kiingereza hichi cha kuhakikisha kwamba maslahi ya Zanzibar yanalindwa lazima tutachukua muda, ndio maana katika hotuba yangu nikasema kuna mambo madogo madogo tunayoyajadili sasa pengine koma imeandikwa hivi sisi hatukubali, pengine neno hili limeandikwa hivi sisi hatukubali lazima itachukua muda tuzungumze. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua msimamo wangu katika Zanzibar hii, Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua msimamo wangu katika masuala ya muungano na namhakikishia kwamba sibadiliki na msimamo ule hata siku moja. *(Makofi)*

Mimi nitaitetea Zanzibar kwa nguvu zangu zote ninavyosema hapa ni kwamba suala hili Mhe. Spika, ni suala ambalo tunalijadili hivi sasa ili haya mambo madogo madogo yaliyojitokeza katika huo mswada wa kuweka utaratibu wa kutafuta katiba mpya uwe ni mzuri, hakuna siri yoyote wala hakuna kificho chochote kile labda Spika, hakuna siri wala hakuna chochote. Kinachofanywa hivi sasa ni kujaribu kupata utaratibu mzuri na makubaliano mazuri hasa katika sheria ile namna ilivyoandikwa, tukishakufanya hivyo tutawaarifu wawakilishi wetu kwa sababu hapa mimi siwezi kuja hapa nikawaambia tumekubaliana hivi lakini neno hili nahisi halikukaa vizuri mtaniona sijafanya kazi yangu, wala Mwanasheria Mkuu mtamuona hajafanya kazi yake.

Lakini tunapokuja tunawaambia tumekubaliana haya na haya kama yalivyozungumzwa pale mnasemaje, hapo ndipo tutakapofanya mnasemaje, nawahakikishie waheshimiwa wajumbe kwamba kwasababu hizo mswada huo wa kikao hiki cha bunge hili haupelekwi katika kikao cha bunge itapelekwa katika kikao cha octoba na hiyo ndio imetupa nafasi zaidi sisi kwa sababu ya kutatua matatizo madogo madogo. Kwa hivyo msiwe na wasi wasi waheshimiwa wawakilishi na wananchi sisi tuko hapa tutalinda maslahi ya Zanzibar na maslahi ya wananchi wetu kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachoomba kusema ni kwamba mambo hayo yakimaliza ambayo hivi sasa tumewapelekea wenzetu kuwaambia jamani mbona hapa pameandikwa hivi na hii tafsiri yake itakuwa hivi na hivi wataturejeshea tutakubaliana, tukishakubaliana hapo itapelekwa bungeni kuarifiwa kabla ya kwenda kujadiliwa katika bunge na italetwa katika Baraza katika kikao cha kawaida kwenye semina kuwaarifu na hapo tutafahamiana. Hapo tutapata maoni yenu na maoni ya wananchi wengine kwa sababu nyinyi ndio mtatoa maoni yao.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba suala hili halijachelewa wala halina usiri lakini tunachukua muda ili kuhakikisha kwamba yale tunayoyataka kwa Zanzibar yanatekelezwa au yanaingizwa yote kwa pamoja, ninachopenda kuwahakikishia Mhe. Spika, ni kwamba suala hili sisi kama ni Wazanzibari ofisi yangu, mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu, tuko kidete hatutokubali hata siku moja kufanya visivyo. Na maoni ya wananchi bila ya shaka tutayaheshimu kwa kadiri ya uwezo wetu na kadiri ya yalivyoletwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nawashukuru sana Waheshimiwa wajumbe kwa kunisikiliza naamini nimejaribu kuelezea mengi kidogo, lakini kuna mengine ambayosikuyaelezea naomba msamaha kwa sababu wakati wenyewe ni mdogo lakini ishaalla tumeyarikodi yote, wafanyakazi wangu wameyachukua na tutayafanyia kazi kwa mujibu wa utaratibu ambao tumeuwekea.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria yakubaliwe. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tunakushukuru sana kwa ufafanuzi wa hoja mbali mbali uliokwisha kutoa hapa, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Spika, kwa kuwa baraza lako tukufu limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 201	Utawala Unguja	42,000,000
Kifungu 301	Ofisi Kuu Pemba	6,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**48,000,000**

FUNGU	**36**	**-**	**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**
Kifungu 011	Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali		263,415,000
	JUMLA YA FUNGU		**263,415,000**
FUNGU	**14**	**-**	**MAKAMA KUU ZANZIBAR**
Kifungu 201	Utawala Unguja		832,000,000
Kifungu 301	Ofisi Kuu Pemba		357,000,000
Kifungu 601	Ofisi ya Kadhi Mkuu		125,000,000
	JUMLA YA FUNGU		**1,324,000,000**
FUNGU	**15**	**AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR**	
Kifungu 201	Utawala Unguja		612,077,000
	JUMLA YA FUNGU		**612,077,000**
FUNGU35	**OFISI YA MKURUGENZI WA MASHITAKA**		
Kifungu 201	Utawala Unguja		550,000,000
Kifungu 202	Kituo cha Mafunzo ya utafiti wa Sheria		50,000,000
Kifungu 301	Ofisi Kuu Pemba		174,000,000
	JUMLA YA FUNGU		**774,000,000**
FUNGU	**36**	**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**	
Kifungu 011	Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali		273,579,000
Kifungu 012	Ofisi ya Mrajis Mkuu Pemba		62,702,000
Kifungu 301	Ofisi Kuu Pemba		282,178,000
Kifungu 401	Idara ya Mipango sera na Utafiri		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nishukuru sana maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri na pia Mwanasehria Mkuu katika kujibu masuala yetu mbali mbali zikiwemo suala yetu mbali mbali likiwemo suala la mchakato wa kuanzishwa kwa katiba mpya ya jamhuri ya Muungano.

Suala langu hapa kwanza nataka niwahakikishie Mhe. Mwanasheria na Mhe. Waziri kwamba naelewa kabisa kwamba tuna *stage* hizi mbili, tuna *stage* ya kuweka uwanja safi na kuweka kanuni za mchezo na mchezo wenyewe. Kwa

hivyo nataka niwahakikishie kwamba kwa mchazo wenyewe wachezaji wamejipanga vizuri sana tukijaaliwa.

Lakini katika hili la kuweka uwanja safi la kanuni Mhe. Mwenyekiti hapo ndio kwenye masuala yetu na tulipouzulia nikiwemo na mimi katika mchango wangu ni kiasi gani haki za Zanzibar zinalindwa hivi sasa wakati wa kuandaa kanuni na kuweka uwanja safi. Na nilisema katika mchango wangu kwamba nilipomsikiliza mwanasheria Mkuu pale Bwawani siku ile nilikuwa na homa sijui ilikuwaje au Mwenyezi Mungu alijua kwamba nikenda pale mambo yangekuwa makali zaidi. Lakini nilikuwa nikifuatilia mjadala nilipokuwa nyumbani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba suala la kuandika Katiba mpya ni sasa na kuri- . *negotiate article of union* Sasa nikauliza kwamba kwa utaratibu huu haki zetuza Zanzibar zimelindwa kiasi gani ndio nikasema kwamba kuna taratibu zinapaswa hapa, sasa nimesikiliza maelezo yao nimeridhika sana. Sasa lililobakia niliuliza nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi katika *process* hii.

Nimezungumza hilo kusema kwamba kama tunazungumza *process* hii ni sawa na kuanza upya katika yale makubaliano, na hata nikisoma katika kitabu cha waziri katika hotuba yake kwamba msingi wake ni mkataba wa muungano ambao wakati ule ulikuwa unahusisha Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi katika kuthibitisha.

Sasa pamoja na majibu yao naomba nielezewe kwa ufasaha zaidi, nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi zaidi ya ile ya kuambiwa kwamba tutajulishwa wao wakishakamilisha zile taratibu, lakini niseme hivi sasa ule mswada kwa wenzetu katika bunge unapitia taratibu na bunge kama ninavyojua lina nafasi mbili. Lina nafasi ya kuwa bunge la muungano kwa mambo yote ya muungano lakini pia bunge lile ni la Tanganyika kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano.

Sasa katika *process* hii wenzetu wanashirikishwa nikauliza Baraza la Wawakilishi na Kamati ya Katiba Sheria na utawala Bora kiasi gani inashirikishwa katika huu utaratibu wa upande wetu sisi wa Zanzibar kwa kuweka hizo kanuni safi, kwa kuweka uwanja safi. Kwa hivyo nilikuwa naomba niwekewe wazi nijue kwamba ule msingi uliotumika pale mwanzo katika muungano wetu unaheshimiwa na Mhe. Waziri mwenyewe kakiri kwamba hatuna nia ya kurejea yaliyokuwa yamepatikana huko nyuma hayatopatikana katika kipindi hicho cha kuandika katiba mpya ya jamhuri ya Muungano.

Kwa hivyo nilikuwa nomba niwekewe hilo tu nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi kwa ujumla wake, sio kuja kuidhinisha mswada ambao umepitishwa Bungeni hivi sasa wakati tunaandaa mswada wa sheria ya Mapitio ya Katiba. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti hivi sasa hatuandai katiba hivi sasa tunaandaa utaratibu wa namna gani hayo majadiliano ya katiba yatakwenda, wakati huo katika huu utaratibu ambao tunaupigania uwe ndio itaelezwa hasa nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi katika utaratibu huo, utaratibu huo katika kuandaa masuala haya unajua kwamba kuna *constituter assembly* sasa hiyo pia lazima tuiwekee utaratibu kabisa. Je, itawashirikisha vipi Wazanzibari haya ndio mambo ambayo sasa hivi tunayaandaa.

Lakini katiba yetu katika kifungu cha 32 pia inatoa utaratibu wa Baraza la wawakilishi kushiriki katika hili hapo baadae, lakini kwa hivi sasa ni suala ambalo tunaliandaa tunaweka utaratibu namna gani Wazanzibari, wawakilishi washiriki katika uandaaji wa katiba hiyo. Ninachosema ni kwamba utaratibu huo tutahakikisha kwamba Wazanzibari wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanashirikishwa ipasavyo katika kuandaa katiba hii.

Mhe. Ismai Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti hili linarejewa sana naomba nisisitize kwamba kwa elimu yangu ndogo ya sheria naelewa hizi tofauti za *process* hizi mbili, najua kwamba hivi sasa hatuandiki katiba mpya. Nataka nieleweke labda niseme hivi ili tuelewani kwa lugha waliyoleta wao, kama kanuni mbovu Mhe. Mwenyekiti, za mchezo na uwanja hauko sawa huwezi kupata mchezo ambao utawaridhisha timu zote mbili, sasa hapo ninachozungumza mimi ni hii taratibu ya kuweka kanuni sizungumzi *roll* ya Baraza katika kuja kuiridhia au kuipitisha katiba, nazungumzia roll ya baraza hivi sasa katika kuweka hizo kanuni na uwanja safi.

Mhe. Mwenyekiti suala langu hili naliuliza kwa sababu kama nilivyosema kwamba kwa maelezo yao wenyewe ambao ndio viongozi wetu tuliowategemea katika suala hili, kwamba *process* hii ni sawa sawa na kuwa tunaanza kule tulikotoka, sasa ninachosema labbda niseme Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa anachangia siku ile Bwawani alisema kwamba katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu cha 98 kinaipa nafasi Bunge kurekebisha vifungu vya katiba au masharti ya katiba yaliyopo hivi sasa, lakini hakitoi fursa ya kuandikwa katiba mpya. Kwa maana nyengine bunge lenyewe ni zao la katiba hii akasema kwamba lazima kutafutwe utaratibu ambao utahakikisha kwamba kama katiba haitoi nafasi kwa bunge kurekebisha katiba na kama haitoi nafasi kuandikwa katiba mpya katiba hiyo hiyo haiwezi kuipa mamlaka bunge kutunga sheria ya mapitio ambayo yatapelekea kutunga sheria mpya.

Sasa ndio nikasema kama ni hivyo huo utaratibu wa hii sheria ya Mapitio ya katiba sio sheria ya kutunga katiba mpya, Je, Baraza la Wawakilishi katika kuiweka hakuna *roll* katika hili, kwa sababu kama ulivyosema katiba hii sio milki ya upande mmoja wala sio ya bunge la Muungano katiba ya Jamhuri ya Muungano ni milki kwa Watanzania wote waliokuweko Tanganyika na waliokuweko Zanzibar, saa sisi Wazanzibari wahusika ni Baraza la Wawakilishi ndio nikasema katika kuipata hiyo sheria ya mapitio ya katiba sio katika kutunga katiba mpya, *mineral* ya Baraza la wawakilishi naomba nielezwe hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti mimi nafikiri Mhe. Mjumbe afahamu kwamba kila kitu kina utaratibu wake, hivi sasa utaratibu huo wa kuandaa upo katika Wizara ya Sheria na katiba na Wizara kama tulivyomwambia tumezungumza na wenzetu pamoja na hilo suala analolisema, sasa mimi kama ni Waziri wa katiba siwezi kuja katika Baraza lako tukufu nikawaambia jamani hili tunasemaje.

Ni mimi ninayetakiwa nilione niwambie wenzetu halafu hapo baadae mimi ninapokuja kuripoti katika Baraza kwamba tumefikia hapa na hapa ndio wao wataweza kusema kwamba hili tunalikubali au hili tunataka hivi, sasa hayo hata hicho kifungu cha 98(a) kinachozungumzia hilo *legality* ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kimo katika mazungumzo yetu tukishakumaliza hayo tutakuja kwa Baraza la Wawakilishi tuwaambie yale ambayo tumekubaliana kuzungumza, haina maana kwamba tukija sisi kuwaambia nido fainali wao watakuwa na mdomo hapo wa kusema na kutoa maoni.

Sasa tuko katika *stage* ya mwanzo ni sisi tunaofanya *ground up* baada ya hiyo *ground up* tutawaletea Waheshimiwa Wawakilishi, hatuwezi *ground up* tukawaambia waheshimiwa Wawakilishi wafanye itakuwa sivyo kiutaratibu, sisi kama ndio watumishi wao tufanye *ground up* tukishakubaliana na wenzetu tutawaambia wenzetu fumefikia hivi na hivi na hilo nahakikisha kwamba tutafanya na tutaleta Baraza la Wawakilishi, tukileta hapo wao watakuwa wanatoa michango yao. Kama wanavyofanya Bunge wao hawajapelekewa hivi sasa hivi sasa kuna mchakato baina ya Mwanasheria Mkuu wao na Mwanasheria Mkuu wetu, Wizara ya Katiba yao na Wizara ya Katiba yetu baadae ndio ao wataarifiwa na sisi tutawaarifu ndio utaratibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sipendi nizozane na Mhe. Waziri lakini kwanza nafurahi katika majibu yake kaieleza *roll* ya Baraza ndilo nililokuwa nalitaka, lakini kidogo sikubaliani nae katika maelezo yake kusema kwamba hivi sasa wenzetu pia hawajalipata. Wenzetu kama Bunge kamati ya Katiba na Sheria inashirikishwa hivi sasa na katika *process* zote zilivyoanza na

wanajua kinachoendelea. Lakini nasema kwa sababu sitaki nionekane kama nina tatizo binafsi na Mhe. Waziri naomba niridhike na maelezo yake kwa sasa tutakuja kuelewana huko mbele ya safari.

Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Kwa kuwa ameshakubali sawa lakini kwa taarifa yake tu- *differences* mambo yanayohusu Muungano na mambo yasiyohusu Muungano, hili ni suala la Muungano Kamati ya Katiba na Sheria ya kule ya Bungeni ndio inayopewa jukumu la kushughulikia haya ndio maana wakaleta huku, baadae hapo sisi ndio tutawaarifu Baraza la wawakilishi

Kifungu 401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	74,554,000
Kifungu 501	Ofisi ya Mufti	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi nimeridhika sana maelezo ya Mhe. Waziri lakini kulikuwa kuna kitu kimoja sikukisikia katika hii Ofisi ya Mufti.

Katika mchango wangu nilisema kwa sababu kuna vipindi hivi tunavyokaa bila ya kuwa na viongozi kama Kadhi Mkuu au Mufti, ingefaa ile *secretariat* ya ofisi ikaundwa uzuri sana ili ikaweza kufanya kazi zake kama kawaida hata kama yule Mufti hayupo. Kwa sababu kuna shughuli za Kiofisi za kikawaida zinaweza zikaendelea na wakati Mufti bado hajachaguliwa au hajateuliwa.

Mhe. Waziri kwa hili hakulieleza vizuri, ipo hii *secretariat* inafanya shughuli zake au *establishment* yake bado, hapo ndio sijaifahamu kidogo. Naomba maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mwakilishi. Ni kweli sikulitaja lakini katika maelezo yake yapo na mimi niliweka hizo notes zangu. *Secretariat* ipo. Hivi sasa Ofisi ya Mufti inaendelea hata kama Mufti hayupo, yupo Katibu wa Mufti, yupo Shekhe ambaye anatoa mawaidha, wapo Wakurugenzi au wakuu wa Idara ambao wote hawa wanakutana likitokea lolote lile linakwenda. Ndio maana mpaka sasa hatujalala katika ofisi hii. Shughuli zinaendelea kama kawaida kwa kupitia hii *secretariat* anayoisema yeye. Kwa hiyo *secretariat* hiyo ipo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nashukuru sana Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu 501	Ofisi ya Mufti	140,435,000
Kifungu 601	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri mwenyewe. Kwa kuwa unakumbuka nilisema nitazuia fungu la hotuba hii lote kwanza naomba kusema kwamba nimebadilisha msimamo wangu. Sasa naunga mkono hoja mia kwa mia.

Pili nitaka kidogo anielimishe Mhe. Waziri huu ujenzi wa hii ofisi utajengwa sehemu gani.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru jengo hili linajengwa Mazizini pale penye Ofisi ya Vitambulisho kabla hujafika Ofisi ya Vitambulisho pana nafasi kubwa sana ile ni nafasi iliyowekwa kwa jengo hili. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu nilikuwa nataka nijue kwa sababu nilikuwa nina wasi wasi kwamba yeye anatuomba fedha kwa ajili ya hatua ya pili. Lakini tumepita pale tumelikuta jengo linaendelea kwa kasi sana.

Nilikuwa nakutoa wasi wasi tu kwamba kuna mawasiliano baina ya Wizara ya Fedha, mtoa fedha na wizara yenyewe. Kwa sababu huku wanatwambia wanatuomba lakini huku ujenzi unaendelea kwa kasi sana. Pamoja na hayo naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, jengo analosema yeye silo. Lile ni jengo la vitambulisho *opposite* na ile ofisi ya vitambulisho. Lakini kwa mfano unapita kwenda kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mkono wa kushoto kabla hujafika jengo la vitambulisho. Yaani tumebanana na jengo la vitambulisho. Hayo ndiyo yale matayarisho niliyosema kwamba tumeshaanza kuyafanyia michoro. Tuna ushirikiano mzuri na Wizara ya Fedha katika suala hili.

Kifungu 601 Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kama idara hii ndio inayozuia mshahara wa Mhe. Abubaka naomba nimrudishie fungu lake la mshahara wake. Suala langu lilikuwa halipo hapo.

Nadhani hili zaidi atatusaidia Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu ni rais hoja hii lakini katika majibu alijibu Mhe. Waziri wa Fedha. Lilihusu suala la mafungu yaliyotengwa kwa ajili ya mishahara kwa zile Idara tatu kubwa. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini hata na wao wafanyakazi wenyewe wa Wizara

ya Katiba kupitia Idara hii ya Utumishi na Uendeshaji. Kuna mapungufu ya mahitaji ya mishahara kama yalivyo kabla hayajaongezwa kwa miezi kadhaa ambalo lilizungumzwa hili katika maoni ya Kamati yetu ya Katiba Sheria na Utawala.

Hata mimi katika mchango wangu nilizungumza. Suala langu lilikuwa ni moja katika majibu yake Mhe. Waziri alipokuwa akisaidia kutoa ufafanuzi alisema kwamba hakuna mshahara utakaokosekana. Nakubali lakini hebu tusaidiwe. Inakuwaje katika kupanga makisio. Kwa mujibu wa mahitaji ya hivi sasa ya wafanyakazi ambao wanajulika kila Wizara wanao na kwa viwango vya sasa kabla ya nyongeza ambayo pengine ikitokea ile *adjustment* ndio unaweza ukasema hujui utaongeza kiasi gani.

Lakini kwa hivi sasa kwa nini katika kupanga kasma za wizara, hupangwa kasma ambazo zina mapungufu ya kitu cha msingi kama cha mshahara kwa miezi mitano, miezi mitatu kama ilivyoonekana katika baadhi za Idara zilizokuwemo katika Wizara hii na isiwe kwa ukamilifu. Halafu ile *adjustment* ndio ianayosubiri lile fungu ambalo lipo katika Wizara ya Fedha.

Naomba maelezo katika suala hili Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kumsaidia Mhe. Mwakilishi Ismail Jussa kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka Mhe. Jussa akubali kwamba tuna zoezi kubwa sana sasa hivi kupitia Wizara ya Utumishi ya kuhakiki watumishi wa umma. Zoezi hili ndilo litakalo tupa uwezo sasa muono wa kuelewa kila taasisi ina idadi gani ya wafanyakazi. Suala ambalo ambaliona yeye kwamba kuna upungufu lisimpe wasi wasi. Kuna taasisi ambazo kama atakumbuka wakati wa Waziri wa Utumishi wa Umma alipokuwa anafanya majumuisho zilidhihirika kwamba baadhi ya watumishi waliambiwa katika fomu wasijaze mishahara yao itajazwa na fiongozi. Hii ina maana kwamba tayari kuna udanganyifu katika eneo hili la mishahara katika kwa taasisi mbali mbali.

Zoezi hili litatupa sisi uwezo wa kuweza kuelewa kila taasisi hasa inahitaji kiasi gani cha mshahara. Nataka nirudie kumuhakikishia kwamba zoezi hili sasa limeshakamilika na narudia tena kusema hakuna mtumishi wa umma atakaekosa mshahara. Baada ya hapo *adjustment* itakuwa sasa tunakwenda na *adjustment* ya uhakika kabisa kuliko hata ambavyo tungetarajia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa uhakikisho huo na kwa msingi huo huo ili niruhusu tuendelee naomba kauli ya Mheshimiwa nadhani katika hili vile vile nitaomba kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Tumeliuliza hili kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Tulipokuwa tukipokea ripoti ya Kamati hii tuligundua suala kama hili lilijitokeza mwaka jana. Kwa hakika katika baadhi ya Idara au Afisi ambazo zipo chini ya Wizara kwa mfano Ofisi ya *DPP* walilazimika kutumia fedha zao wa *OC* ili kufidia ile sehemu ya mishahara na kuathiri sehemu za maendeleo au shughuli nyengine ambazo zilikuwa za utendaji kazi pale katika Ofisi. Kwa sababu kahamisha fungu la OC yaani *Other Charges* kupeleka kufidia lile fungu la mishahara ambalo lina upungufu. Sasa nilikuwa naomba kauli ya Mhe. Waziri atuthibitishie kwamba mwaka huu hilo halitotokea na kwamba fedha zote ambazo zimepangwa kwa *Other Charges* zitatumika kwa shughuli zake na mishahara itatoka kule ambapo inapaswa itoke. Ili tupate kuendelea Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kama nilivyokuwa namsaidia Mhe. Waziri wa Katiba awali kwamba katika kifungu cha Mfuko Mkuu tuna fedha tumeiweka pale kwa ajili ya kuweza kuangalia maeneo ambayo yatakuwa na mapungufu katika mshahara. Sidhani kama tutakwenda katika OC kwa sababu fedha pale zipo. Baada ya zoezi hili tutakuja ambalo tumelikamilisha na Wizara ya Utumishi ndio tutakapokuja sasa tutaangalia wapi ambapo pana mapungufu ya mshahara. Naamini kuna taasisi nyengine zinamshahara mwingi zaidi kuliko watu tulivyowapa. Kwa hivyo nazo kule tutaziondoa tuzirejeshe huku ili tuzipange kwa wale ambao wenye upungufu. Kwa hivyo nataka nimuhakikishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba asiwe na wasi wasi ya hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Tuendelee Mhe. Mwenyeketi, nashukuru.

Kifungu 601	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	438,552,000
Kifungu 701	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Unguja	229,950,000
Kifungu 702	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba	70,050,000
Kifungu 801	Afisi ya Msajili wa Haki Miliki	100,000,000
Jumla ya Fungu		**1,672,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 46 – TUME YA KUCHUNGUZA SHERIA

Kifungu 201	Idara ya Utawala	174,914,000
Jumla ya Fungu		**174,914,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 – MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 201	Utawala Unguja	300,000,000
Jumla ya Fungu		**300,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 – OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 201	Utawala Unguja	534,000,000
Jumla ya Fungu		**534,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
Kifungu 401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru katika mchango wangu nilizungumzia suala hili la mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria na nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mhe. Omari Yussuf Mzee, naungana nayo sina wasi wasi nayo. Naoma suala dogo tu aniridhishe ili tumalizie suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, orodha kwa mujibu wa maelezo yake suala hili litakuwa limetajwa katika ukurasa wa 661 unaozungumzia Afisi Rais Fedha na Uchumi, Mipango na Maendeleo, Voti 73000 inazungumzia programu ya ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar. Imetajwa kwa pamoja pale bilioni tano na milioniu mia tatu. Tulipokuwa tukitoa pendekezo hili tulikuwa tunasema kwa nini hapa moja wapo katika option hii tulitoa. Ile nia njema ya Waziri aliyoieleza hapa isionekane na kuainishwa kama ilivyoainishwa kwengine.

Ninachokusudia Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kitabu hiki hiki ukurasa wa 639 kwenye ujenzi Vot 750000. Pameorodheshwa miradi yote ya ujenzi kuanzia ukurasa ule mpaka 641 ambayo inasimamiwa kupitia Wizara ya Fedha na wizara nyengine. Jengo hili halikutajwa pale. Hapa ambapo pana mradi au programu ya ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar limewekwa kwa ujumla wake.

Nilikuwa nasema kwa sababu mwenyewe keshakiri kwamba hili ndio jengo la kwanza litakalopewa umuhimu na serikali. Anatuhakikishia kwamba katika kuchapishwa kwa kitabu kipya cha *estimate* katika *section* ile itatajwa hili fungu la Maendeleo la Wizara ya Katiba na Sheria lionekane linaendelea na shughuli zake kama ilivyokuwa linaruhususiwa naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria kutoa ufafanuzi juu ya maelezo yaliyotolewa na Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Mwenyekiti, nilingelifurahi sana kama ningekuwa na uhakika wa hilo ambalo analolizungumza ningelilisema. Lakini kama nilivyoeleza awali kwamba taasisi zetu nyingi zinakaa katika majengo mabovu. Nikianza kunukuu hapa, nikasema katika kitabu niweke jengo la Wizara ya Katiba na Sheria, halafu baadaye Wizara ya Mawasiliano wamekuja na michoro natakiwa kulipia. Tayari ki *audit* nnakwiri, wivu utakwenda kwa Wizara ya Katiba na Sheria hizo fedha ni za kwangu, umempaje Mawasiliano.

Ndio nilichosema kama Mhe. Mwakilishi akubali kwamba hii vote ni kwa ajili ya majengo ya Serikali. Jengo la Wizara ya Katiba na Sheria utaratibu ambao wao sasahivi wapo mbali zaidi katika kutekeleza yale majukumu ambayo tuliyoyatoa ukilinganisha na Wizara ya Mawasiliano, ukilinganisha na Wizara ya Mawasiliano, ukilinganisha na Wizara ya Utumishi, hata ukilinganisha na Wizara ya Ajira. Na wao katika jengo lao tunataka tuwaongezee ile ghorofa ya juu kule.

Ndio maana nikasema nachelea kuandika hivyo kwamb vote hii ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Katiba. Nataka Mhe. Mwakilishi na atuamini, jengo la kwanza tutakalojenga kutumia fedha hizi ni jengo la Wizara ya Katiba. Lakini tumesema tunataka tuanze na majengo mawili, jengo la Wizara ya Katiba na Jengo la Wizara ya Utumishi. Naamini kwa pesa hizi kwa majengo haya mawili hawataweza kumaliza. Bajeti ya Mwaka kesho tutamaliza majengo haya mawili ili mwaka kesho tuje na pesa kidogo kwa ajili ya majengo mengine mawili na mwaka wa keshokutwa tutamalizana nao.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka tu *roll over* tuende miaka miwili miwili tuweze kumaliza majengo. Namuomba Mhe. Mwakilishi akubali kwamba sisi hatutoandika lakini akubali kauli ya Waziri wa Fedha kwamba jengo la kwanza tutakalolianza ni jengo la Katiba na Sheria.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Zanzibar ni nyumbani kwa Kiswahili na tuna maneno mengi yaliyoakis, mwenendo wetu wa kisiasa kutoka makubaliana ya muafaka mpaka maridhiyano. Na mimi nataka kumuhakikishia Mhe. Waziri kwamba nimekubali, nimeafiki na nimeridhia. Tuendelee ahsante.

Kifungu 401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	140,000,000
Jumla ya Fungu		**140,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana, nakushukuru Mhe. Waziri, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kazi nzuri tumeifanya kwa kumalizia shughuli ya Wizara hii. Nakushukuruni kwa kunipa mashirikiano makubwa kuendesha kikao hiki.

Sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa 11:00 jioni wakati ambapo tutasikiliza hotuba ya Wizara ya Afya. Ahsante sana.

(Saa 6:45 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Afya

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante kabla sijaanza naomba niwaarifu Wajumbe kwamba mlipewa karatasi za nyongeza tunaomba radhi ilibidi tufanye masahihisho hayo, lakini masahihisho hayo yanajieleza wenyewe.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi kupokea, kujadili, kuchangia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa kazi za maendeleo na kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana kwa mara nyengine tukiwa na afya nzuri katika kikao cha bajeti cha Baraza lako tukufu. Hii ikiwa ni bajeti ya mwanzo tokea Serikali ya awamu ya saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa kuingia madarakani.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya, kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar katika uchaguzi uliofanyika mwezi wa Oktoba, 2010 na kuwa Rais wa mwanzo wa Zanzibar kuongoza Serikali yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Aidha, tunampongeza kwa umahiri wake wa kuongoza kwa hali ya amani yenye utulivu na maelewano katika kipindi chake kifupi tokea aingie madarakani. Mhe. Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongezee hekima katika uongozi wake. Vile vile, tunakupongeza wewe Mhe. Spika, pamoja na wajumbe wako wote wa Baraza hili tukufu kwa kuweza kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Mhe. Spika, mafanikio ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hayawezi kufikiwa pindipo nchi ikiwa haina amani na utulivu. Hatua mbali mbali zilizochukuliwa hadi kufikia uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa zimeleta faraja, mshikamano na matumaini makubwa kwa wananchi wa Zanzibar; jambo ambalo ni la msingi kuelekea upatikanaji wa maendeleo ya nchi yetu. Sina budi kuwashukuru wale wote walioanzisha na kuzifanikisha hatua zote zilizotufikisha kwenye umoja huu wa kitaifa kwa maslahi ya nchi yetu. Mhe. Spika, kila nilipopata nafasi nimekuwa nikisisitiza kwamba lile lenye faida kwa sote ndilo lenye faida kwa kila mmoja wetu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukurani, sasa naomba uniruhusu nitoe maelezo ya muundo, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya Wizara ya Afya kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012.

MUUNDO WA WIZARA YA AFYA

Mhe. Spika, ufanisi wa utekelezaji wa malengo na majukumu ya wizara pamoja na mambo mengine hutegemea muundo, uongozi na usimamizi mzuri wa wizara. Kutokana na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa wizara sasa ina idara zifuatazo:-

1. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti
2. Idara ya Utumishi na Uendeshaji
3. Idara ya Kinga na Elimu ya Afya
4. Idara ya Tiba
5. Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja
6. Idara ya Bohari Kuu ya Dawa
7. Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali
8. Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali
9. Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba

Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho 1.1.

Mhe. Spika, kabla sijaelezea utekelezaji wa kila idara, naomba nitoe mukhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, wizara iliidhinishiwa jumla ya Tsh.10,638,000,000 kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho, na Tsh. 1,020,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hata hivyo, kutokana na muundo mpya wa wizara baada ya uchaguzi mkuu, wizara iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 10,124,752,951 kwa kazi za kawaida, mishahara na maposho na Tsh. 800,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi April, 2011 jumla ya Tsh. 8,250,551,618 (81%) ziliingizwa. Kati ya hizo Tsh.7,364,120,793 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 886,430,825 kwa ajili ya kazi za kawaida (*other charges*). Vile vile wizara iliingiziwa jumla ya Tsh. 552,334,028 (69%) kwa kazi za maendeleo. Aidha, wizara ilipangiwa kuchangia kiasi cha Tsh. 12,891,000 katika mfuko mkuu wa serikali. Hadi kufikia Aprili, 2011 jumla ya Tsh. 26,655,600 (207%) ya makadirio zilikusanywa. Ufafanuzi wa mgao wa fedha kwa kila idara na zile za maendeleo pamoja na mapato unatolewa katika kiambatisho A, B na C.

IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ni moja kati ya idara zenye majukumu makubwa katika kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za afya. Pia inabeba majukumu ya kutayarisha mipango ya utekelezaji ya muda mfupi na ya muda mrefu, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo inapata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo, kusimamia kazi za utafiti zinazohusiana na afya ili kuhakikisha kwamba taarifa zinazopatikana katika tafiti hizo zinasaidia kutoa maamuzi yenye ushahidi wa kitaalamu (*Evidence based decisions*). Majukumu ya Idara hii yanafanikishwa kwa kupitia Divisheni ya Mipango na Bajeti, Divisheni ya Utafiti, Divisheni ya Ufuatiliaji na Tathmini, Divisheni ya Taarifa za Afya na Divisheni ya Sera na Sheria

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Idara ilifanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kutoa mafunzo kwa wakuu wote wa vitengo vilivyomo ndani ya wizara juu ya utayarishaji wa *MTEF* pamoja na uandaaji wa Mpango Kazi wa wizara.

b) Kushiriki katika kutayarisha mpango wa mwaka wa utekelezaji utoaji wa huduma juu ukatili wa aina zote (*Multi sectoral Annual Plan on Gender Based Violence*).

c) Kuratibu utekelezaji wa kazi zinazopata msaada kupitia mradi wa Umoja wa Mataifa unaojulikana kama *Joint Program support 5 (JP5).*

d) Kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, idara imeandaa mkutano wa pamoja na wakuu wa vitengo na miradi katika utayarishaji wa mpango wa miaka 3 (*UNDAP*) unaotarajiwa kuanza kutumika Julai 2011 hadi Juni 2013.

e) Kusimamia uanzishwaji wa Akaunti za Timu za Afya za Wilaya (*District Health Service Account*) ambayo itakuwa kama mfuko wa fedha wa wilaya (*Basket Fund).*

f) Imeratibu na kutoa ushauri wa kisheria katika mambo mbali mbali yanayohusu Wizara ya Afya pamoja na kusimamia kesi zinazoikabili wizara.

g) Imekamilisha rasimu za Miswada ya Sheria ya Afya ya Jamii (*Public Health Act),* na mswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(Chief Government Chemist Laboratory Agency Act).*

h) Imesimamia shughuli zote za takwimu pamoja na taarifa mbali mbali za afya kutoka katika Hospitali na Vituo vya

Afya na kutoa viashiria mbali mbali katika kupima utekelezaji wa Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) na Mpango Mkakati wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya (*Health Sector Reform Strategic Plan*).

i) Imeratibu taarifa zote za ufatiliaji na tathmmini ndani ya miradi na program za wizara ambazo hutekeleza malengo na mikakati ya sera

j) Imeweza kutayarisha rasimu ya mwanzo ya muongozo wa mfumo wa taarifa za afya (*HIS policy guideline*).

k) Imefanikiwa kuandaa kitabu cha taarifa za afya kwa mwaka 2009 (*Health Information Bulletin - HIB* 2009) na kusambazwa kwa wadau mbali mbali wa nje na ndani ya wizara.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 idara hii pamoja na mambo mengine ina malengo yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa muongozo wa mfumo wa kuchangia huduma za afya.

(b) Kufanya tathmini juu ya maeneo ya utafiti ndani ya sekta ya afya.

(c) Kuandika nyaraka za kutafutia misaada kwa wafadhili mbali mbali.

(d) Kuzipitia na kuzifanyia marekebisho Sheria ya Wauguzi na Wakunga (*Nurses and Midwives Act No.9 of 1986* na Sheria ya Hospitali binafsi (The Private Hospital regulations Act No. 4 of 1994.

(e) Kukamilisha kitabu cha taarifa za afya kwa mwaka 2010 (*HIB 2010*)

(f) Kuandaa Mpango Mkakati wa Taarifa za Afya.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo hayo, idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 131,000,000.00 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Tsh. 85,000,000.00 Idara ya Mipango Unguja na Tsh. 46,000,000.00 kwa Pemba.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo na majukumu ya Idara hii yanafanywa kupitia divisheni zifuatazo:-

a) Divisheni ya Nguvu Kazi

b) Divisheni ya Utawala

c) Mhasibu Mkuu wa Wizara
d) Kitengo cha Kumbukumbu na Masjala ya Siri.

Mhe. Spika, kwa pamoja divisheni hizi hutoa huduma kwa idara nyengine zote ili kuhakikisha kwamba kazi za kitaalam, tiba na kinga za Wizara ya Afya zinafanyika kwa ufanisi. Kwa pamoja divisheni hizi hutekeleza mikakati ya kupata wafanyakazi, kusimamia mafunzo ya nje na ndani ya wizara na utoaji wa huduma za utawala wa siku hadi siku. Aidha, shughuli nyingine zinazosimamiwa na idara hii ni pamoja na:-

a) Kusimamia masuala yote yanahusiana na ajira na kuwapangia kazi kulingana na fani walizonazo.
b) Kusimamia haki na maslahi ya wafanyakazi pamoja na kuhakikisha kuwa wastaafu na waliofariki wanakamilishiwa taratibu za kupata mafao yao kikamilifu.
c) Kusimamia na kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi wa wizara, ili kupata wataalamu wa fani zote za afya.
d) Kutunza na kutengeneza miundombinu yote ya wizara, kuanzia vituo vya afya vya msingi hadi Hospitali Kuu ya Rufaa pamoja na taasisi nyengine zote zilizo chini ya Wizara ya Afya.
e) Kusimamia ujenzi wa majengo mapya ya wizara yanayojengwa na serikali au Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 idara imeweza kutekeleza yafuatayo:-

a) Wafanyakazi wapya wa kudumu 132 wa fani mbali mbali wameajiriwa katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011. Angalia kiambatisho Nam. 3.1.

b) Kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi wafanyakazi 114 (wanaume 68 na wanawake 46), kiambatisho namba 3.2 kinafafanua zaidi.

c) Kutathmini wafanyakazi wa wizara ili kujua idadi halisi iliyopo, taaluma zao na sehemu wanazofanyia kazi na mahitaji ya mafunzo ya wafanyakazi wake. Matokeo ya tathmini hiyo yameonyesha kuwa wizara ina wafanyakazi 3,366 na kubaini upungufu wa wafanyakazi takriban kwa fani zote za afya. Tatizo la baadhi ya wafanyakazi

kutopangiwa katika maeneo husika kulingana na fani zao pia lilionekana.

d) Kuwalipia ada ya masomo jumla ya wanafunzi 16 waliokuwa wakisoma elimu masafa (*Distance Learning*) katika fani ya uuguzi.

e) Kuandaa mwongozo wa kufundishia wakuu wa Vituo vya Afya jinsi ya kuongoza vituo vyao.

f) Kutoa mafunzo kwa Maafisa wa Wilaya na Makatibu Muhtasi wa wizara namna ya kuingiza taarifa za nguvu kazi katika *"Human Resource Data Base".*

g) Kufanya matengenezo ya majengo, mitambo, mashine, umeme, na maji katika hospitali na vituo vyote vya afya pamoja na miradi yote ya maendeleo ya wizara.

h) Kusimamia ujenzi wa majengo mapya yaliyojengwa na wizara pamoja na yale yaliyojengwa na wadau mbali mbali.

i) Kusimamia ununuzi wa vifaa na zana mbali mbali zenye thamani ya jumla Tshs. 313,647,788.20 (jenereta la Hospital ya Mwembeladu, vifaa vya wodi ya wazazi ya Hospital ya Mnazi Mmoja, zana na vifaa kwa ajili ya kuboresha huduma za uchunguzi katika Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, kompyuta na mashine za fotokopia kwa ajili ya Programu ya Malaria.

j) Kusimamia ununuzi wa vifaa vya tiba, dawa za tiba ya magonjwa nyemelezi, kwa ajili ya programu ya UKIMWI vyenye thamani ya Tshs. 375,917,387.50

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/12 idara imejipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kuajiri vijana wapya wa fani mbali mbali wakiwemo wanaomaliza Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kulingana na mahitaji ya wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
b) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya kanuni na taratibu za kazi ili zieleweke kwa wafanyakazi wote.
c) Kuwapatia mafunzo ya utawala na uongozi wafanyakazi 80.
d) Kuwapatia nafasi za masomo wanafunzi wapya 20 wa kada tofauti.

e) Kuongeza vituo viwili vitakavyotoa elimu masafa kwa Unguja na Pemba .
f) Kuratibu uanzishwaji wa tiba kwa njia ya mawasiliano ya simu (*Telemedicine*) katika Hospitali za Mnazi Mmoja na Chake Chake.
g) Kutoa mafunzo kwa viongozi wa taasisi za afya juu ya utumiaji wa takwimu za nguvu kazi katika kufanya maamuzi ya utendaji.
h) Kuangalia miundombinu yote ya wizara ili kuhakikisha inafanya kazi ipasavyo na kwa wakati wote ili kuimarisha huduma za afya.
i) Kuandaa mpango wa manunuzi wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wakuu wa vitengo.
j) Kutoa elimu ya Sheria ya Ununuzi kwa wakuu wa vitengo pamoja na wafanyakazi.
k) Kusimamia taratibu na sheria za uondoaji wa mali za serikali katika hospitali pamoja na vitengo vilivyomo ndani ya wizara.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya mwaka 2011/12 idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 212,000,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Tsh. 142,500,000 Idara ya Uendeshaji na Utumishi Unguja na Tsh. 69,500,000 kwa Pemba. Pia naomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh. 8,627,000,000 kwa ajili ya mishahara na maposho ya Wizara ya Afya. Kati ya hizo Tsh. 6,200,406,000 kwa Unguja na Tsh. 2,426,594,000 kwa Pemba.

OFISI YA MDHAMINI WA AFYA PEMBA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunaahirisha shughuli zetu kwa muda mpaka umeme utakaporudi.

(Baraza liliahirishwa kwa muda kutokana na kukatika kwa umeme)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru hiyo yote ni dalili kwamba hatuna dhambi. Mhe. Spika, ofisi hii ndio msimamizi mkuu wa huduma za afya kisiwani Pemba. Mbali na usimamizi wa huduma za afya, shughuli zote za kiutawala zikiwemo mipango na utumishi nazo zinaratibiwa na ofisi hii. Taarifa zote za utekelezaji, malengo na matumizi chini ya ofisi hii zimeelezwa kupitia idara husika.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia na kufuatilia utoaji wa huduma bora za afya mijini na vijijini pamoja na kubuni mbinu za kukabiliana na maradhi mbalimbali yakiwemo ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Aidha, inajukumu la kusimamia na kutoa elimu ya afya kwa jamii kwa lengo la kujikinga na maradhi mbali mbali. Idara hii ina programu na vitengo vifuatavyo:-

Ofisi za Afya Kanda ya Unguja na Pemba

Mhe. Spika, Ofisi za Afya Kanda ya Unguja na Pemba ni ofisi zenye majukumu ya kusimamia utowaji wa huduma za afya, katika ngazi za wilaya na vijiji. Pia ni kiungo muhimu kati ya vitengo na taasisi nyengine za serikali na zisizo za serikali za ndani na nje zinazoshughulika na kazi za utoaji wa huduma za afya katika wilaya na vijiji. Aidha, Ofisi za Kanda zinasimamia na kuratibu kazi za Timu za Afya za Wilaya, hospitali za vijiji na vituo vya afya.

Mhe. Spika, kwa kushirikaiana na *ADB*, *DANIDA* pamoja na michango ya wananchi hali ya majengo ya vituo vingi vya afya pamoja na huduma zinazotolewa katika vituo hivyo zinaridhisha.

Mhe. Spika, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na maradhi ya kuhara na kutapika ikiwemo ya miripuko ambayo kwa kiasi kikubwa yanaathiri afya za wananchi wetu pamoja na uchumi kwa ujumla. Kuzuka kwa maradhi ya miripuko kunatokana na hali isiyoridhisha ya mazingira inayopelekea utumiaji wa maji yasiyo salama, utumiaji mdogo wa vyoo katika baadhi ya maeneo na utumiaji wa vyakula visivyohifadhiwa ipasavyo. Ofisi zetu za kanda zimefanikiwa kudhibiti maradhi ya kipindupindu na pia kutibu vizuri pale yalipotokea.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi za Afya Kanda zitaendelea kusimamia utendaji wa kazi katika Timu za Afya za Wilaya, hospitali za vijiji na vituo vya afya, upatikanaji wa vifaa na dawa na kushajihisha jamii katika kuimarisha huduma za afya.

Mhe. Spika, katika kufanikisha agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Idara ya Kinga kupitia ofisi hii inakamilisha tathmini na makisio ya kubadilisha na kumalizia vituo vya Mpendae na kile cha Kwamtipura ili viweze kumalizwa na kutoa huduma kamilifu katika daraja la pili (*PHCU+*). Kukamilika kwa matengenezo hayo kunatazamiwa kupunguza msongamano wa wagonjwa wa Wilaya ya Mjini kukimbilia kufuata huduma katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Kitengo cha Elimu ya Afya

Mhe. Spika, Kitengo cha Elimu ya Afya kina majukumu makubwa ya kuelimisha jamii kwa kutumia mbinu shirikishi ili kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Kitengo hiki ni kiungo kikuu katika kuunganisha kazi zote za kuelimisha jamii zinazohusiana na masuala ya afya. Ili kufanikisha kazi hiyo kitengo kimekuwa kikishirikiana na vitengo viliomo ndani na nje ya wizara.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kitengo kilifanya mikutano mbali mbali ambapo mada kuu zilihusu kinga dhidi ya maradhi yanayoonekana kuwaathiri wananchi. Aidha, radio na televisheni za serikali na za watu binafsi zilitumika kuelimisha jamii ambapo zaidi ya vipindi 24 vilirushwa hewani.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi na walimu katika skuli na Madrasa wanajikinga na maradhi, kitengo kimefanya ufuatiliaji, ukaguzi na kutoa elimu ya afya ya mazingira katika skuli 12.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Kitengo cha Elimu ya Afya kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa elimu ya afya kwa jamii kuhusiana na Kitabu cha Ukweli Kuhusu Maisha kwa lengo la kuimarisha afya ya mama na mtoto.
b) Kuandaa muongozo wa Sera ya Elimu ya Afya nchini.
c) Kuendelea kutoa ushirikiano wa kitaalamu kwa miradi, vitengo na wadau wote wanaotoa taaluma ya elimu ya afya katika jamii.

Kitengo cha Afya ya Mazingira

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya ya Mazingira kinafanya kazi za kuimarisha, kustawisha na kulinda Afya ya Jamii kutokana na mambo yahusianayo na mazingira kwa kutayarisha sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Vile vile hutoa taaluma, mbinu, mikakati na kushajihisha jamii kuchukua hatua za kuimarisha mazingira ili isiwe chanzo cha maradhi na majanga.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuhakikisha kuwa Wizara ya Afya inatumia sheria zinazoenda na wakati, kitengo kilifanya mkutano wa kuandaa rasimu ya kwanza ya Sheria ya Afya ya Jamii kwa kuwashirikisha na wadau kutoka taasisi mbali mbali zikiwemo Idara ya Mazingira, Mamlaka ya maji, Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu, Baraza la Manispaa, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*), Wizara ya Kilimo na Taasisi zisizo za kiserikali za Wanasheria.

Mhe. Spika, kitengo kilitoa mafunzo kwa mafundi waashi 110 juu ya ujenzi wa vyoo vya gharama nafuu katika wilaya za Unguja na Pemba ikiwa ni awamu ya pili yenye lengo la kukamilisha Shehia zilizobaki ambapo vyoo 19 vya aina ya sungura vilijengwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 kitengo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuikamilisha Sheria ya Afya ya Jamii.
b) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa ngazi ya Shehia juu ya mkakati wa mbinu shirikishi jamii ya maji na usafi wa mazingira kwa Mkoa wa Mjini Magharibi.
c) Kuandaa Miongozo ya Afya ya Jamii kwa wananchi.
d) Kuandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa miaka 5 wa Afya ya Mazingira.
e) Kuimarisha usimamiaji na ufuatiliaji wa miradi ya afya ya mazingira.

Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi kina jukumu la kutoa huduma za kufanya ukaguzi wa mazingira ya kazi, uchunguzi wa afya za wafanyakazi, kutoa ushauri nasaha na elimu ya afya kwa wafanyakazi wa serikali na sekta binafsi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 jumla ya maeneo 19 yalifanyiwa kazi hii ikiwa ni pamoja na Hoteli, Vilabu vya Pombe, Mikahawa na nyumba za kulala wageni pamoja na jengo la Chuo cha Kilimo cha Kizimbani ambalo linatarajiwa kufanywa Kiwanda cha kusindika mazao na cha vinywaji baridi.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 3,154 walichunguzwa afya zao kutoka katika taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za kiserikali pamoja na wafanyabiashara wa vyakula. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kwamba wafanyakazi 161 walionekana na matatizo mbali mbali kama inavyojionesha katika kiambatisho namba 5.1. Aidha, wale wote waliogundulika na matatizo walipelekwa kwa madaktari husika kwa kupatiwa matibabu na ushauri.

Mhe. Spika, wizara imeweza kufungua ofisi ya Afya ya Wafanyakazi Pemba baada ya kupata msaada kutoka Shirika la Maendeleo la Denmark. Aidha, kwa

mwaka wa fedha 2011/2012 kitengo kitaendelea na kazi zake za kawaida ikiwemo kuwajengea uwezo wafanyakazi wake.

Kitengo cha Afya Bandarini

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya Bandarini kina jukumu la kuzuia na kuchukua tahadhari juu ya uingizwaji wa maradhi ya kuambukiza kutoka nje ya Zanzibar. Ili kuhakikisha azma hiyo inafikiwa, kitengo hulazimika kufanya ukaguzi wa vyombo vinvyoingia kutoka nje ya Zanzibar na kusimamia ufukizaji na upulizaji wa dawa kwa ajili ya kuua wadudu wanaosambaza maradhi.

Aidha, kutoa ushauri na kusimamia usafi wa mazingira eneo la bandarini na Uwanja wa ndege na kutoa elimu ya afya sehemu za kazi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kitengo kiliweza kufanya ukaguzi wa vyombo 401 vya baharini na viwanja vya ndege pamoja na wafanyakazi wake. Mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi huo ni pamoja na wafanyakazi kutofanyiwa uchunguzi wa afya zao (*medical checkup*), kuwepo kwa wadudu mbali mbali (Mende na Panya), ukosefu wa vifaa vya usafi na uelewa mdogo wa elimu ya afya kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, jumla ya raia wa kigeni 186,832 waliopitia Uwanja wa ndege na 55,461 kupitia Bandarini wamekaguliwa ili kujua kama wamepatiwa kinga dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Manjano. Jumla ya abiria 1,393 walibainika kutokuwa na kadi zinazothibitisha kuwa walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa huo. Kati ya hao 63 walipatiwa chanjo hapa Zanzibar na wengine waliruhusiwa kutokana na kutoa vithibitisho vinavyowaruhusu kuto kuchanjwa.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2011 kitengo kiliwapatia chanjo wasafiri 988, kati yao 830 walipatiwa chanjo ya maradhi ya Homa ya Manjano na 158 walipatiwa chanjo ya Homa ya Uti wa Mgongo (*Meningitis*).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kitengo kimejipangia kufanikisha malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha kazi za ukaguzi bandarini pamoja na uwanja wa ndege.
b) Kushiriki katika mafunzo ya Kanuni mpya za Afya za Kimataifa *(International Health Regulation - IHR).*

Kitengo cha Mienendo na Udhibiti wa Maradhi (*Epidemiology*)

Mhe. Spika, kitengo hiki kina jukumu la kushughulikia mienendo ya maradhi na udhibiti wa magonjwa pamoja na kufanya uchunguzi na kutoa taaluma juu ya maradhi ya mripuko.

Mhe. Spika, kitengo kimeweza kutoa mafunzo ya uchunguzi wa magonjwa ya mripuko (*outbreak investigation*) kwa wafanyakazi wa vituo vya afya, mahospitalini na Timu za Afya za Wilaya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kufuatia mripuko wa maradhi ya Homa ya Manjano nchini Uganda mwanzoni mwa mwaka huu, kitengo kiliweka mikakati ya kuhakikisha kuwa ugonjwa huo hauingii katika nchi yetu. Mikakati hiyo ilijumuisha utoaji wa elimu kwa jamii kwa njia ya redio na televisheni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kitengo kitaendelea kufuatilia mienendo ya maradhi nchini na kuishauri wizara katika kuandaa sera, mikakati na miongozo ya kukabiliana na maradhi ya miripuko na yanayoibuka.

Kitengo cha Lishe

Mhe. Spika, kitengo hiki kina majukumu ya kuhakikisha na kusimamia ulishaji na ufuatiliaji wa maendeleo ya ukuaji wa mtoto. Kitengo kinafanya kazi zake kwa kushirikiana na vitengo vya Idara ya Kinga, Hospitali, Timu za Afya za Wilaya pamoja na taasisi nyingine zilizo nje ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kitengo kilifundisha wakufunzi 16 na wafanyakazi 273 wa vituo vya afya juu ya matibabu ya utapiamlo Unguja na Pemba. Mafunzo kama hayo yametolewa kwa wanafunzi wa Chuo cha Afya cha Mbweni, ambapo jumla ya wanafunzi 58 wa Kada ya Afisa Tabibu wamepatiwa mafunzo hayo. Katika ngazi ya jamii jumla ya wakufunzi wanaotokana na jamii 1,815 kutoka shehia zote za Pemba walishiriki na 2,610 kutoka shehia 174 za Unguja. Lengo la mafunzo hayo ni kupunguza na ikiwezekana kuondoa vifo vinavyochangiwa na matatizo yanayotokana na utapiamlo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kitengo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa mafunzo ya matibabu ya utapiamlo kwa wafanyakazi wa vituo vya afya Unguja na Pemba.
b) Kutoa mafunzo katika ngazi ya jamii juu ya utambuzi na ufuatiliaji wa watoto wenye matatizo ya utapiamlo mkali.
c) Kutoa mafunzo kwa watunza dawa wa wilaya katika uhifadhi wa chakula dawa (*Therapeutic Food*).

Programu ya Kupambana na Malaria

Mhe. Spika, Programu ya Kupambana na maradhi ya Malaria ina majukumu ya kuhakikisha kuwa wananchi wanajikinga na maambukizo ya malaria na kwa wale waliopata maradhi haya wanapata tiba sahihi. Msukumo zaidi umelengwa kwa wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano. Ili kufanikisha malengo haya njia na mikakati mbali mbali hutumika.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 katika kutoa tiba sahihi jumla ya wananchi 96,476 walichungunzwa kwa kutumia vipimo vya uchunguzi vya darubini na njia ya haraka ya kuchunguza malaria (*Rapid Diagnostic Test - RDT*), ambapo 485 (asilimia 0.5 ya waliochunguzwa) walibainika kuwa na vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa malaria, kati yao 78 walikuwa watoto chini ya miaka 5. Ufafanuzi zaidi unatolewa katika kiambatisho namba 5.2.

Mhe. Spika, katika mzunguko wa 6 wa upigaji dawa, jumla ya nyumba 67,571 (95.7%) za Pemba zilipigwa dawa kati ya nyumba 70,608 zilizokadiriwa. Kwa Wilaya nne za Unguja (Kati, Kusini, Kaskazini "A" na "B") jumla ya nyumba 53,891 (96.6%) zilipigwa dawa kati ya nyumba 55,796 zilizokadiriwa. Aidha, wilaya ya Mjini na Magharibi upigwaji dawa tayari umekamilika.

Mhe. Spika, mafunzo mbali mbali yanayohusiana na kujikinga na malaria, upigaji wa dawa, kukabiliana na miripuko ya maradhi katika jamii na mapitio ya vielelezo vya uhamasishaji jamii kuhusiana na kudhibiti malaria yalitolewa kwa wafanyakazi wa afya na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuwakinga na malaria wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano wizara iligawa vyandarua 34,375 bure katika shehia 17 za Wilaya ya mjini Unguja. Shehia hizo ni Malindi, Mkunazini, Shangani, Kiponda, Kwamtipura, Magomeni, Mwembe Makumbi, Mlandege, Vikokotoni, Kidongo Chekundu, Nyerere, Amani, Jang'ombe, Mchangani, Kwahani, Chumbuni, Muungano. Aidha, vyandarua 12,413 vilivyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (*UNICEF*) viligawiwa kwa kinamama katika wilaya sita za Unguja kwa kupitia vituo vya afya. Kwa upande wa Pemba zoezi la ugawaji litaendelea hivi karibuni. Ufafanuzi zaidi wa vyandarua vilivyogawiwa unaonekana katika kiambatisho namba 5.3

Mhe. Spika, suala la kufanya uhakiki wa vimelea ni muhimu katika kutoa ufafanuzi na maelekezo ya kiwango cha kuwepo kwa maradhi ya malaria. Ili kuweza kufanikisha azma hiyo, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 programu ilijiwekea lengo la kuongeza vituo 28 zaidi vinavyotumika kufanya uhakiki huo

ambapo jumla ya vituo 25 vimeongezwa, na kufanya jumla ya vituo 90 sasa kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Spika, uchunguzi wa vimelea vya ugonjwa kwa watu wasiougua (*active case detection*) pia hutumika kufuatilia juhudi za wizara katika kuondoa tatizo la malaria. Kazi hii inaendelea kwa vile vituo vinavyoripotiwa kuwa na wagonjwa wengi wa malaria. Vituo vya Tumbe, Shumba Vyamboni, Jendele, Cheju na Uzi viliripoti idadi kubwa ya kesi za malaria na hivyo uchunguzi wa damu ulifanywa kwa watu wote wa vijiji hivyo. sambamba ufuatiliaji wa mwenendo wa mbu (*entomological monitoring*) pia ulifanyika.

Mhe. Spika, pamoja na kazi za kawaida, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Programu ya Kupambana na Malaria imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza kugawa vyandarua katika Wilaya zilizobaki.
b) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi za NGOs katika kampeni za Maliza Malaria Zanzibar kwa kutumia siku za afya ya vijijni (*village Health day).*
c) Kuanzisha mradi wa upatikanaji wa dawa kwa bei nafuu katika hospitali na maduka ya dawa binafsi (*affordable medicine - AMFM*) ili kuokoa maisha ya mwanadamu.
d) Kuimarisha mfumo wa huduma za Afya ya msingi wilayani (*Strengthening District Health System*).
e) Kudhamini jumuiya za kitaalam katika kusimamia ubora wa viwango.

Programu ya Kichocho, Minyoo, Matende na Mabusha

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa maradhi ya Kichocho, Minyoo, Matende na Mabusha yanadhibitiwa na hatimae kuondoshwa kabisa; hii ikiwa ni pamoja na kukinga na kuzuia ulemavu utokanao na maradhi hayo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, jumla ya watu 2,025 walifanyiwa uchunguzi dhidi ya ugonjwa wa Kichocho. Kati ya hao 1,684 (83.2%) waligundulika na maradhi hayo (wanawake 264 na wanaume 1,420). Wagonjwa wote walipatiwa matibabu na kutakiwa kurudi tena baada ya miezi miwili. Aidha, Wagonjwa walipatiwa elimu ya afya ili kuepuka uwezekano wa kupata maambukizo mengine. Taarifa kamili za wagonjwa waliochunguzwa zinafafanuliwa katika kiambatisho namba 5.4

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na wizara ya elimu, zoezi la kufanya tathmini ya hali ya Kichocho na Minyoo lilifanywa katika skuli 48 (24 Unguja na 24

Pemba). Ripoti za awali zinaonyesha kuwa minyoo aina ya *Trichuris trichiura* ndiyo inayoongoza. Kutokana na matokeo hayo skuli zote za Unguja na Pemba zilipatiwa dawa za kupambana na maradhi ya Kichocho na Minyoo isipokuwa kwa skuli za Wilaya ya Kusini ambazo walipatiwa dawa za minyoo pekee. Uchunguzi uliofanyika umeonyesha kwamba tatizo la maradhi haya kwa wakaazi wa Wilaya ya Kusini ni chini ya asilimia moja (Prevalance 0.5).

Mhe. Spika, katika juhudi za kuhakikisha kwamba ugonjwa wa matende hauwaathiri wananchi wa Zanzibar, jumla ya watu 121 walifanyiwa uchunguzi katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 ambapo hakuna aliyebainika kuwa na vimelea vinavyosababisha maradhi hayo. Ni matumaini mazuri Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 programu imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kwa kushirikiana na Shirika la Kimarekani la SCORE (*Schistosomiasis Consortium for Operational Research and Evaluation*) itaanzisha mpango wa miaka mitano (5) wa kutokomeza kabisa ugonjwa wa Kichocho utakaojulikana kwa jina la **"***Zanzíbar Elimination of Schistosomiasis Transmisión* (*ZEST*)".

b) Kuendelea kufuatilia upatikanaji wa huduma ya upasuaji wa mabusha katika hospitali zote za wilaya na vijiji.

c) Kuendeleza shughuli za utafiti wa makonokono ambao ni walezi wa viini vya maradhi ya kichocho katika mito, madimbwi na maziwa.

Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Kifua Kikuu na Ukoma

Mhe. Spika, Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Kifua Kikuu na Ukoma ina wajibu wa kuchunguza, kutibu, kufuatilia wagonjwa walioacha matibabu na kutoa elimu ya afya kwa jamii namna ya kujikinga na maradhi hayo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Programu imeendelea na juhudi za kuwashirikisha wananchi katika matibabu ya Magonjwa ya Kifua Kikuu na Ukoma, ambapo mpango wa ulishaji dawa za kifua kikuu kwa jamii (*Community TB Care*) umeendelea. Mpango huu ambao unaonekana kupendwa na jamii umeonyesha mafanikio makubwa ambapo kwa sasa wagonjwa wengi wa kifua kikuu wanakula dawa zao wakiwa majumbani chini ya uangalizi wa familia. Takwimu zinaonyesha kwamba kati ya wagonjwa 314 waliogunduliwa katika kipindi hiki, wagonjwa 223 (71%) wanakula dawa majumbani chini ya uangalizi wa familia zao.

Mhe. Spika, katika juhudi za kupambana na ugonjwa wa Ukoma suala la uchunguzi wa wagonjwa wapya ni muhimu sana. Katika uchunguzi uliofanywa, jumla ya watu 110 walichunguzwa kwa upande wa Unguja, ambapo watu 5 waligundulika na ugonjwa huo. Kwa upande wa Pemba jumla ya watu 73 walichunguzwa ambapo hakuna mtu aliyebainika kuwa na vimelea vya maradhi hayo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 programu imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea na utoaji wa mafunzo kwa watendaji juu ya utoaji wa huduma za kifua kikuu, Kifua Kikuu na UKIMWI pamoja na Ukoma.
b) Kufanya mafunzo ya siku saba (7) kwa wahudumu 40 wa maabara kuhusu "*smear microscopy*" na "*External Quality Assuarance*".
c) Kufanya uchunguzi wa maambukizi ya virusi vinavyosababisha maradhi ya UKIMWI kwa wagonjwa wapya wa Kifua Kikuu.
d) Kusambaza dawa za Kifua Kikuu na Ukoma katika vituo vyote vinavyotoa huduma hizi.

Programu ya Kupambana na Maradhi ya Watoto na Magonjwa ya Kuharisha (IMCI)

Mhe. Spika, programu ya IMCI (*Integrated Management of Childhood Illnesses*) ina jukumu la kusimamia utoaji wa matibabu sahihi kwa watoto walio chini ya miaka mitano kama miongozo inavyoelekeza. Lengo kubwa la programu hii ni kupunguza vifo vinavyosababishwa na magonjwa yanayowakabili watoto walio chini ya miaka mitano. Maradhi haya ni pamoja na magonjwa ya malaria, homa ya mapafu, kuharisha, surua na utapiamlo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 programu imeweza kutoa mafunzo kwa watendaji 40 wa vituo mbali mbali vya Unguja na Pemba juu ya matumizi ya muongozo mpya wa *IMCI*.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 programu imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuchapisha mwongozo na nyenzo za kufundishia "*IMCI guideline and training materials*".
b) Kutoa mafunzo rejea kwa wale wote waliopata mafunzo ya awali ya ''*IMCI*.''

c) Kutoa mafunzo ya awali ya *IMCI* kwa wale wasiopata mafunzo hayo.
d) Kuupitia mwongozo wa huduma ya watoto wachanga (*New Born Care*) na kuchapisha.
e) Kutoa mafunzo ya huduma ya watoto wachanga kwa wafanyakazi wa vituo vya afya Unguja na Pemba.

Programu ya Huduma za Macho

Mhe. Spika, Programu ya Huduma za Macho Zanzibar (*Zanzibar Comprehansive Eye Care Service - ZCES*) ina majukumu ya utoaji wa huduma za macho kwa jamii. Lengo kubwa ni kupunguza na kutokomeza kabisa upofu unaoweza kuepukika pamoja na kutibu wagonjwa walioathirika. Programu inafanya shughuli zake kwa kushirikiana na shirika la "*Sight Saver International*" ya nchini Uingereza. Aidha, programu pia inashirikiana na jumuiya mbali mbali za kiserikali na zisizo za kiserikali katika utoaji wa huduma za macho.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 programu imeweza kuwahudumia wagonjwa 14,525 (wanaume 5,007 wanawake 3,740 na watoto 5,778) ambao walikuwa na matatizo mbali mbali. Wagonjwa 231 walifanyiwa upasuaji mkubwa na 353 upasuaji mdogo. Aidha, wagonjwa 2,830 walipatiwa miwani, 552 walibainika na ugonjwa wa presha ya macho (*glaucoma*) na wengine walipatiwa matibabu mbali mbali.

Mhe. Spika, programu kwa kushirikiana na wenzetu wa mji wa Cape Town - Afrika ya Kusini tuliweza kufanya utafiti wa ugonjwa wa vikope (*Rapid assessment for the Trachoma Survey*), katika wilaya ya Micheweni. Utafiti ulikusudia kubaini ukubwa wa tatizo na kujua sababu zinazopelekea kuwepo kwa tatizo hilo. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa ugonjwa huu uko juu ya kiwango kilichowekwa na *WHO* cha asilimia 10 kwa watoto na asilimia moja kwa watu wazima kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo. Mkitizama hiki kijadweli kinatisha kutokana na idadi hii ya maradhi.

Jadweli 1: **Matokeo ya utafiti wa ugonjwa wa vikope Wilaya ya Micheweni 2010**

Maelezo/Umri	**Watoto (mwaka 1 - 9)**	**Watu wazima (40 +)**
Idadi ya waliochunguzwa	50	50
Asilimia ya walioonekana na vimelea	32	14

Kiwango cha wastani (%) kinachokubaliwa na WHO	10	1

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Jumuiya isiyo ya Kiserikali (*Zanzibar Outreach Program - ZOP*) ilifanya ukaguzi wa afya ya macho kwa wanafunzi 334 ambapo watoto 284 walibainika na udhaifu wa uoni na 119 walipatiwa miwani.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 programu imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kunyanyua na kuendeleza viwango vya elimu kwa wafanyakazi katika fani ya macho kwa kuwapatia watendaji mafunzo ya ndani na nje.
b) Kuimarisha utoaji wa huduma za upimaji na utoaji miwani.
c) Kuimarisha utoaji huduma za macho kwa kununua na kuweka vifaa muhimu vinavyohitajika katika hospitali ya wete Pemba.
d) Kuendelea kutoa huduma za macho vijijini (*outreach screening and surgical visits*).
e) Kuendeleza na kuimarisha huduma za mradi wa macho kwa kuongeza nguvu zaidi huko Pemba (*Pemba eye care Initiatives*).

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya mwaka 2011/12 idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 212,590,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Tsh. 104,590,000 Idara ya Kinga na Elimu ya Afya Unguja na Tsh. 108,000,000 kwa Pemba.

Aidha, idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 86700000 kwa ajili ya uendeshaji Timu za Afya za Wilaya. Kati ya hizo Tsh. 45,100,000 kwa Unguja na Tsh. 41,600,000 kwa Pemba.

IDARA YA TIBA

Mhe. Spika, Idara ya Tiba ina jukumu la kusimamia hospitali 3 za wilaya na hospitali 4 za vijiji. Hospitali hizo ni Abdalla Mzee, Chake Chake na Wete pamoja na Kivunge, Makunduchi, Micheweni na Vitongoji.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 huduma za matibabu ya nje, huduma za kulaza wagonjwa na huduma za uchunguzi wa maradhi ziliendelea kutolewa katika hospitali hizo. Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje 185,371

yaliripotiwa katika hospitali hizo, wanaume (81,903) na wanawake 103,468. Aidha, jumla wagonjwa 12,793 walilazwa kati ya hao 316 (2.5%) walifariki dunia. Kiambatanisho namba 6.1 kinafafanua zaidi.

Mhe. Spika, katika kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kipindi cha 2010-2015, Wizara ya Afya imekusudia kuziimarisha hospitali ya Chake Chake kuwa hospitali ya rufaa kwa Pemba, hospitali za Abdalla Mzee na Wete kufikia kiwango cha hospitali za Mkoa sambamba na kuzifanya hospitali zote za vijiji (*Cottage*) kuwa hospitali za Wilaya.

Mhe. Spika, utekelezaji wa majukumu haya unategemea sana upatikanaji wa rasilimali ikiwemo fedha, wafanyakazi wenye sifa na vifaa bora na vya kisasa. Ni azma ya wizara kutekeleza malengo hayo kwa awamu kama vile itakavyoonekana katika malengo makuu ya Wizara ya Afya ya kila mwaka yatakayowasilishwa katika baraza lako hili tukufu. Kwa kuanzia wizara imeazimia kulitekeleza hili kupitia miradi mipya ya maendeleo ambayo imetengewa fedha kwa ajili ya kuimarisha hospitali hizi kufikia daraja nilizozitaja.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa watendaji katika hospitali za idara hii, Wizara ya Afya imewapeleka Pemba wafanyakazi 161 wa fani mbali mbali ili waweze kushirikiana na wenzao walioko huko katika kutoa huduma. Tunawaomba waheshimiwa viongozi wa huko hasa Wabunge na Wawakilishi, washirikiane na wizara katika kuwasaidia vijana hao kupata makazi bila kuwalipisha ili wasisumbuke katika usambazaji huo.

Mhe. Spika, uchambuzi wa takwimu za wagonjwa wanaohudumiwa katika hospitali hizi uliofanywa kwa mwaka 2009 unaonyesha kuwa maradhi kumi yaliyoongoza kwa kusababisha wagonjwa kulazwa ni kuharisha, shinikizo la damu, kuharibika kwa mimba, ngiri, kuvunjika, maradhi ya mapafu, maambukizo katika njia ya mkojo, upungufu wa damu, pumu na vidonda. Aidha, maradhi yaliyoongoza kusababisha vifo ni pamoja na homa ya mapafu, Maambukizo ya damu (*Septicaemia*), Upungufu mkubwa wa damu, kuharisha, shinikizo la damu na ajali.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi niruhusu nitoe mafanikio yaliyopatikana kwa kila hospitali na vitengo vilivyomo katika idara hii kwa kipindi cha mwaka wa bajeti uliomalizika.

Hospitali ya Chake-Chake

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 wizara iliweza kufanya matengenezo ya vyumba vya maabara, chumba cha *X-ray* na jengo la macho. Sambamba na matengenezo hayo hospitali pia ilipatiwa vifaa mbali mbali zikiwemo mashine mpya na za kisasa za uchunguzi wa macho na gari ya kubebea wagonjwa. Aidha, tatizo la upungufu wa maji hospitalini hapo limeondolewa. Upatikanaji wa vifaa na zana hizo sambamba na kuwepo daktari bingwa mzalendo na wale kutoka Jamhuri ya Cuba imesaidia sana kuongeza ufanisi kwa hospitali hiyo.

Mhe. Spika, kwa sasa hospitali hii ina jumla ya wafanyakazi 160 wakati mahitaji halisi ni wafanyakazi 262. Upungufu mkubwa unaonekana katika taaluma za afya hasa wauguzi na madaktari. Wauguzi waliopo ni 38 wakati mahitaji halisi ni 78. Kwa upande wa madaktari na madaktari wa meno waliopo ni 11 wakati mahitaji halisi ni 21.

Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Spika, Hospitali ya Abdalla Mzee ni hospitali ambayo inawahudumia wananchi wa Wilaya ya Mkoani na kwa mashirikiano na Jamhuri ya Watu wa China hospitali hii imekua ikipokea madaktari bingwa saba wa fani mbali mbali, ambao hubadilishana kwa kila kipindi cha miaka miwili. Aidha, madaktari hao huwa wanakuja na msaada wa dawa na vifaa mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Afya kupitia msaada wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, imezifanyia matengenezo makubwa nyumba zote wanazoishi madaktari wa kichina, pamoja na kuziwekea vifaa vya kisasa na umeme wa jua (*Solar Panel*). Utengenezaji huo sasa umeziweka nyumba hizo katika mazingira mazuri yanayopelekea madaktari hao kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Sina budi kupitia Baraza hili kuwashukuru ndugu zetu hawa wa Jamhuri ya Watu wa China ambao wamekuwa ni marafiki wa kudumu kwa misaada yao mikubwa kwa wananchi wa Zanzibar na hasa kule katika hospitali ya Abdalla Mzee.
Mhe. Spika, kwa nia ya kuimarisha utoaji wa huduma, serikali imeipatia hospitali hii vifaa vipya na vya kisasa vya meno. Upatikanaji wa vifaa hivi umesaidia sana kuimarisha huduma hizi ambapo kwa sasa wagojwa wanaweza kupata huduma zote za msingi za meno katika hospitali hiyo. Sambamba na hilo wizara imefanya matengenezo ya chumba cha upasuaji, wodi ya wazazi na chumba cha maabara.

Mhe. Spika, idadi ya wafanyakazi waliopo katika hospital hii ni 129 wakati mahitaji halisi ni 258. Upungufu mkubwa unaonekana katika wataalamu wa fani za afya ambapo kwa sasa wapo 64 tu, wakati mahitaji halisi ni 125, hivyo kuna upungufu wa watalaamu 61. Wizara imeliona tatizo hili na kwamba juhudi za makusudi zimeanza kuchukuliwa ili kupunguza tatizo hili.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi kuwa wizara ina nia ya kuimarisha hospitali hii na hatimae kuipandisha daraja kuwa hospitali ya Mkoa. Ninapenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa wizara imeanza kuchukua hatua za awali za kuandika mradi pamoja na gharama zinazohitajika za kuipandisha daraja hospitali hiyo. Aidha, mazungumzo ya awali na Jamhuri ya Watu wa China yamefanywa ambapo kimsingi wamekubali kugharamia matengenezo makubwa ya hospitali hiyo. Matengenezo hayo yatahusisha ujenzi mpya wa wodi ya wazazi, wodi ya watoto na matengenezo makubwa ya majengo yaliyopo.

Hospitali ya Wete

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Afya imempeleka daktari bingwa mzalendo wa maradhi ya wanawake kufanya kazi katika hospitali hiyo. Daktari huyo mbali na kutoa huduma katika hospitali hiyo pia amekuwa akiwafuata wagonjwa katika hospitali nyengine na katika vituo vya afya kwa ajili ya kutoa huduma kwa kinamama wenye matatizo ya afya ya uzazi.

Mhe. Spika, hatua nyengine zilizochukuliwa na wizara ni kuipatia hospitali hiyo X-ray mashine mpya na ya kisasa pamoja na vifaa na zana za kutolea huduma ya meno. Vile vile matengenezo madogo madogo katika chumba cha upasuaji, chumba cha *ultra sound*, jengo la kitengo cha macho, wodi ya wazazi na wodi ya watoto yalifanywa. Pia tatizo la uhaba wa maji hospitalini hapo limepatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, Hospital ya Wete nayo inakabiliwa na tatizo la upungufu wa wafanyakazi, kwani hospitali hii ina jumla ya wafanyakazi 164 sawa na asilimia 57 ya mahitaji halisi ya wafanyakazi. Kama zilivyo hospitali nyenginezo pengo kubwa liko katika wataalamu wa fani za afya ambapo kwa upande hospital hii wataalamu wa afya waliopo ni 99 ambao ni sawa na asilimia 66 ya mahitaji halisi.

Mhe. Spika, hospitali hii ni kongwe na majengo yake yanahitaji matengenezo makubwa, wizara inaendelea kutafuta misaada ili kuifanyia marekebisho makubwa nayo iwe na hadhi ya hospitali ya Mkoa.

Hospitali za Vijiji (*COTTAGE HOSPITALS*)

Mhe. Spika, kama nilivyoleza katika utangulizi Wizara ya Afya ina azma ya kuzipandisha daraja hospital zote za vijiji kuwa hospital za wilaya kwa mintaarafu ya kuimarisha na kuwasogezea wananchi huduma na hatimae kupunguza msongomano usio wa lazima wa wagonjwa katika hospital kuu ya Mnazi Mmoja pamoja na zile za wilaya.

Mhe. Spika, hali ya sasa ya wafanyakazi katika hospital hizi bado sio nzuri kwani kuna wafanyakazi 233 ambao ni sawa na asilimia 70 ya idadi halisi inayohitajika. Bila shaka idadi ya wafanyakazi watakaohitajika itaongezeka kwa kila hatua itayochukuliwa na Wizara kuzipandisha daraja hospitali hizi. Hivyo ni dhahiri juhudi za pekee zinahitajika katika kukabiliana na changamoto hii.

Hospitali ya Makunduchi

Mhe. Spika, hospitali ya Makunduchi ni hospitali ambayo hupokea wagonjwa kutoka maeneo tofauti ya Wilaya ya Kusini na uendeshaji wake unasaidiwa sana na shirika lisilo la kiserikali la *Health Improvement Project Zanzibar* (*HIPZ*). Shirika hilo limekuwa likitoa msaada wa vifaa, dawa, motisha kwa wafanyakazi na kuleta madaktari kila muda ambao hutoa huduma za matibabu, ikiwemo kufanya upasuaji. Ninapenda kuchukuwa fursa hii kulipongeza shirika hilo kwa maamuzi yake sahihi ya kushirikiana bega kwa bega na Wizara ya Afya katika kuwapatia huduma bora wananchi wa Wilaya ya Kusini na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 hospitali imepokea msaada wa mashine ya nusu kaputi (*Anaesthetic Mashine*) ambayo inasaidia kufanikisha huduma za upasuaji. Pia hospitali ilipatiwa msaada wa kitanda cha kuzalishia, vitanda vya kulaza wagonjwa na magodoro yake. Kazi nyengine muhimu zilizofanyika ni kuzifanyia matengenezo wodi ya wazazi, jiko na wodi ya wanaume.

Mhe. Spika, sambamba na huduma za upasuaji zilizoanza katika hospitali hii, pia huduma za damu salama, *ultra sound* na huduma maalum ya gari la wagonjwa kwa ajili ya wazazi zinapatikana. Taarifa za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki zinaonyeshwa katika kiambatisho namba 6.1

Mhe. Spika, huduma ya kuwafuata mama wajawazito majumbani ili kujifungulia katika hospitali imepelekea kuongezeka kwa kinamama

kujifungua katika hospitali hii kutoka wastani wa kinamama 20 kwa mwezi hadi kufikia 55 kwa mwezi. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni mama mmoja aliefariki kwa matatizo ya uzazi, kifo hicho kilisababishwa kwa kuchelewa kufikishwa hospitalini. Nia ya wizara hii ni kuzifanya hospitali za Kivunge, Vitongoji na Micheweni zifikie kiwango hiki.

Hospitali ya Kivunge

Mhe. Spika, Hospitali ya Kivunge ni hospitali pekee katika Mkoa wa Kaskazini Unguja; hupokea wagonjwa wote wanaopata rufaa katika vituo mbali mbali vya afya vilivyomo katika Mkoa huo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 wizara iliazimia kuimarisha huduma za dharura kwa wagonjwa ambapo sehemu maalum kwa ajili huduma hizo imetengwa. Wafanyakazi 20 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya jinsi ya kuwahudumia wagonjwa hao. Huduma hizi zinategemewa kuanza rasmi katika mwaka huu wa fedha. Taarifa za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki zinapatikana katika kiambatisho namba 6.1

Hospitali ya Micheweni

Mhe. Spika, hospitalli hii ni kiungo muhimu katika Wilaya ya Micheweni. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 hospitali imefanikiwa kupata vitanda na magodoro ambavyo vinatumika katika wodi mpya ya wazazi iliyojengwa kwa msaada wa *ZAYADESA*. Aidha, nyumba moja ya daktari imefanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 11 wapya wa kada tofauti wamepelekwa katika hospitali hii ya Micheweni; Maafisa Tabibu (2), Wafanyakazi wa maabara (4), Muuguzi afya ya akili (1), Wauguzi wakunga (2) na Wafanyakazi wa madawa (2). Ni matumaini ya wizara kwamba, ongezeko hili la wafanyakazi litasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali ya Micheweni. Taarifa za mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki zinapatikana katika kiambatisho namba 6.1

Hospitali ya Vitongoji

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, wizara imefanikiwa kuifanyia matengenezo madogo hospitali hiyo, ikiwemo kupaka rangi katika sehemu ya wagonjwa wa nje, kubadilisha mabomba ya maji safi, kutengeneza gari la kubebea wagonjwa na matengenezo katika mfumo wa maji machafu. Taarifa za

mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki zinapatikana katika kiambatisho namba 6.1

Huduma za Uzazi katika Hospitali za Idara ya Tiba

Mhe. Spika, akinamama kujifungulia katika hospitali ni moja kati ya mikakati ya kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi. Hivyo wizara imeendelea kutoa huduma za kujifungua katika hospitali zote za wilaya na zile za vijiji (*Cottage Hospitals*). Kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 jumla ya wajawazito 7,356 walilazwa katika hospitali hizo. Kati ya hao wajawazito 5,447 walijifungua kwa njia ya kawaida na 310 (5.4%) walijifungua kwa njia ya upasuaji. Kinamama 20 (0.3%) walifariki dunia kwa sababu mbali mbali. Kiambatisho namba 6.2 kinafafanua zaidi**.**

Huduma Katika Kliniki Maalum

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wake baadhi ya magonjwa yamewekewa kliniki maaalum ili kuyapa msukumo na kuweza kuyashughulikia ipasavyo. Maradhi hayo ni pamoja na kisukari, sindikizo la damu, pua, masikio na koo, kifua kikuu, viungo, maradhi ya uasharati, ngozi, magonjwa ya kike na macho.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 jumla ya wagonjwa 48,622 walipatiwa huduma katika klinininiki hizi zilioko katika hospital hizi. Wagonjwa waliohudumiwa katika kliniki ya matibabu ya macho waliongoza na kufuatiwa na wale wa kliniki ya matibabu ya meno na matibabu ya masikio, koo na pua. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Kiambatisho namba 6.3

Usafirishaji wa Wagonjwa Nje ya Nchi

Mhe. Spika, miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili Wizara ya Afya ni ongezeko la wagojwa wanaohitaji kusafirishwa nje ya nchi. Licha ya kuimarika baadhi ya huduma katika hospitali zetu bado wagonjwa wanaoshindikana nchini ni wengi.

Mhe. Spika, Wizara hulazimika kuwaombea fedha nyingi na za kigeni ili kuwapeleka wagonjwa hao nje ya nchi hususan wale wenye maradhi ya moyo, figo na saratani. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 wagonjwa waliopelekwa kwa matibabu nje ya nchi ni 60. Hali ya uchumi wa nchi yetu umewafanya wengi wa wagonjwa kukwama na wengine kupoteza maisha. Wakati nasoma hotuba hii kuna wagonjwa wasiopungua 190 ambao wanasubiri fedha kupelekwa matibabuni nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mkakati ambao wizara yangu inauchukuwa na kuamini kuwa ndio ufumbuzi wa suala hili ni kuimarisha hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Kama nitakavyo eleza katika maelezo ya hospitali hiyo mpango maalum umetayarishwa wa kuhakisha kuwa hospitali hiyo inakuwa na madaktari bingwa na vifaa vinavyo hitajika ili kuweza kutoa huduma ambazo hapo kabla ililazimika wagojwa kuzifuata nje ya nchi**.**

Mhe. Spika, Idara hii mbali ya jukumu la kushughulikia utoaji wa huduma katika hospitali hizo pia ina wajibu wa kusimamia uendeshaji wa kitengo cha Maradhi yasioambukiza na Mpango wa damu Salama hapa Zanzibar.

Mpango wa Damu Salama

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Damu Salama ina jukumu la kukusanya damu, kuichunguza na kuigawa katika hospitali na hatimae kwa wagonjwa watakaohitaji damu hiyo. Lengo la kuwepo mpango huu ni kuhakikisha upatikanaji wa damu salama na ya kutosha kutoka kwa wachangiaji wa hiari, ambayo itapatikana kwa urahisi mara tu inapohitajika. Mpango huu pia una nia ya kupunguza na ikiwezekana kuondosha kabisa ukusanyaji damu **kwa lazima** kutoka kwa ndugu na jamaa wa mgonjwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Mpango wa Damu Salama ulijipangia kukusanya, kuzichunguza, kuzihifadhi na kuzisambaza katika hospitali mbali mbali za Unguja na Pemba jumla ya unit 6,000 za damu kutoka kwa wachangiaji wa hiari. Hadi kufikia Machi 2011, jumla ya unit 4,730 (79%) zilikusanywa na kuchunguzwa, kati ya hizo unit 4,141 zimeshagawiwa katika hospitali zinazohusika na kutumika kwa wagonjwa waliohitaji.

Mhe. Spika, mafanikio haya yamepatikana kutokana na juhudi mbali mbali zilizochukuliwa na wafanyakazi wa mpango huu ikiwemo kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari katika skuli, vyuo, mikusanyiko ya kidini, katika vyombo vya habari, vilabu vya mipira na sanaa na vikosi vya ulinzi. Aidha, uhamasishaji wa uundaji wa "*donor club"* uliendelea na vilabu 4 vipya viliundwa hivyo kufanya idadi ya vilabu vyote kufikia 44.

Mhe. Spika, lengo jengine la Mpango wa Damu Salama kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ilikuwa ni kuongeza matumizi ya sehemu ya damu *(blood components)* badala ya kutegemea damu yote kwa ukamilifu. Ili kufanikisha azma hiyo mpango huu kwa kushirikiana na madaktari kutoka Benki ya Damu *(Blood Bank)* ya Norway iliweza kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 70 kutoka katika hospitali zote za Unguja na Pemba. Mafunzo

hayo yalihusu utumiaji mzuri wa damu na "components" na jinsi ya kuchukua hatua iwapo kutajitokeza matatizo yanayoambatana na tiba ya damu.

Mhe. Spika, huduma za Benki ya Damu katika kisiwa cha Pemba ziliimarika sana baada ya kupelekwa gari na vifaa vya kukusanyia na kuhifadhia damu katika kituo chake kiliopo katika hospitali ya Wete. Usambazaji wa damu katika hospitali nyenginezo zilioko Pemba kwa kila ilipohitajika ulifanyika bila ya matatizo yeyote.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mpango wa Damu Salama umejipangia malengo yafuatayo:-

a) Kuhamasisha zaidi jamii na kukusanya damu unit 6,500 kwa mwaka.

b) Kuendeleza Kamati ya Damu Salama ya Taifa ili kusimamia utumiaji mzuri wa damu na *"Components".*

c) Kuimarisha uchangiaji damu kwa hiari na huduma za Damu Salama katika Kanda ya Pemba.

d) Kuziimarisha klabu za wachangiaji damu *"Donor Clubs"*

e) Kuondosha kabisa uchangishaji damu wa lazima kutoka kwa ndugu wa mgonjwa "*Replacement Donations".*

Kitengo cha Maradhi Yasioambukiza

Mhe. Spika, suala la maradhi yasiyoambukiza ni la kimataifa na Mkutano wa Afya wa Dunia uliofanyika mwezi Mei 2011 huko Geneva umejadili kwa urefu na kuweka azimio litakalofikishwa kwenye Umoja wa Mataifa. Moja kati ya mazingira ya kutisha yanayoikabili hali ya sekta ya Afya ni kuongezeka kwa kasi kubwa kwa maradhi ya kisukari, saratani, moyo na maradhi ya kibofu cha mkojo.

Mhe. Spika, ukubwa halisi wa tatizo hili kwa hapa Zanzibar bado haujajulikana kwani wananchi wengi hatujakuwa na tabia ya kuchunguza afya zetu kabla hatujaugua. Wizara ya Afya imeandaa utafiti ulioanza tokea mwezi wa Juni 2011 na unatarajiwa kumalizika Julai 2011 wenye nia ya kutafuta ukubwa wa tatizo hilo pia sababu zinazopelekea wananchi kupatwa na maradhi hayo. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia sana katika kuandaa mikakati ya kupambana na maradhi haya thakili.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Afya imeendelea kutoa elimu ya afya kwa wananchi kama moja ya mikakati madhubuti ya kupambana na maradhi haya. Vipindi mbali mbali vilitolewa katika redio na televisheni, pia kutoa elimu katika makundi tofauti ya jamii ikiwemo walimu, wanafunzi, masheha, viongozi wa dini na katika vikundi vya mazoezi.

Matokeo ya juhudi hizi yameanza kuonekana kwani wizara imebaini kuongezeka kwa kasi kwa vikundi vya hiari vya mazoezi. Jambo hili linatia faraja ya kuwa elimu na ushauri inayotolewa na wataalamu wetu wa afya inaeleweka.

Mhe. Spika katika kipindi cha bajeti cha mwaka 2011/2012, kitengo kimejipangia malengo yafuatayo:-

a) Kukamilisha kufanya utafiti wa maradhi yasioambukiza.

b) Kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na maradhi yasioambukiza.

c) Kuendelea kuwaelimisha wafanyakazi wa afya jinsi ya kugundua maradhi na kutowa matibabu.

d) Kuendelea kutoa elimu ya afya pamoja na kuwafanyia uchunguzi wafanyakazi wa taasisi mbali mbali.

e) Kuwaelimisha waganga wa jadi kuweza kuwashauri wagonjwa wafike hospitalini mapema badala ya kujenga itikadi potofu.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya mwaka 2011/12 idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 351,949,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Tsh. 122,035,000 Idara ya Tiba Unguja na Tsh. 229,914,000 kwa Pemba.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inajumuisha hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya wazazi ya Mwembeladu na Hospitali ya wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali kuu ya rufaa kwa Zanzibar. Mbali na huduma za rufaa hospitali hii pia inatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa nje pamoja na huduma nyengine za uchunguzi

kama vile *X-ray, ultra sound, CT scan* na kutoa huduma nyenginezo kupitia kliniki za maradhi maalum. Huduma nyengine ni zile za kupeleka wataalamu wa matibabu vijijini na katika baadhi ya vituo vya afya *(out-reach services).* Aidha, hospitali hii hutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar na Chuo cha Madaktari wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba katika hatua za kuifanya hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa, wizara imepokea madaktari 13 waliohitimu kutoka vyuo mbali mbali nje ya Zanzibar kwa mafunzo ya vitendo *(Internship).* Tumelifanya hili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi 2011 jumla ya wagonjwa 41,240 walilazwa, kati yao wanawake 28,056 na wanaume 13,184. Wagonjwa 637 (1.5% ya wagonjwa wote waliolazwa) walifariki dunia. Jumla ya wagonjwa 97,206 walipatiwa huduma za matibabu ya nje. Kiambatisho namba 7.1 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 hospitali iliendelea kutoa huduma za uzazi ambapo jumla ya wajawazito 7,564 walilazwa kati ya hao 5,593 walijifungua kwa njia ya kawaida na 1,322 (19.1%) ya wajawazito wote waliojifungua walifanyiwa upasuaji.

Mhe. Spika, idadi hii ni kubwa sana hivyo, wizara yangu inajiandaa kufanya uchunguzi wa sababu zinazopelekea kiwango kikubwa cha upasuaji. Aidha, kinamama 29 (0.4%) walifariki dunia. Ufafanuzi zaidi unatolewa kiambatisho namba 7.2.

Mhe. Spika, huduma katika kliniki maalum mbali mbali ziliendelea kama kawaida na wagonjwa 65,568 walipatiwa huduma katika kliniki hizo. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatisho namba 7.3.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza hili kwamba huduma za maabara zimeimarika kwa kiasi kikubwa. Kwa sasa Maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina uwezo wa kupima aina ya vipimo 67 ukilinganisha na aina ya vipimo 30 katika kipindi cha mwaka uliopita. Hii imewapunguzia wananchi usumbufu wa kwenda Dar es Salaam kwa kufanya vipimo. Vile vile daktari bingwa mzalendo wa shughuli za maabara *(Pathologist)* amerejea nchini baada ya kumaliza masomo na tayari ameshaanza kazi. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeweza kununua mashine ya kupimia moyo na pia kupata daktari bingwa wa maradhi ya moyo.

Mhe. Spika, moja kati ya maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ni kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa. Mtaalam aliyesaidia kutayarisha mpango mkakati wa miaka 5 ya Hospitali ya Mnazi Mmoja amekamilisha ripoti ya awali iliyolenga kuifanya hospitali hii kuwa ya rufaa.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kushirikiana na Agakhan Hospital ya Dar es Saalam, iliendesha uchunguzi wa saratani ya matiti. Katika zoezi hilo jumla ya wanawake 713 walichunguzwa kati ya hao wanawake watatu walithibitika kuwa na matatizo hayo, hivyo walipatiwa matibabu. Mbali na uchunguzi, elimu kuhusiana na saratani ya matiti ilitolewa na kuwataka kinamama kufanya uchunguzi wa afya zao mapema iwezekanavyo pindi tu wanapoona dalili ambazo si za kawaida.

Mhe. Spika, Madaktari kutoka Valencia – Spain kwa kushirikiana na madaktari wetu wanaendelea kuja kufanya uchunguzi pamoja na kutoa matibabu ya upasuaji wa kichwa na mgongo *(Neuro Surgery)* kila baada ya miezi miwili. Takwimu zinaonyesha kwamba jumla ya wagonjwa 497 walifanyiwa uchunguzi ambapo jumla ya wagonjwa 69 walifanyiwa upasuaji wa kichwa na mgongo. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na wagonjwa 35 waliofanyiwa upasuaji huo kwa mwaka uliopita 2009/2010. Ujio wa madaktari hao umeokoa Tshs. 345,000,000 ambazo zingehitajika kupeleka wagonjwa hao kwa matibabu nje ya nchi.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kushirikiana na *Zanzibar Outreach Program (ZOP)* inaendelea kusogeza huduma karibu na wananchi hususan vijijini ili kuweza kuwafikia wananchi walio wengi. Jumla ya wagonjwa 3,428 katika vijiji mbali mbali walichunguzwa afya zao, miongoni mwao wagonjwa 2,026 walibainika kuwa na matatizo ya macho, wagonjwa 878 matatizo ya masikio, wagonjwa 77 waligundulika kuwa na maradhi ya kisukari, wagonjwa 328 walibainika kuwa na shinikizo la damu na 295 walionekana kuwa na matatizo mengine mbali mbali. Aidha, wananchi waliogundulika kuwa na matatizo walipatiwa huduma za matibabu.

Mhe. Spika, Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana mkataba na Serikali ya Uholanzi kuifanyia ukarabati pamoja na upanuzi hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia mradi maalum wa maendeleo *(ORIO PROJECT).* Mradi huu utahusisha ukarabati wa kiwanda cha zamani cha dawa ili iwe ni sehemu itakayoweza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje *(outpatient),* wodi ya wazazi, wodi ya watoto na wagonjwa wa dharura *(accident and emergency)* hivyo basi kupunguza msongamano ndani ya hospitali kuu ya Mnazi Mmoja. Mradi huo utagharimu jumla ya Tsh.

21,056,568,985/= ambapo serikali itachangia asilimia 50 ya gharama hiyo, na utekelezaji wake unategemewa kuanza rasmi katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kupitia Hospitali ya Mnazi mmoja pia imetiliana mkataba na *Haukeland University Hospital* kwa lengo la kubadilishana wataalamu wa taasisi hizo, hivyo wataalamu wetu watapata fursa ya kwenda kujifunza nchini Norway. Utekelezaji wa mradi huu unategemewa kuanza rasmi mwezi wa Septemba mwaka huu ambapo wataalamu wetu watatu watakwenda nchini Norway kupata mafunzo na kufanya kazi kwa miezi sita. Pamoja na kubadilishana huko kwa madaktari Hospitali ya Norway inakusudia kujenga jengo la makaazi hapo Mbweni ili madaktari hao wanapokuja wapate sehemu ya makaazi. Jengo hilo pia litatumiwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja pale ambapo madaktari hao watakuwa hawapo nchini.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inatambua umuhimu wa kuwepo kwa lifti zenye kufanya kazi hospitalini hapo, hivyo katika kuhakikisha huduma hiyo inapatikana bila ya usumbufu wowote, lifti mpya imenunuliwa na tayari inafanya kazi na matengenezo ya lifti nyengine yanaendelea.

Hospitali ya Wazazi Mwembeladu

Mhe. Spika, Hospitali ya Mwembeladu inahusika na utoaji wa huduma za uzazi na inasaidia sana katika kupunguza mrundikano wa wajawazito wanaohitaji huduma za kujifungua katika Hospital ya Mnazi Mmoja. Aidha, hospitali hii husaidia kinamama wanaohitaji huduma za uzazi kutoka vitongoji mbali mbali vya mji wa Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai 2010 mpaka Machi, 2011 jumla ya wajawazito 3,543 walilazwa, kati ya hao 3,240 walijifungua kwa njia ya kawaida na wale waliohitaji huduma za upasuaji walipelekwa Hospital ya Mnazi Mmoja. Ufafanuzi zaidi unatolewa katika kiambatisho namba 7.2

Mhe. Spika, Matengenezo makubwa katika chumba cha upasuaji na maabara yameweza kuendelea. Napenda kuliarifu baraza lako tukufu pamoja na wananchi wote kwa ujumla kwamba huduma za upasuaji kwa wajawazito wanaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida zimeanza kuanzia mwezi wa Aprili ambapo hadi kufikia mwezi wa Juni 2011 wajawazito 28 walipatiwa huduma hii. Ni imani yangu kwamba huduma hizi zitaweza kupunguza msongomano katika hospitali ya Mnazi Mmoja na kuondosha usumbufu kwa kinamama wanaohitaji kupatiwa huduma hii.

Hospitali ya Wagonjwa wa Akili – Kidongo Chekundu

Mhe. Spika, Hospitali ya Kidongo Chekundu ndio hospitali kuu ya rufaa kwa magonjwa ya akili na magonjwa mengine yanayohusiana na ubongo hapa Zanzibar. Huduma nyengine zinazotolewa ni zile za kutoa matibabu kwa waathirika wa madawa wa kulevya.

Mhe. Spika, jumla ya wagojwa wapya 790 walipatiwa huduma za kulazwa miongoni mwao wagonjwa 350 walikuwa wanaume na wanawake ni 440. Kwa upande wa huduma za nje jumla ya wagonjwa 8,484 walipatiwa matibabu katika hospitali hiyo kati ya hao wanawake walikuwa ni 4,364 na wanaume 4,120. Idadi ya wagonjwa waliolazwa kwa mwaka huu imeongezeka ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo wagonjwa 574 walilazwa, hali hii inaweza kuashiria ongezeko la matatizo ya maradhi ya akili kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na utumiaji wa dawa za kulevya kwa vijana na ongezeko la hali ngumu za maisha pamoja na matatizo mengine ya kifamilia.

Mhe. Spika, ujenzi wa jengo la mapokezi, ofisi, pamoja na jiko unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Mbali na ujenzi huo, majengo ya wodi nambari moja ya wanawake na wodi nambari mbili ya wanaume yamefanyiwa matengenezo. Matarajio yetu ni kwamba kumalizika kwa ujenzi huu kutasaidia kupelekea utoaji wa huduma katika mazingira mazuri zaidi.

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi mmoja imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo kwa mwaka 2011/2012:-

a) Kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa, uchunguzi na matibabu kwa kuhakikisha vifaa na dawa muhimu zinapatikana wakati wote.
b) Kuendelea kutekeleza mradi na marekebisho ya utendaji ya hospitali kuu ya Mnazi Mmoja ili ifikie vigezo vya kuwa Hospitali ya Rufaa pia yenye kujitegemea.
c) Kuimarisha huduma katika wodi ya wazazi ili kupunguza vifo vya kinamama na watoto wachanga.
d) Kuimarisha huduma za afya ya akili *(Mental Health).*
e) Kuongeza baadhi ya vitengo hasa vya uchunguzi wa kansa na huduma za maradhi ya figo.

f) Kuongeza huduma za kisasa za matibabu ya maradhi ya moyo na yale mengine yasiyokuwa ya kuambukiza

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya mwaka 2011/12 Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 272,178.000 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA

Mhe. Spika, hii ni Idara mpya ambayo kazi zake zikitekelezwa chini ya Kitengo cha Dawa, Vifaa na Zana za Tiba. Idara hii ina jukumu la kupokea, kutunza pamoja na kusambaza dawa katika Hospitali na vituo vya Afya. Aidha, idara iliweza kupokea na kutunza dawa pamoja na zana za tiba kutoka vitengo mbali mbali, na kuweza kuzisambaza kwa wakati katika hospitali na vituo vya afya.

Mhe. Spika, ni jambo linaloeleweka kuwa Bohari kuu ya Dawa inahitaji eneo kubwa la kuweza kuhifadhia dawa na zana ambalo kwa sasa ni tatizo kubwa linaloikabili idara hii. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeipatia Wizara ya Afya moja ya jengo ambalo lilikuwa likitumiwa na Kiwanda cha Sigara. Wizara italifanyia ukarabati jengo hili ili liwe la kisasa kwa ajili ya kuhifadhia dawa na zana za tiba pamoja na usambazaji wake. Hatua za awali za kulifanyia ukarabati jengo hilo zinatarajiwa kuanza mara moja katika kipindi cha mwaka wa bajeti 2011/2012. Fedha kwa ajili ya mradi huu zitatolewa na serikali pamoja na ufadhili wa *USAID* na *DANIDA.*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 idara imejipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kubadilisha mfumo wa usambazaji wa dawa uwe wa mahitaji ya dawa zinazotakiwa badala ya ule wa kupeleka dawa hata kama hazitakiwi *(Push to Pull System).*

b) Kuimarisha utendaji katika bohari ya dawa.

Mhe. Spika, ili idara iweze kutekeleza malengo yake ya mwaka 2011/12 inaomba kuidhinishiwa jumla Tsh. 29,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa *(National Medicine Policy)*, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu *(essential medicines)*, zana za tiba katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Serikali, na kusimamia utumiaji sahihi wa dawa hizo *(rational medicine use).*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ofisi imefanikiwa kupokea dawa muhimu pamoja na zana za tiba kutoka sehemu mbali mbali ambazo zilisambazwa katika hospitali pamoja na vituo vyote vya Afya kwa ajili ya matumizi. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika kiambatisho namba 9.1

Mhe. Spika, kwa ufadhili wa *UNFPA* Ofisi ya Mfamasia Mkuu imefanikiwa kukipitia *(revise)* Kitabu cha Orodha wa dawa muhimu *(Essential Medicine list)*, na kupelekea kuwa na orodha mpya ya dawa muhimu ambazo ndizo zinazotumika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, utoaji wa dawa sahihi kwa mgonjwa ni jambo muhimu katika afya ya mwanadamu anapofikwa na maradhi, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ofisi imefanikiwa kutoa mafunzo kwa matabibu *(Prescribers)* na watoaji dawa *(Dispensers)* juu ya utumiaji sahihi wa dawa (rational medicine use) pamoja na kutoa vipeperushi kwa wafanyakazi, vinavyowakumbusha juu ya matumizi yalio bora ya dawa kwa mgonjwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ofisi imejipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa mafunzo kwa watabibu na watoaji dawa juu ya utumiaji sahihi wa dawa pamoja na kutoa vipeperushi kwa wafanyakazi na kwa wananchi juu ya matumizi yalio bora ya dawa.

b) Kwa kupitia ufadhili wa Shirika la Afya duniani *(WHO)*, ofisi inategemea kufanya utafiti juu ya utumiaji wa dawa kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na kutengeneza muongozo wa utoaji bora wa dawa *(Guidelines for good dispensing practice).*

Mhe. Spika, ili ofisi iweze kutekeleza malengo yake ya mwaka 2011/12 inaomba kuidhinishiwa jumla Tsh. 749,487,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, dawa na zana.

MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni chombo muhimu sana kwa Taifa. Maabara hii ina jukumu la kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kuthibitisha usalama na ubora wa vyakula na dawa kutoka ndani na nje ya nchi vinakuwa salama kwa afya za wanadamu. Maabara pia ina jukumu la kutoa ushauri juu ya matumizi bora ya kemikali na kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka taasisi tofauti vinavyohusiana na makosa ya jinai.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 maabara imeweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wote wanaofanya kazi za uchunguzi *(Analysts)* huko Tanzania Bureau of Standard *(TBS)* Dar es salaam. Mafunzo hayo yalihusu kujua viwango vya kitaifa na kimataifa vya sampuli mbalimbali. Pia maabara imeweza kununua baadhi ya kemikali na mashine za kufanyia uchunguzi kama vile "incubator" ambayo itasaidia katika kuimarisha utendaji mzuri wa kazi katika maabara.

Mhe. Spika, rasimu ya sheria ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(Chief Government Chemist Laboratory Agency)* imetayarishwa ambayo kwa sasa imefikishwa kwa Mwanasherika Mkuu wa Serikali kwa masahihisho ya mwisho kabla ya kuufikisha katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, maabara iliendelea na shuguli za kufanya kazi zake za uchunguzi, ambapo jumla ya vielelezo 482 vilichunguzwa katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011. Vielelezo hivi vinatoka, Wizara ya Mambo ya Ndani, Taasisi za Watu Binafsi na Wafanyabiashara kama inavyosomeka kwenye kiambatisho namba 10.1.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kufanya matengenezo makubwa ya jengo la Maabara ambalo maandalizi yake tayari yameshaanza baada ya kupatiwa jengo na serikali hapo Kiwanda cha Sigara Maruhubi

b) Kutayarisha rasimu ya Sheria ya Kemikali

c) Kuongeza vifaa vya kisasa vya kufanyia uchunguzi

Mhe. Spika**,** ili iweze kutekeleza malengo yake ya mwaka 2011/12 Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, inaomba kuidhinishiwa jumla Tsh. 55,096,000 kwa

matumizi ya kazi za kawaida, kati ya hizo Tsh. 47,700,000 Unguja na Tsh. 7,396,000 Pemba.

TAASISI MAALUM ZA WIZARA YA AFYA

Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar

Mhe. Spika, Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar kina jukumu la kufundisha wataalamu wa afya wa fani mbali mbali ili kupelekea kukidhi mahitaji ya watalamu hao katika sekta ya afya.

Mhe. Spika, chuo hiki kinaendelea kutoa mafunzo kwa viwango vya diploma katika fani za Uuguzi Ukunga, Uuguzi Magonjwa ya Akili, Maafisa Tabibu, Maafisa Afya Mazingira, Mafundi Sanifu wa Maabara na Mafundi Sanifu wa Madawa. Katika mwaka 2011 jumla ya wanafunzi 343 walihitimu mafunzo mbali mbali na wanafunzi wanaoendelea na mafunzo katika kada tofauti ni 566. Ufafanuzi unapatikana katika kiambatisho namba 11.1.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 chuo kimeanzisha Programu ya Afya ya Mazingira kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *Copenhagen* na *SUZA.* Katika kulifanikisha hilo mafunzo ya walimu wa walimu *(TOT)* yaliendeshwa na jumla wafanyakazi 27 kutoka taasisi mbali mbali walipata mafunzo hayo. Mhe. Spika, kwa mashirikiano na *Hankeland University Hospital Norway,* chuo kimeingiza mtaala wa mafunzo ya utengenezaji wa vifaa vya hospital *(Bio Medical Engineering).* Mafunzo haya yanategemewa kuendeshwa katika Chuo cha Afya katika mwaka 2012.

Mhe. Spika, Chuo kimeweza kuwaendeleza wafanyakazi wake kielimu ambapo jumla ya walimu 6 wanaendelea na mafunzo ya shahada ya kwanza katika vyuo vya Tanzania Bara na mmoja anatarajiwa kumaliza masomo ya Shahada ya Pili katika fani ya Medical Education nchini Uingereza. Aidha, jumla walimu 6 wamemaliza masomo yao ya shahada ya kwanza na wanaendelea kusomesha chuoni hapo.

Mhe. Spika**,** wizara imeendelea kupanua chuo hichi kwa kujenga jengo litakalotumika kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza pamoja na majengo mawili ya dakhalia kwa msaada wa Serikali ya Oman. Majengo haya yanatarajiwa kumalizika baada ya mwaka mmoja. Madhumuni ya upanuzi huu ni kuweza kutoa mafunzo ya juu ya shahada ya kwanza kwa kuanzia na kada ya Uuguzi.
Mhe. Spika, chuo kinakabiliwa na changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yake:-

a) Upungufu wa wafanyakazi wa kudumu hasa walimu.
b) Upungufu wa vitabu vya kisasa vya kufundishia.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012 chuo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuanzisha utaratibu mpya wa teknologia ya kisasa kupitia *"website"* utakaofuatwa na wanafunzi wakati wa kujiunga na chuo
b) Kuipitia mitaala ya masomo katika fani ya Afisa Tabibu, Afisa Afya ya Mazingira, na kada ya Dawa.
c) Kuimarisha ulinzi wa eneo la chuo kwa kujenga ukuta unaozunguka eneo hilo.
d) Kuanza maandalizi ya jengo la mikutano na la kusomeshea *(Conference and Lecture Hall)* na ujenzi wa jengo la kliniki ya chuo.

Maabara ya Afya ya Jamii (PHL – Idc) Pemba

Mhe. Spika, Maabara ya Afya ya Jamii *(PHL – IDC)* ni Taasisi inayoendeshwa kwa mashirikiano na Taasisi isiyo kuwa ya kiserikali *IVO DE CARNERI*, iliopo Milan - Italy. Lengo kuu la taasisi hii ni kufanya tafiti juu ya mienendo ya maradhi yanayoathiri afya ya jamii pamoja na kutafuta mbinu mbali mbali za kuyadhibiti.

Mhe. Spika, taasisi hii inasimamia miradi ifuatayo ambayo inagharamiwa na Jumuiya za Kimataifa. Miradi hiyo ni pamoja na:-

a) Mradi wa Kifua Kikuu: Mradi wa kifua kikuu unafanya uchunguzi wa kina kwa kutumia *TB microscopy, Concentration and Culture.* Aidha, una mpango wa kufanya utafiti wa uwezo wa dawa zinazotumika *(drug sensitivity testing)* chini ya ufadhili wa *Italian Cooperation.*

b) Mradi wa Mafunzo: Mradi huu unahusika na kutoa mafunzo ya *"Management of Programmes for Communicable Diseases Control in Sub–Saharan Africa", (MPCD 2010).* Inajumuisha washiriki kutoka bara la Asia, Marekani, Ulaya na Afrika. Lengo ni kuitangaza *PHL* katika ngazi za kimataifa. Mafunzo haya yanafadhiliwa na *IVO DE CARNERI FOUNDATION.*

c) Mradi wa Maji: Mradi huu unaendeshwa kwa mashirikiyano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Lengo la mradi huu ni kuangalia ubora wa maji.

d) Mradi wa Malaria: Mradi huu unahusika na uchunguzi wa malaria kwa kuchunguza upya asilimia 10 ya sampuli zote ambazo zimeonekana na vimelea vya malaria kutoka hospitali na vituo vya afya vinavyotumia darubini. Lengo ni kupata matokeo sahihi na bora ya uchunguzi wa malaria. Mradi huu unafadhiliwa na *Italian Co-oporation*.

e) Mradi wa Matumizi ya Dawa ya *Mebendazo*: Mradi huu unaangalia usalama wa matumizi ya dawa ya *mebendazole* ya kutafuna ya 500mgs kwa watoto wa miaka miwili mpaka kumi. Mradi huu unafadhiliwa na Johnson & Johnson.

Mhe. Spika, taasisi hii ina miradi mingi ya utafiti ambayo inasaidia sana kuongeza taaluma ya utafiti kwa vijana wa Zanzibar. Hata hivyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watalamu wenye sifa na ujuzi wa juu katika utafiti na wenye ubunifu wa tafiti zitakazowavutia wafadhili na kujenga mashirikiano na taasisi nyingine.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

Mhe. Spika, bodi hii inafanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 1994 *(Private Hospital Regulation Act)*. Kazi kubwa ya bodi hii ni kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa hospitali na vituo binafsi vya Afya kwa kuzikagua na kuzipatia maelekezo au hata kuzifunga kabisa pale zinapokosa vigezo vinavyotakiwa. Hivyo bodi huhusika na usajili na kutoa leseni na kuweka masharti ya uanzishwaji wa hospitali hizo. Kwa hivi sasa zipo hospitali na vituo binafsi vya afya 78, Unguja 67 na Pemba 11.

Mhe. Spika, bodi ilifanya ukaguzi katika hospitali na vituo binafsi vyote ambapo katika ukaguzi huo jumla ya hospitali na vituo binafsi 11 zilifungwa baada ya bodi kutoridhika na utaratibu wa uendeshaji. Hata hivyo vituo hivyo zilifunguliwa baada ya kukamilisha masharti waliyopewa. Mikutano ya kila baada ya miezi miwili kwa wajumbe wa Bodi ilifanyika ikiwa na lengo la kujadili mambo mbali mbali ya uendeshaji wa hospitali na vituo binafsi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 bodi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuhamasisha wamiliki kujenga hospitali za kisasa na kuwa na programu za kuwaendeleza kiutaalamu wafanyakazi wao.

b) Kuhakikisha upatikanaji takwimu sahihi za magonjwa kutoka hospitali binafsi.

c) Kukuza ushirikiano na jeshi la polisi na Serikali za mitaa katika kuhakikisha sheria zinafuatwa.

Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi.

Mhe. Spika, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ina jukumu la kisheria kudhibiti ubora na usalama wa Chakula, Dawa, Vipodozi na vifaa vya tiba.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi iliweza kufanya ukaguzi katika sehemu mbalimbali ili kuhakikisha usalama wa bidhaa hizo kwa matumizi ya wananchi. Jumla ya maduka ya chakula 270, ghala 20, mikahawa 20, maduka makubwa ya dawa 24, maduka ya dawa baridi (OTC) 150, maduka ya kuuzia nyama 40, machinjio 4, viwanda 4 na hoteli 7 za kitalii zilikaguliwa.

Mhe. Spika, maabara ya Bodi ilifanikiwa kuchunguza sampuli 440 za chakula, sampuli 417 zilikuwa salama na sampuli 23 hazikufaa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, sampuli 34 za dawa, dawa za tiba asili na vipodozi zilichunguzwa ambazo zote zilikuwa salama kwa matumizi.

Mhe. Spika, Bodi iliweza kuteketeza jumla ya tani 24.4 za mtama, tani moja ya mchele aina ya Basmat, ndoo 6 za asali zenye ujazo wa lita 120, chumvi isiyo na madini joto kilo 25, kontena moja la bidhaa mchanganyiko, kilo 232 za nyama. Sambamba na hilo jumla ya tani 28 za sukari na tani 234 za mchele zilirudishwa zilikotoka kwa mujibu wa sheria baada ya kubainika kuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 bodi ilifanikiwa kubaini kuwepo kwa bidhaa bandia katika masoko mbalimbali. Miongoni mwa bidhaa hizo ni pamoja na rangi za vyakula, vinywaji baridi, maji, maziwa na dawa za binadamu na mifugo. Baada ya kubaini matatizo hayo hatua za kisheria zilichukuliwa kwa wahusika 10 kufikishwa mahakamani.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Programu ya Malaria, Bodi iliweza kufanya ukaguzi katika vituo vya Afya vya Serikali na vile vya binafsi ili kubaini kuwepo kwa athari zisizotarajiwa za dawa "*Adverse Reaction*". Aidha, Bodi

iliweza kutoa elimu juu ya umuhimu wa mashirikiano katika udhibiti wa bidhaa za Chakula, Dawa, Vipodozi na vifaa vya Tiba kwa watendaji wa halmashauri, watoa huduma za Dawa, Chakula na watendaji wa vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 bodi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuongeza mashirikiano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kukabiliana na maradhi ya mifugo yanayoambukiza binadamu *(Zoonotic Diseases).*

b) Kushiriki katika mpango wa uchunguzi wa dawa zilizo chini ya kiwango na dawa bandia kwa Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*).

c) Udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa za kutibu malaria za bei nafuu.

d) Kudhibiti udanganyifu katika bidhaa za Chakula (Food Adulteration).

e) Kudhibiti bidhaa za chakula zenye kemikali hatarishi.

Baraza la Wauguzi na Wakunga

Mhe. Spika, Baraza la Wauuguzi na Wakunga linafanya kazi kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 1986. Baraza hili lina jukumu la kusajili wauguzi na wakunga waliopo Zanzíbar, kusimamia kazi za uuguzi, kusimamia haki za wauguzi, kunyanyua na kuendeleza huduma za uuguzi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mkunga au muuguzi yeyote atakayekwenda kinyume na maadili ya uuguzi na ukunga.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Wauguzi na Wakunga limeweza kutekeleza mambo mbali mbali ikiwemo kufanya ukaguzi wa Utendaji wa kazi katika hospitali na vituo vyote vya afya, kusimamia mafunzo ya uuguzi, kusajili na kuwapa leseni wauguzi wapya 50.

Mhe. Spika, baraza limefanya ukaguzi katika vyuo vya uuguzi vikiwemo vyuo vya watu binafsi na kutoa ushauri unaostahiki katika utoaji wa mafunzo yanayohusiana na fani ya uuguzi. Aidha, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha

Agakhan jumla ya wauguzi 16 (10 Unguja na 6 Pemba) wamepatiwa masomo ya kujiendeleza.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Bodi imejipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Kutafuta washirika wa maendeleo waweze kusaidia maendeleo ya uuguzi.
b) Kuwatafutia wauguzi fursa za masomo ya muda mrefu na muda mfupi.
c) Kutengeneza miongozo ya kuendesha na kusimamia huduma za kiuguzi.
d) Kuanzisha mfumo maalumu wa kusajili wauguzi kwa kutumia kompyuta (Computerized System).

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala *(Traditional and Alternative Medicine Council)* ni chombo kilichoundwa chini ya sheria No 8 ya mwaka 2008, na lina jukumu la kisheria kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa tiba asili na tiba mbadala.

Mhe. Spika, suala la kusajili waganga wa Tiba asili ni suala muhimu sana kwani tiba hii ikitolewa visivyo sahihi inaweza kuhatarisha afya za wananchi wetu. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 baraza limefanikiwa kuwasajili waganga wa kienyeji 81 ambao watakuwa wanatoa tiba ambayo imekubalika kisheria pamoja na kuwahamasisha masheha katika kufanya usajili wa waganga.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa waganga wa kienyeji wanatoa tiba sahihi kulingana na maelekezo ya afya, baraza limefanikiwa kutoa taarifa hizo kupitia mikutano yake ya kila mwezi ili kujadiliana juu ya utoaji wa ushauri na maelekezo katika utoaji wa huduma za tiba asili. Sambamba na hilo baraza limefanikiwa kutengeneza Kanuni (*Regulations*) za Tiba Asili na Mbadala na kutoa elimu kwa waganga.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 baraza limeazimia:-

a) Kuendelea kusajili waganga, maduka na vituo vya afya vya Tiba asili na mbadala.
b) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa tiba asili na mbadala.
c) Kuwafikia waganga wote kupitia masheha.

MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa Idara zote na taasisi za wizara sasa naomba uniruhusu kueleza utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Uendeshaji wa miradi hii unatokana na fedha za Serikali, misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wetu wa Maendeleo. Kwa kipindi cha mwaka 2010/11 Wizara ya Afya imekuwa ikitekeleza jumla ya miradi 7 ya maendeleo ambayo ni:-

a) Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya.
b) Mradi wa Kupambana na Maambukizo ya UKIMWI.
c) Mradi wa Chanjo za Mama na Mtoto.
d) Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto.
e) Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi.
f) Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Akili.
g) Mradi wa Chuo cha Madaktari cha Zanzibar.

Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya

Mhe. Spika, Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya una jukumu la kuratibu utekelezaji wa sera ya afya, kutengeneza miongozo mbalimbali ili iweze kutumika katika sehemu tofauti, kubuni njia na kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. Mradi huu pia unahusika na utengenezaji na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Sekta Afya

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Mradi umeweza kukamilisha mapitio ya Sera ya Afya toleo la mwaka 2011. Mapitio haya yalifanyika baada ya mabadiliko ya muundo wa Serikali, hali iliyopelekea kubadilika kwa baadhi ya malengo na mikakati.

Mhe. Spika, mradi umefanikiwa kuratibu Mkutano wa Tano wa Mwaka wa Mapitio ya Sekta ya Afya ambao unawakutanisha wadau wanaosaidia sekta hii pamoja na Washirika wa Maendeleo na asasi zisizo za serikali wa ndani na nje ya Zanzibar. Lengo kuu la mkutano huu ni kutathmini utekelezaji wa mpango wa mwaka wa kazi za Wizara ya Afya kwa kuangalia zaidi mafanikio na changamoto zilizoikabili sekta kwa mwaka husika.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, mradi umeweza kuratibu mapitio ya mkakati wa Afya ya Jamii *(Community Health Care Strategy).* Mkakati huu una lengo la kushirikisha jamii katika masuala ya afya na hatimaye kufanya maamuzi juu ya afya zao.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha huduma zitolewazo hospitalini zinakuwa na viwango na ubora unaostahiki kitaifa na kimataifa, mradi kwa kushirikiana na Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja wametayarisha muongozo wa kutathmini ubora wa huduma za afya "*Quality Assessment Tool"*.

Mhe. Spika, ripoti ya mapitio ya matumizi ya fedha kwa sekta ya afya 2008/2009 *(Public Expenditure Review)* imekamilika. Ripoti hiyo husaidia kujua vyanzo vya fedha na matumizi katika sekta ya afya ili kuweka mikakati kwa mwaka unaofuata.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 mradi umejiwekea malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu utowaji wa huduma za uzazi katika vituo vya afya 34 vilivyopendekezwa.
b) Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa afya ya jamii *"Community Health Care Strategy"*
c) Kuandaa mwongozo wa rufaa ili uweze kutumika hospitalini
d) Kufanya mapitio ya mpango mkakati wa afya wa miaka mitano
e) Kuandaa mpango wa muda mrefu wa jinsi ya kugharamia sekta ya afya.

Mradi wa Kudhibiti Maambukizo ya UKIMWI Zanzibar

Mhe. Spika, Mradi wa Kudhibiti Maambukizo ya UKIMWI una jukumu la kuratibu kazi za kuzuia kasi ya ueneaji wa Virusi vya UKIMWI katika jamii, kuwahudumia wagonjwa walioambukizwa, kupunguza unyanyapaa kwa waathirika wa VVU na kutoa elimu ya afya kwa jamii juu ya tabia zinazochangia maambukizo ya VVU.

Mhe. Spika, Utafiti uliofanyika mwaka 2007/08 "*Tanzania HIV and Malaria Indicator Survey" (THMIS)* umeonyesha kuwa asilimia 0.6 kwa watu wenye umri wa miaka 15-49 wanaishi na VVU. Aidha, Uchunguzi wa VVU kwa kinamama waliopimwa katika vituo vinavyotoa huduma ya mama na mtoto inaonyesha kwamba asilimia 0.6 wameathirika.

Mhe. Spika, majukumu mengine ya mradi huu ni kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto *(PMTCT Services),* huduma hizi zinaendelea kutolewa katika vituo 39 katika kliniki za mama wajawazito na watoto. Hadi kufikia Machi 2011 vituo vimeengezeka kufikia 49 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 jumla ya wajawazito 33,779 walihudhuria katika kliniki ya huduma za ujauzito, kati ya hao 30,864 (91.4%) waliochunguzwa Virusi vya UKIMWI na wajawazito 201 (0.7%) waligundulika na virusi vya UKIMWI. Takwimu zinaonyesha kwamba asilimia ya waliochunguzwa kwa mwaka 2009/2010 haina tofauti na waliochunguzwa mwaka 2010/2011. Sijui inatupa matumaini kwamba hali si mbaya.

Mhe. Spika, mradi umefanikiwa kutanua huduma za tiba kwa wagonjwa wa UKIMWI, jumla ya hospitali 8 zinatoa huduma hizo. Hospitali nyengine 4 (Makunduchi, Abdalla Mzee, Ubago na Ali Khamis Camp) zimefanyiwa tathmini. Kati ya hizo hospitali ya Ubago haikufikia kiwango cha kutoa huduma. Zile nyengine zitaanza kazi mara moja.

Mhe. Spika, elimu kwa makundi hatarishi huwa inatolewa. Makundi yenyewe ni wanaume wanaofanya tendo la ngono na wanaume wenziwao (MSM), wanawake wanaofanya biashara ya ngono (FSW) *(female sex workers)* na wale wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya sindano (IDUs). Kwa kipindi cha mwaka 2010, jumla ya wateja 1,379 wa kundi la (MSM) na (FSW) walipewa elimu juu UKIMWI. Kati yao wateja 1,013 walikubali kupimwa kwa hiari maambukizi ya VVU (530 MSM, 483 FSW) ambapo wateja 48 (14 MSM, 34 FSW) waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Wameshawishiwa wamekwenda wamekutikana na maradhi. Mh! Hatari.

Mhe. Spika, msaada wa chakula kutoka *"Clinton Heath Access Initiative"* (CHAI) hutolewa kwa wagonjwa wanaopata matibabu katika kliniki ya huduma na tiba. Hadi Disemba 2010, jumla ya wagonjwa 538 (361 Wanawake na 177 wanaume) wameorodheshwa na kupewa chakula.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010, jumla ya watu 73,046 (35,641 wanawake na 37,405 wanaume) walichunguzwa katika vituo 55 vya ushauri nasaha na upimaji VVU wa hiyari. Aidha, watu 10,059 (3,756 wanawake na 6,303 wanaume) waliochunguzwa VVU kupitia vituo vya dharura. Kati ya waliopimwa katika vituo vya dharura 1,729 (17%) waligundulika kuwa wanaishi na VVU; wanawake ni 1,106 na wanaume ni 623.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 mradi umejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kuimarisha tiba na ushauri kwa kuwapatia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV) kwa watu wanaoishi na VVU bila malipo kwa wale wote wanaostahiki.

b) Kuimarisha na kupanua huduma za kuzuia maambukizo ya mama kwenda kwa mtoto Unguja na Pemba katika vituo vinavyotoa huduma za mama wajawazito kufikia asilimia 50 kutoka asilimia 24.

c) Kuimarisha na kupanua huduma za Ushauri nasaha na upimaji na kuhakikisha nyenzo na vifaa vinapatikana kwa wakati.

d) Kufanya utafiti wa kujua idadi ya watu wa makundi maalum na kasi ya mambukizi ya UKIMWI kwenye makundi hayo.

e) Kutumia mwongozo mpya wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto unaozingatia mapendekezo mapya ya Shirika la Afya Duniani.

f) Kuendelea kuwahamasisha na kuielimisha jamii na watoa huduma za afya kwa njia ya vyombo vya habari, vipeperushi juu kupunguza unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU.

g) Kushirikiana na Idara ya madawa ya Kulevya na Kurekebisha tabia kwa kuanzisha utoaji wa huduma na tiba na kuwapatia dawa watumiaji 200 wa madawa ya kulevya.

Mradi wa Chanjo za Mama na Mtoto

Mhe. Spika, Mradi wa Chanjo za Mama na Mtoto ni miongoni mwa miradi inayotoa huduma za msingi za afya ya mama na mtoto. Kazi ya msingi ya mradi huu ni kutoa chanjo kwa watoto na mama dhidi ya magonjwa tisa yanayozuilika kwa chanjo ambayo ni Kifua Kikuu, Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya ini, Homa ya uti wa mgongo, Kichomi, Polio (kupooza) na Surua.

Mhe. Spika**,** Huduma za chanjo za mama na mtoto ziliendelea kutolewa katika vituo vyote vyenye huduma za afya ya uzazi Unguja na Pemba. Mradi wa chanjo ulijipangia lengo la kuchanja kufikia asilimia 90 kwa chanjo zote katika wilaya 8 kati ya kumi za Zanzibar. Juhudi zaidi zitaelekezwa katika wilaya za Micheweni na Mkoani ambazo hazijafikia lengo.

Mhe. Spika, katika eneo ambalo tumefanikiwa sana ni mradi wa chanjo za mama na mtoto ambapo baadhi ya chanjo zimefikia zaidi ya asilimia 90. Hata hivyo chanjo ya mwanzo ya polio baada tu ya kuzaliwa mtoto (*Polio zero*) inaonekana kuwa chini ya lengo. Kwa ufafanuzi zaidi angalia viambatisho namba 12.1a na 12.1b.

Mhe. Spika**,** Mikutano ya uhamasishaji jamii juu ya umuhimu wa chanjo kwa watoto ilifanyika kwa wilaya zote za Unguja na Pemba. Mikutano hii iliwashirikisha viongozi katika ngazi ya jamii wakiwemo masheha, viongozii wa kidini, wahamasishaji, wakunga pamoja na watu wengine maarufu katika vijiji. Lengo ni kuwafikia watoto wote wanaostahiki kuchanjwa ikiwa katika vituo vya afya au wakati wa kampeni ya chanjo.

Mhe. Spika**,** kutokana na viwango vya chanjo kwa upande wa Pemba kuwa si vya kuridhisha sana, mradi wa chanjo umefanya utafiti wa kuangalia usahihi wa takwimu za chanjo *"coverage survey*". Matokeo ya utafiti huo yatatuwezesha kujua sababu za viwango vya chini kwa Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Mradi umejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuinua kiwango cha chanjo kufikia 90% kwa wilaya zilizo chini ya lengo.
b) Ukarabati wa ofisi ya chanjo Pemba na kujenga vyumba vya baridi (*cold rooms)* Unguja na Pemba.

c) Kuwaendeleza wafanyakazi wa ngazi zote kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali (yakiwemo ya uongozi na ya utekelezaji wa kazi za chanjo kila siku).

d) Kufanya kampeni ya chanjo ya surua.

e) Kuanzisha chanjo mpya dhidi ya maradhi ya homa ya kichomi (*pneumococcal vaccine).*

Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Spika, Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto una jukumu la kuimarisha afya ya mama na mtoto kwa nia ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Kazi hizi zinachangia kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia namba 4 na 5 na (MKUZA II).

Mhe. Spika, Majukumu ya Mradi wa afya ya uzazi na mtoto ni kuratibu shughuli za uzazi salama zinazojumuisha huduma za mama wajawazito, huduma za kujifungua, huduma baada ya kujifungua, huduma ya mama wenye kuharibikiwa na mimba, uzazi wa mpangilio, huduma rafiki kwa vijana na uchunguzi wa saratani za kizazi. Pia kwa kushirikiana na mradi wa kudhibiti

maambukizo ya UKIMWI unatoa huduma za kuzuia maambukizo VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi uliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa kuharakisha kupunguza vifo vya kinamama na watoto (*Road Map to Accelerate Reduction of Maternal and Child Mortality).* Lengo la mpango huu ni kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi kufikia 130 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2015. Takwimu zinaonyesha kwamba hali ya vifo vitokanavyo na uzazi katika hospitali za Zanzibar imepungua kutoka 422 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2008 hadi kufikia 287 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2010.

Mhe. Spika, vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vimefikia asilimia 51 katika kila watoto 1,000 waliozaliwa hai kwa mwaka 2010 kutoka vifo 54/1000 kwa mwaka 2008. Wastani huu unakaribia kufikia lengo namba 4 la milenia la kupunguza idadi ya vifo vya watoto kufikia vifo 40/1000 ifikapo mwaka 2015. Aidha, vifo vya watoto wa chini ya miaka 5 vimepungua kutoka 79/1000 mwaka 2008 hadi 73/1000 mwaka 2010. Lengo la milenia ni kufikia wastani wa vifo 67/1000 ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2010/2011 mikakati mbali mbali ilitekelezwa ili kuwezesha kufikia malengo hayo ikiwemo kuongeza vituo vya kutoa huduma za kuzalisha kutoka 14 mwaka 2009/2010 hadi 18 mwaka huu. Takwimu zinaonyesha kwamba jumla ya wajawazito 793 walijifungua katika vituo hivyo ukilinganisha na wajawazito 636 waliojifungua 2009/2010. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 12.2.

Mhe. Spika, licha ya mafanikio hayo bado kuna idadi kubwa ya wajawazito wanaojifungulia majumbani chini ya usimamizi wa wakunga wa jadi. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2010 taarifa zinaonyesha kwamba asilimia 50 ya wajawazito wanajifungulia majumbani, hali inayoweza kuhatarisha maisha ya mama na mtoto. Katika kukabiliana na tatizo hilo uhamasishaji unafanywa katika ngazi tofauti.

Mhe. Spika, huduma za uchunguzi wa mama baada ya kujifungua unaimarika siku hadi siku. Jumla ya kinamama 1078 walihudhuria katika kliniki na kupatiwa huduma hizo katika kipindi cha siku 2 hadi 7. Takwimu zinaonyesha kwamba idadi kubwa ya kinamama bado hawajapata mwamko wa kutumia huduma hizi. Hivyo tunawaomba kinamama wanaojifungua kuhudhuria kliniki mara baada ya kujifungua kwa mpangilio uliowekwa. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 12.3.

Mhe. Spika, huduma rafiki kwa vijana zimeendelea kutolewa kwa vijana walio na umri kati ya 10 mpaka 24. Huduma hizi zinatolewa katika vituo 20 (10 Unguja 10 Pemba) kwa lengo ya kuwawezesha vijana kupata elimu juu ya masuala ya afya ya uzazi, kujikinga na mimba katika umri mdogo, kujikinga na maambukizi ya VVU na huduma nyengine za afya ya uzazi. Kwa kipindi cha Julai 2009 hadi machi 2010 jumla ya televisheni 5 na DVD 10 zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma hizo.

Mhe. Spika, kazi nyingine muhimu iliyofanywa na mradi huu ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpangilio. Kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 jumla ya watumiaji wapya 7586 walisajiliwa katika kliniki mbali mbali za Unguja na Pemba. Aidha, utafiti wa Tanzania Demografia na Afya *(Tanzania Demographic and Health Survey 2010)* uliofanywa mwaka 2010 unaonyesha kwamba watumiaji wa huduma za uzazi wa mpangilio wameongezeka kutoka asilimia 9 mwaka 2004/05 hadi asilimia 12 kwa mwaka 2010.

Mhe. Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za mradi huu miongozo mbali mbali imetayarishwa ikiwemo mwongozo wa kukusanyia taarifa za huduma za mama na mtoto na mwongozo wa huduma za mama baada ya kujifunguwa *(Post Natal Care Guideline)*.

Aidha, mradi uliendelea kutoa mafunzo juu ya umuhimu wa matumizi ya njia za uzazi wa mpangilio kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya, Viongozi wa kidini na Wakunga wa jadi wakiwemo wahudumu wa kujitolea ili kuondokana na dhana potofu kwa jamii juu ya huduma hizi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi umejipangia kutekeleza kazi zifuatazo:-

a) Kuendelea kuimarisha huduma za mama na mtoto
b) Kushajiisha jamii ili wajawazito waweze kujifungua katika hospitali na vituo vya afya pamoja na kuhudhuria kliniki baada ya kujifungua.
c) Kuendelea kushajiisha jamii kutumia njia za uzazi wa mpangilio
d) Kuimarisha huduma rafiki kwa vijana (*Youth Friendly Services*)
e) Kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa vya uzazi.
f) Kushajihisha ushirikishwaji wa wanaume ikiwemo viongozi wa dini katika huduma za afya ya uzazi pamoja kutumia njia za uzazi wa mpangilio.

Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vinavyotokana na Uzazi

Mhe. Spika, Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi ulianzishwa mwaka 2007 na utamalizika mwaka 2012, chini ya ufadhili wa Serikali pamoja na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Mhe. Spika**,** lengo kuu la mradi huu ni kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuimarisha miundo mbinu ya wizara pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wake.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 jumla ya wafanyakazi nane wamepelekwa masomoni kusomea fani mbali mbali katika vyuo vya Tanzania Bara na nchini Uganda. Aidha, vijana (28) wamepelekwa Tanzania Bara kwa masomo ya Waganga wasaidizi (*Clinical Officer)* kwa ufadhili wa mradi huu.

Mhe. Spika, katika hotuba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2010/2011 ilielezwa hatua zilizofikiwa katika ukamilishaji wa nyumba ishirini (20) za wafanyakazi kwenye vituo vya afya huko Pemba.

Nafurahi leo hii kulieleza Baraza lako tukufu kuwa nyumba zote ishirini (20) zimekamilika na kukabidhiwa Wizara ya Afya na kwamba tayari zimeshakabidhiwa kwa wafanyakazi. Naipongeza Kampuni ya "*Mazrui Building Contractor"* pamoja na Wahandisi wa Mradi huu kwa juhudi walizozionyesha kufanikisha ujenzi huo.

Mhe. Spika, sambamba na mafanikio haya wizara kupitia mradi huu imeweza kuvipatia vifaa na samani vituo vya afya vya Matemwe, Mahonda, Chwaka kwa Unguja Kojani, Konde na Kengeja huko Pemba ambavyo vimejengwa upya ama kutanuliwa.

Mhe. Spika, wizara imekuwa ikitoa maelezo ya azma ya kujenga jengo la kuhudumia wagonjwa wa akili kisiwani Pemba (Hospitali ya Wete). Nachukuwa nafasi hii kulieleza Baraza lako tukufu kwamba ujenzi huo umeanza rasmi chini ya *"Stance Technic and Civil Engineers Limited"* ya Arusha, Tanzania na kusimamiwa na wahandisi wa mradi huu. Ujenzi huu utagharimu kiasi cha Tsh. 306,788,585.60

Mhe. Spika, baada ya kupata mafanikio makubwa ya utekelezaji, wizara inafanya juhudi ya kuona mradi unaongezewa muda zaidi baada ya kumaliza muda wake ifikapo Disemba 2012.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2011/2012 mradi umejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi *(short course)* kwa walimu 10 wa Chuo cha Taaluma za Sayanzi za Afya – Mbweni.

b) Kugharamia mafunzo ya kipindi cha mwaka mmoja kwa walimu 3 na wafanyakazi wengine 2 kutoka Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni.

c) Kusimamia ujenzi na kulipatia vifaa na samani jengo la Huduma za Afya ya Akili Pemba.

d) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya mradi baada ya kukamilika miaka 4 ya utekelezaji wake.

e) Kufuatilia wafanyakazi waliopatiwa masomo kupitia mradi huu, kuangalia sehemu wanazofanya kazi baada ya kurudi masomoni.

Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Akili

Mhe. Spika, Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Akili una jukumu kuu la kuratibu shughuli zote za Afya ya Akili Zanzibar, ikiwemo kusimamia haki na ustawi wa watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 jumla ya wanafunzi 851 (wanaume 381 na wanawake 470) wapya wanaoanza masomo kutoka skuli 16 za wilaya za Unguja walifanyiwa uchunguzi wa afya ya akili. Lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata elimu bila ya kujali hali ya kiafya au ulemavu na wale walioonekana na matatizo wamepatiwa matibabu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi uliendelea kutoa huduma za kufuatilia wagonjwa vijijini *(out-reach services)*, hadi kufikia machi 2011 jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma ni 670 (wanawake 355 na wanaume 315).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi umejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukarabati wa Majengo ya Hospitali ya Wagojwa wa Akili Kidongo Chekundu.

b) Kutoa mafunzo kwa watoa huduma ili kuweza kugundua dalili na matatizo ya afya ya akili na kuweza kuyatibu kwa wakati.

Mradi wa Chuo cha Madaktari Zanzibar

Mhe. Spika, Mradi una lengo la kutoa mafunzo ya udaktari hapa nchini kwa nia ya kuongeza idadi ya wataalamu katika fani hiyo na kupunguza gharama za kuwapeleka masomoni nje ya nchi.

Mhe. Spika, hadi kufikia sasa jumla ya wanafunzi 38 wanaendelea mwaka wa tatu hapa Unguja na 12 wanaendelea mwaka wa pili kisiwani Pemba. Kuwepo kwa Chuo hiki Zanzibar kutapelekea kupunguza uhaba wa madaktari kwa gharama nafuu na muda mfupi.

Mhe. Spika, mfumo huu wa ufundishaji ni bora zaidi kuliko ule uliozoeleka kwani una wapa fursa wanafunzi kupata mafunzo ya vitendo tokea mwaka wa mwanzo, unawawezesha kujua hali ya kiafya katika mazingira yao halisi na pia jamii inapata fursa ya kuhudumiwa na wanafunzi hao katika kipindi chote cha mafunzo.

Mhe. Spika**,** Chuo kimejiwekea malengo yafuatayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012:-

a) Kukifanya chuo kitambulike na elimu ya juu Tanzania.

b) Kushirikisha madaktari wazalendo katika utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wetu.

c) Kununua vitendea kazi bora kwa maendeleo ya chuo na wanachuo kwa jumla.

d) Ufuatiliaji wa upatikanaji wa miundombinu bora ya utekelezaji wa shughuli za chuo.

Mhe. Spika, mbali na utekelezaji wa miradi hiyo, wizara kwa mwaka wa fedha ujao 2011/2012 itatekeleza jumla ya miradi minne mipya nayo ni:-

a) Mradi wa Ujenzi wa Bohari kuu ya Dawa

b) Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

c) Mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja

d) Mradi wa kuzipandisha hadhi Hospitali za Vijiji na Wilaya

Mhe. Spika, ili miradi hii iweze kutekeleza malengo yake ya mwaka 2011/12 Wizara ya Afya inaomba kuidhinishiwa jumla Tsh. 2,500,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, kuna changamoto kama tano ya kwanza upatikanaji wa dawa muhimu **b**ado haujatupa matumaini kwa sababu dawa chache tunazotumia katika hospitali zetu ni zile za msaada kutoka DANIDA.

Mhe. Spika, upatikanaji wa dawa muhimu bado haujatupa matumaini kwa sababu dawa chache tunazotumia katika hospitali zetu ni zile za msaada kutoka *DANIDA*. Wagonjwa kununulishwa dawa bado ni changamoto kubwa na inaendelea kutusumbua, ukweli ni kwamba suala hili hatulifurahii hata kidogo.

Mahitaji ya dawa muhimu kwa mwaka hazipungui Tsh bilioni tatu. Kiwango kinachotegemewa kutokana na misaada ya wahisani kwa ununuzi, utuzanzaji na usambazaji wa dawa ni Tsh. Bilioni 1.5. Serikali kwa mwaka huu imetutengea Tsh. 700,237,000/= kwa dawa na zana.

Mhe. Spika, moja katika tatizo sugu ambalo linalalamikiwa sana na wananchi ni kutokuwa na mfumo mzuri wa kuchangia huduma za matibabu. Suala hili limezaa mjadala mkubwa sana wakati wa Baraza lililopita pale wajumbe wa Baraza hili wakiwakilisha ripoti za Kamati za Baraza.

Mhe. Spika, suala la uchangia wa huduma za afya lilielezwa bayana katika sera ya afya ya mwaka 1999 ilipitishwa na kukubaliwa na Wajumbe wa Baraza katika mkutano wa tano kikao cha 19 mwaka 2000. Hivyo, hivi sasa wizara imo katika hatua za mwisho kukamilisha utaratibu wa kuchangia unaooleweka kulingana hali za wananchi wetu.

Mhe. Spika, kuimarika kwa huduma bora za afya kunaonekana kutetereka kutokana na uhaba wa wafanyakazi hasusan madaktari na wauguzi pamoja na watendaji wengine wenye fani tofauti. Mahitaji ya madaktari bingwa (*specialist*) ni 109 na waliopo ni 17 tu, madaktari (*MD*) walipo 18 mahitaji ya wizara 55, kwa sasa tuna wauguzi 305 wanaohitajika 941. Ufafanuzi wa idadi iliopo na mahitaji halisi inaonekana katika kiambatisho 13.1

Mhe. Spika, wizara inaendelea kuchukua hatua za dharura na za kudumu katika kupunguza na hatimae kumaliza kabisa tatizo hilo. Upungufu wa madaktari utazidi kutoweka pale wanafunzi 38 wa Chuo cha Madaktari waliofika mwaka wa tatu waliopo hapa Unguja na wanafunzi 12 walioko huko Pemba watakapomaliza masomo yao. Aidha, Chuo cha Afya kinaongeza idadi ya wanafunzi wa fani mbali mbali ambao ni matarajio yetu kwamba watasaidia kupunguza tatizo hili.

Mhe. Spika, kumekuwepo na kilio cha muda mrefu sana kuhusu ufinyu wa maslahi ya wafanyakazi wa fani zote zikiwemo za afya na fani nyingine tofauti. Malalamiko haya yamezaa utamaduni dhaifu wa madaktari na wauguzi kukimbilia kufuata maslahi mazuri nje ya Zanzibar na kwenye sekta binafsi. Taarifa zinaeleza kwamba katika kipindi cha miaka 10 iliopita jumla ya madaktari zaidi ya 15 na wauguzi wapatao 70 wameondoka katika sekta ya afya. Maradhi haya yameanza kuambukizwa na katika kada nyengine.

Mhe. Spika, naomba kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Nchi, Ofisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutangaza kuwepo kwa mabadiliko ya mafao ya wafanyakazi katika mwaka huu wa fedha. Ni mategemeo ya wizara kwamba tofauti ya mishahara ya wafanya kazi wa afya wa Bara na Zanzibar haitokuwa kubwa sana hivyo hatutegemei wafanya kazi wetu kukimbia kwa sababu ya maslahi.

Mhe. Spika, tunaomba wafanyakazi wetu wajenge uzalendo baada ya serikali kuzingatia maslahi yao. Wizara itaendelea kufanya kila juhudi kuhakikisha kwamba maslahi yao kama sare za kazi na malipo ya zamu za usiku yanawekewa utaratibu unaoeleweka na kuelezwa bayana.

Mhe. Spika, **K**itengo cha Huduma za Dharura (*Intesive Care Unit*) hakiko katika hali nzuri. Katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kilichopita Wajumbe walitoa maagizo mazito juu ya kutaka kuona hali hii inabadilika.

Mhe. Spika, gharama za kukiweka katika hali nzuri ili kiwe cha kisasa haipungui Tshs. 800,000.000, matengenezo yake ni makubwa na wizara haitomudu kutimiza maagizo ya Kamati ya Baraza lako kwa muda mfupi. Hata hivyo, juhudi zinafanywa ili kuona kitengo hicho kinakuwa katika hali nzuri na ya kuridhisha.

Mhe. Spika, kuongezeka kwa maradhi yasioambukiza kama vile kisukari, saratani, moyo na maradhi ya kibofu cha mkojo ni moja kati ya hali ya kutisha inayoikabili sekta ya afya. Ni vizuri Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wote kwa ujumla, kuelewa kwamba katika kipindi hiki nchi yetu imekuwa inakabiliwa na maradhi ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza, na hivyo kuongeza gharama za matibabu.

Mhe. Spika, kuongezeka kwa maradhi haya ni kutokana na mwamko mdogo kwa jamii kuelewa kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Ukweli wa hali ilivyo katika jamii ni kwamba wananchi sote tunaumwa na wala hatutaki kukubali kwamba tunaumwa. Naomba kutoa wito kwa wananchi wote kuwa na tabia ya kupima afya zetu kabla hatujaumwa.

Mhe. Spika, wizara imeamua kuelekeza mbinu zake mpya za kukabiliana na matatizo haya kwa kuweka kipaumbele katika kuimarisha elimu ya kinga mijini na vijijini ambayo itaunganishwa pamoja na kitita cha afya ya msingi (*Essential Health Care Package - EHCP*). Kuanzia sasa huduma katika vituo vyetu vya afya zitakuwa ni huduma zinazojumuisha jamii na watoa huduma kwa pamoja katika masuala ya tiba na kinga (*Community Health Strategy*) na dhamana kubwa ya masuala haya yatashirikisha Kamati Kiongozi za Afya za Shehia (*Health Custodian Committees*)

Mhe. Spika, changamoto nilizozieleza ni kubwa sana, mashirikiano ya kutosha kutosha kutoka kwa Wadau wa maendeleo, Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge na Taasisi binafsi ikiwemo jamii yenyewe yatasaidia sana kupunguza matatizo ya kiafya kwa wananchi wetu.

MALENGO MAKUU YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Afya itaendelea na jitihada zake za utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa kuzingatia Sera ya Afya 2011, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na MKUZA II. Katika kutekeleza hayo Wizara imejiwekea malengo makuu yafuatayo:-

a) Kuweka mfumo utakaoainisha mgawanyo wa wafanyakazi wa afya ambao utazingatia taaluma waliyonayo na kwa kuzingatia mahitaji ya sehemu.
b) Kufanya maandalizi ya mfumo ya majaribio ya mfumo wa kutathmini ufanisi wa utendaji wa kazi kwa ngazi ya kituo na hospitali katika wilaya mbili kwa kuzingatia viashiria vya afya.
c) Kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa uchangiaji wa huduma za afya.
d) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Afya ya Jamii (*Community Health Strategy).*
e) Kufanyia ukarabati mkubwa wa majengo yaliyokuwa ya kiwanda cha sigara kwa ajili ya Bohari Kuu ya Dawa na Maabara ya Mkemia Mkuu.
f) Kuchukua hatua za awali kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa.
g) Kuanza matayarisho ya kuzipandisha daraja Hospitali za Kivunge, Micheweni, vitongoji, Wete na Abdalla Mzee.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kila mmoja anahitaji kuwa na afya bora kwa muda wote, na pale atakapohitaji huduma za afya basi azipate kwa wepesi na urahisi kulingana na mahitaji. Hili ndilo lengo kubwa la Wizara ya Afya kwa wananchi wa nchi hii. Hata hivyo, napenda kusisitiza tena kupatikana kwake hakuwezi kutegemea Wizara ya Afya peke yake, bali itategemea pia ushiriki wa taasisi za Afya za Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, makundi ya kijamii na hata mtu mmoja mmoja. Wizara ya Afya itajitahidi kuwashauri wadau wote wa sekta ya afya na jamii kwa jumla ili tuweze kufikia lengo la afya kwa wote kwa wepesi na ufanisi.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa huduma za afya kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 yalishajiishwa na michango mbali mbali iliyotolewa na wajumbe wa Baraza lako wakiwa ndani na nje ya Baraza. Sina budi kuwashukuru kwa hilo na natumai wataendeleza utaratibu huo kwa lengo lile lile la kuwapatia huduma bora wananchi na si vyenginevyo.

Mhe. Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitowashukuru viongozi wenzangu ndani ya wizara kwa mashirikiano na michango mikubwa walionipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa urahisi na kwa ufanisi. Naomba nitoe shukrani zangu za pekee kwa Naibu Waziri wa Wizara hii Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya, Katibu Mkuu Dk. Mohamed Saleh Jiddawi na Mkurugenzi Mkuu wa Afya Dk. Malik Abdalla Juma, pamoja na Wakurugenzi wote. Aidha, pongezi maalum ziende kwa timu ya wataalamu waliosaidia kuandika, kunakili na hatimae kuichapisha hotuba hii nikaweza kuisoma mbele ya Baraza lako.

Nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa misaada wanayonipa na kwa juhudi kubwa walizoonyesha katika kuwatumikia wananchi pamoja na hali ngumu wanayopambana nayo, hasa ukosefu wa nyenzo na maslahi hafifu. Nawaomba waendelee na moyo huo huo wa upendo kwa wale wote wanaowahudumia.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imepata mchango mkubwa kufanikisha malengo haya kutoka mashirikia ya Kitaifa na Kimataifa, pamoja na nchi marafiki, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, wahisani wa ndani na nje ya nchi. Misaada yao na michango yao mbali mbali tunaithamini sana na wizara kwa dhati kabisa inawashukuru. Napenda shukrani hizo ziende kwa *WHO, UNFPA, UNICEF, UNDP, ADB, SIGHT SAVERS, WORLD BANK, HEALTH FOUNDATION, CLINTON FOUNDATION, PEPFAR, AGAKHAN, ITALIA COOPERATION, SAVE THE CHILDREN, GAVI, USAID, CDC, DANIDA,*

GLOBAL FUND, JICA, IVO DE CARENERI FOUNDATION. Mhe. Spika, pia shukran zetu ziende kwa Serikali za Japan, Uingereza, Cuba, Marekani, Egypt, India, Oman, Israel, China, Hispania na wale wote ambao sikuwataja katika hotuba yangu hii.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2011-2012

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu na malengo ya wizara kupitia Idara na taasisi za Wizara ya Afya, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu lipokee na kujadili na hatimae kuidhinisha matumizi ya Tsh. 10,727,000,000 kati ya hizo Tsh. 8,627,000,000 kwa mishahara na maposho, Tsh.2,100,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh.2,500,000,000 kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo. Hivyo, naliomba baraza lako kuturuhusu kutumia jumla ya Tsh. 13,227,000,000. Aidha, wizara inatarajia kukusanya jumla ya Tsh. 537,000,000 kutokana na vianzio vyake ikiwemo michango ya wananchi katika kuchangia huduma za afya na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, kwa idhini yako Naomba kutoa hoja.

Kiambatisho Namba 3.1: **Wafanyakazi wa kudumu walioajiriwa na Wizara ya Afya kwa kipindi cha Julai 2010 - Machi 2011**

KADA	W/UME	W/KE	JUMLA
Pharmacentical Tech	13	5	18
Public Health Nurse "B"	**	27	27
Leboratory Tech	15	7	22
Health Officer	14	8	22
Mwanasheria	1	0	1
Afisa Utawala	1	0	1
Mfamasia	1	2	3
Mhandisi – (Electric Eng)	0	1	1
Mhandisi - Bio Medcal Tech	0	1	1
Bio Chemist	0	3	3
Medical Officer	0	2	2
Clinical Officer	14	11	25
Dental Therapist	1	1	2
Dental Surger	1	1	2
Economist	0	1	1
Physiotherapist	1	0	1
Jumla	**62**	**70**	**132**

** *Kada hii ni kwa wanawake tu*

Kiambatisho Namba 3.2: **Taarifa ya Mafunzo kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011**

No.	KOZI	CHUO	KUANZA NA KUMLIZA	WALIOPELEKWA		JUMLA
				W/ME	W/KE	
1	BSC. SOCIAL WORK	UGANDA	Sept. 2010 – Sept. 2013	0	1	1
2	BSC MEDICAL IMAGE	MENGO UNIVESITY-UGANDA	Sept.2010 - Sept. 2011	4	0	4
3	ADVANCED DIPLOMA IN MENTAL HEALTH	MUCHS	2010-2012	1	1	2
4	ADV. DIP IN MARKETING, PROCUR. AND SUPPLY	DODOMA	Sept. 2010 - Sept. 2012	0	1	1
5	BSC – NURSING	DODOMA	Sept. 2010 – Sept. 2013	1	0	1
6	BSC. NURSING MGT	MUCHS	Sep. 2010 – Sep. 2013	1	0	1
7	M. D	IMTU	Sep. 2010	5	0	5
8	BSC. DIAGNOSTIC ULTRA SOUND	UGANDA	Sep. 2010 – Sep.2013	2	0	2
9	CERTICICATE IN FINANCIAL ADMINISTRATION	ZANZIBAR	Sep. 2010 – Sep. 2011	1	2	3
10	BSC CLINICAL MEDICINE	CHINA	Sep. 2010 – Sep.2015	5	3	8
11	DIPLOMA ANAETHESIA	KCMC	Sep. 2010- Sep. 2012	1	0	1
12	MBBS MEDICINE	IMTU	Sep. 2010 – Sep. 2013	10	8	18
13	CERTIFICATE IN PUBLIC ADMINISTRATION	ZANZIBAR	Sep. 2010 – Sep. 2011	1	0	1
14	BSC.HEALTH SERVICEMANAGEMENT.	ISLANIC UNIVERSTRY UGANDA	Sep. 2010- 2013	0	1	1
15	LOW - VISION	SWEDEN	Sep. 16 – Oct. 2010	0	1	1

16	INTERNATIONAL HEALTH	DENMARK	Sep. 2010 – Sep. 2011	0	1	1
17	BACHELOR OF SURGERY AND MEDICINE	IMTU	Sep. 2010 – Sep. 2015	4	2	6
18	BACHELOR OF MEDICINE	CHINA	Sep. 2010 – Sep. 2016	2	3	5
19	CLINICAL OFFICERS	TANGA	Sep. 2010 – Sep. 2012	1	0	1
20	CONFLICT RESOLUTION	KIU	Oct. 2010 – Oct. 2013	1	0	1
21	BACHELOR OF SCIENCE IN MEDICAL LABORATORY	IMTU	Oct. 2010 – Oct. 2013	1	0	1
22	INFORMATION TECHNOLOGY	ZANZIBAR	Oct. 2010 – Oct. 2013	1	0	1
23	PUBLIC ADMINISTRATION	ZANZIBAR.	Oct. 2010 - Oct. 2013	1	0	1
24	BSC- NURSING	ST. JOHN UNIVERSITY	Oct 2010 – Oct. 2013	2	8	10
25	POST-GRADUATE DIPLOMA IN SOCIAL WORK	INSTITUTE OF SOCIAL WORK	Nov. 2010 – Nov. 2011	1	1	2
26	BUSSINESS INFORMATION TECHNOLOGY	ZANZIBAR	Oct. 2010 – Oct. 2013	1	0	1
27	ADVANCED DIPLOMA IN HISTOTECHNOLOGY ST	MUHIMBILI UNIVERSTY	Oct. 2010 – Oct. 2012	1	0	1
28	MASTER OBSTESTRIAN	DALIAN UNIVERSITY	Oct. 2010 – Oct. 2013	0	1	1
29	MASTER OF HEALTH SYSTEM MGT	MZUMBE UNIVERSITY	Nov. 2010 – Jun. 2012	1	0	1
30	MSC. NATURAL RESOURCE ASSESSMENT	UDSM	Sep. 2010 – Sep. 2012	1	0	1
31	ADVANCED DIPLOMA IN MEDICAL LAB. SCIENCE	OPEN-UNIVERSITY MUHIMBILI	Sep. 2010 – Sep.2012	1	0	1
32	MASTER IN ADMISTRATION	KIU – DAR BRANCH	Sep. 2010 – Sep. 2012	1	0	1

33	HIGHER DIPLOMAIN MGT AND ADMINISTRATION	ESAMI	Nov. 2010 – Nov. 2012	2	1	3
34	BSC. CLINICAL MEDICINE	MT. KENYEA UNIVERSITY	Jan. 2011 – Jan. 2014	1	0	1
35	BSC. BUSSINESS ADMINSTRATION	MALAYSIA	Jan. 2011 – Jan. 2013	1	0	1
36	AMO	TANGA	Sep. 2010 – Sep. 2012	1	2	3
37	BSC. SOCIAL WORK	UGANDA	Sep. 2010 – Sep. 2013	1	2	3
38	DEGREE IN PROCUREMENT AND SUPPLY.	KIU	March 2011 – March 2014	0	1	1
39	GUIDING AND COUNCELLING	KIU	Feb. 2011 - 2013	5	0	5
40	BSC. – PHARMACY	UKRAINE	Jan. 2011- Jan. 2013	2	0	2
41	DIPLOMA HUMAN RESOURCE MGT	E.P.A	Jan. 2011 – Jan. 2015	0	1	1
42	DIPLOMA IN PHARMACEUTICAL SCIENCE	C.H.S	2010 - 2013	2	4	6
43	MASTER IN H.R DEVELOPMENT	INDIA	2011-2012	0	1	1
44	MASTER IN MEDICAL EDUCATION	U.K	2010-2012	1	0	1
	TOTAL			**68**	**46**	**114**

Kiambatisho Namba 5.1: **Matatizo yaliogunduliwa wakati wa Uchunguzi wa Afya za Wafanyakazi**

Aina ya Tatizo	**Idadi**
Hypertension	54
UTI	34
Hepatitis B	18
HIV Positive	13
Hypotension	10
Typhoid	10

Poor Vision	5
Hepatitis C B	3
Allergy	3
Epileptic	2
Loss Of Hearing	2
Deformity Left Hand	1
Head Eczema	1
Diabetic	1
Ptb	1
Otitis Medium	1
Heart Enlargmut	1
Splush Of Liquarami On Face	1
Jumla	**161**

Kiambatisho Namba 5.2: **Taarifa za uchunguzi wa vimeea kwa njia ya darubini na RDT katika Vituo vya Afya, Julai – Disemba 2010**

	Idadi	Wenye Vimelea	Asilimia
Waliochunguzwa kwa Darubuni	29,233	135	0.5
Watoto chini ya miaka 5	9,537	36	0.4
Waliochunguzwa kwa RDT	37,797	272	0.7
Watoto chiniya miaka 5	19,909	42	0.2

Kiambatisho Namba 5.3: **Takwimu halisi za vyandarua vilivyogaiwa kwa mama wajawazito kwa Wilaya sita za Unguja.**

Wilaya	**Idadi ya vyandarua vilivyotolewa**
Kusini	851
Magharibi	3,482

Kaskazini “A”	2,594
Kaskazini “B”	1,558
Kati	1,937
Mjini	1,991
Jumla	**12,413**

Kiambatisho Namba 5.4: **Jadweli ya Idadi ya Wagonjwa Waliochunguzwa Ugonjwa wa Kichocho, Julai 2010-Machi 2011**

Mwezi	**Waliokaguliwa**	**Waliobaininka na Maradhi**			**Asilimia**
		Wanaume	**Wanawake**	**Jumla**	
Julai	208	152	34	18	89.4
Agosti	217	162	34	196	90.3
Septemba	213	150	25	175	82.2
Oktoba	269	204	28	232	86.2
Novemba	188	132	15	147	78.2
Disemba	312	174	51	225	72.1
Januari	269	186	35	221	82.2
Februari	228	170	31	201	88.2
Machi	121	90	11	101	83.5
Jumla	**2025**	**1420**	**264**	**1684**	**83.2**

Kiambatisho Namba 6.1: **Mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki katika hospitali za Idara ya Tiba, Julai 2010 - Machi 2011**

Hospitali	Wagonjwa wa Nje		Waliolazwa		Waliofariki	
	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me
Abdallah Mzee	14,276	9,778	1,365	655	30	36
Micheweni Cottage	10,101	8,072	918	437	10	15
Vitongoji Cottage	6,297	6,038	286	206	2	10
Chake Chake	31,350	3,729	3,100	1,195	55	54
Wete	18,907	6,852	1,649	659	25	44
Makunduchi Cottage	8,909	6,134	404	248	10	2
Kivunge Cottage	13,628	1,300	1,397	274	13	10
Jumla	**1 03,468**	**81,903**	**9,119**	**3,674**	**145**	**171**

Kiambatisho Namba 6.2: **Taarifa ya hali Uzazi katika Wodi ya Wazazi kwa Hospitali za Idara ya Tiba, Julai 2010 hadi Machi 2011**

Hospitali	Wajawazito waliolazwa	Waliojifungua kwa		Watoto waliozaliwa hai		Wazazi Waliofariki
		Njia ya kawaida	Upasuaji	W'me	W'ke	
Micheweni	610	448	ns	246	210	1
Vitongoji	127	104	ns	54	51	0
Chake Chake	2,409	1,832	179	1,065	931	10
Wete	1,127	881	36	457	487	6
Mkoani	1,164	856	87	516	456	3
Kivunge	1,504	979	ns	518	507	0
Makunduchi	415	347	8	183	182	0
Jumla	**7,356**	**5,447**	**310**	**3,039**	**2,824**	**20**

Kiambatisho namba 7.1: **Mahudhurio ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki katika Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Julai 2010 - Machi 2011**

Hospitali	Wagonjwa wa Nje		Waliolazwa		Waliofariki	
	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me
Mnazi Mmoja	50,069	47,137	28,056	13,184	259	378
Mwembe Ladu	*	**	6,076	**	0	0
Mental	4,364	**4,120**	440	350	0	0
Jumla	**54,433**	**51,257**	**34,572**	**13,534**	**259**	**378**

** Huduma hizi hazitolewi katika Idara hiyo*

*** Haihusiki*

Kiambatisho Namba 7.2 : Taarifa ya hali Uzazi katika Wodi ya Wazazi kwa Hospitali za Mnazi Mmoja na Mwembeladu, Julai 2010 hadi Machi 2011

Hospitali	Wajawazito	Waliojifungua kwa		Watoto waliozaliwa hai		Wazazi walio fariki
	waliolazwa	Njia ya kawaida	Upasuaji	W'me	W'ke	
Mnazi mmoja	7,564	5,593	1,322	3,615	3,676	29
Mwembe Ladu	3,543	3,240	*	1,582	1,707	0
Jumla	**11,107**	**8,833**	**1,322**	**5,197**	5,383	**29**

** Huduma zilikua hazijaanza kutolewa*

Kiambatisho namba 7.3: Mahudhurio ya Wagonjwa katika klinik za Maradhi maalum hospitali ya Mnazi Mmoja Julai 2010- Machi 2011

Kliniki	Wanawake	Wanaume	Jumla
Acupuncture	1,284	1,030	2,314
Dental	1,829	1,758	3,587
Diabetic	2,883	2,090	4,973
Ear Nose & Throat (ENT)	2,265	3,099	5,364
Eye	8,385	5,969	14,354
Gynaecology	1,202	**	1,202
Care & Treatment (CTC)	4,787	2,618	7,405
Hypertension	1,023	504	1,527
Orthopedic	885	1,762	2,647
Pediatric	438	746	1,184
Physiotherapy	1,022	868	1,890
Skin Diseases	2,003	1,446	3,449
Surgical OPD	1,990	3,227	5,217
Major Theatre	445	525	970
Minor Theatre	2,683	6,716	9,399
Eye Theatre	45	41	86
Jumla	**33,169**	**32,399**	**65,568**

** *Haihusiki*

Kiambatisho Namba 9.1: **Thamani ya Dawa na Zana za Tiba zilizopokelewa na Wizara ya Afya kutoka kwa wadau wa Maendeleo, Julai 2010 – March 2011**

S/N	JINA	THAMANI YA DAWA/CHANJO - Tsh.
1	DANIDA	547,088,740
2	SMZ	234,170,986
3	ADB	221,020,500
4	GLOBAL FUND	77,254,500
5	UNICEF	46,315,500
6	ICAP	9,518,210
7	USAID	575,000
JUMLA KUU		**901,772,450**

Kiambatisho Namba 10.1: **Idadi ya Sampuli zilizochunguzwa Julai 2010- Machi 2011**

SAMPULI	POLISI	WAFANYA BIASHARA	WATU BINAFSI
Bhangi	96	0	0
M/kulevya	90	0	0
Pombe	66	0	0
Mikojo	190	0	0
Damu	14	0	0
Tindikali	2	0	0
Swarbs	1	0	0
Sumu	4	0	0
Mchele	0	5	0
Maji	0	2	0
Chakula	0	2	0
Pipi	0	1	0
Mafuta	0	1	0
Sabuni	0	2	0
Dawa	0	3	0

Pembejeo	0	0	1
Soda	0	0	2
Jumla	**463**	**16**	**3**

Kiambatisho Namba 11.1: **Idadi ya Wanafunzi Wanaoendelea na Masomo Chuo cha Afya Mbweni**

Kada	**Mwaka 1**	**Mwaka 2**	**Mwaka 3**	**Mwaka 4**
Wauguzi		102		112
PHN B	29	77		
Maafisa Afya		73		
Maafisa Tabibu		74		
Maabara		99		
Jumla	**29**	**425**		**112**
Jumla KUU	**566**			

Kiambatisho namba 12.1a: **Taarifa ya huduma ya Chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja Julai - Disemba 2010**

WILAYA	**WALENGWA (Target Popn)**	**BCG**		**POLIO 3**		**SURUA**	
		IDADI	**%**	**IIDADI**	**%**	**IDADI**	**%**
Kati	2,232	1,159	51.9	1,305	58.5	1,374	61.6
Kaskazini"A"	4,568	2,204	48.2	2,095	45.9	2,173	47.6
Kaskazini"B"	2,722	1,347	49.5	1,189	43.7	1,313	48.2
Kusini	1,072	455	42.4	560	52.2	582	54.3
Mjini	7,399	6,952	94.0	4,645	62.8	4,559	61.6
Magharibi	7,527	4,995	66.4	4,165	55.3	3,816	50.7
Unguja	**25,520**	**17,112**	67.1	**13,959**	54.7	**13,817**	54.1
Chakechake	5,873	3,359	57.2	2,538	43.2	2,512	42.8
Micheweni	6,117	2,578	42.1	2,217	36.2	2,275	37.2
Mkoani	6,279	2,395	38.1	2,095	33.4	2,523	40.2
Wete	6,223	3,407	54.7	2,621	42.1	2,897	46.6

Pemba	**24,492**	**11,739**	**47.9**	**9,471**	38.7	**10,207**	41.7
Zanzibar	**50,012**	**28,851**	**57.7**	**23,430**	46.8	**24,024**	48.0

Kiambatisho namba 12.1b: Taarifa ya Huduma ya Chanjo kwa Watoto chini ya mwaka mmoja Januari - Machi, 2011

WILAYA	WALENGWA (Target Popn <1)	BCG		POLIO 3		SURUA	
		IDADI	%	IIDADI	%	IDADI	%
Kati	2,254	508	22.5	695	30.8	753	33.4
Kaskazini"A"	4,721	949	20.1	957	20.3	784	16.6
Kaskazini"B"	2,835	583	20.6	584	20.6	508	17.9
Kusini	1,080	194	18.0	284	26.3	209	19.4
Mjini	7,484	3,183	42.5	1,793	24.0	2,169	29.0
Magharibi	7,477	1,695	22.7	1,355	18.1	1,301	17.4
Unguja	**25,851**	**7,112**	**29.3**	**5,668**	**21.9**	**5,724**	**22.1**
Chakechake	6,136	1,506	24.5	1,193	19.4	1,217	19.8
Micheweni	6,363	1,195	18.8	1,021	16.0	1,021	16.0
Mkoani	6,505	369	5.7	353	5.4	374	5.7
Wete	6,466	1,613	24.9	1,128	17.4	1,170	18.1
Pemba	**25,470**	**4,683**	**18.4**	**3,695**	**14.5**	**3,782**	**14.8**
Zanzibar	**51,321**	**11,795**	**23.0**	**9,363**	**18.2**	**9,506**	**18.5**

Kiambatisho Namba 12.2: **Idadi ya Wajawazito Waliojifungua Katika Vituo vya Afya Julai 2010 hadi Machi, 2011**

Kituo	**Idadi ya Wazazi waliojifungua (2009/2010)**	**Idadi ya Wazazi waliojifungua (2010/2011)**	**Watoto wa Kike waliozaliwa**	**Watoto wa Kiume waliozaliwa**	**Jumla ya Watoto Wote**
Bumbwini Misufini	46	30	20	10	30
Chukwani	30	99	50	48	98
Fuoni	201	197	123	95	218
Jambiani	13	8	5	3	8
Makangale	50	36	20	15	35
Muyuni	3	2	0	2	2
Ndagoni	96	114	63	42	105
Pujini	37	48	17	31	48
Uroa	22	26	11	17	28
Wingwi	8	9	8	4	12
Bogowa	83	61	32	25	57
Nungwi	30	33	23	10	33
Gomani	10	7	2	4	6
Maziwa Ng'ombe*	7	37	18	19	37
Gamba		2	2	0	2
Fundo		7	4	1	5
Donge Vijibweni		57	32	27	59
Konde		20	11	9	20
TOTAL	**636**	**793**	**441**	**362**	**803**

***Kiambatisho namba 12.3*: Mahudhurio Katika huduma ya mama baada ya kujifungua katika klinik Julai 2009 - Machi 2011**

Wilaya	**Kati ya siku ya 2 - 7**	**Kati ya siku ya 8 - 28**	**Kati ya siku ya 29 - 42**
Kati	91	148	117
Kaskazini"A"	142	539	437
Kaskazini"B"	22	89	74
Kusini	44	20	57
Mjini	181	793	527
Magharibi	167	235	203
Chakechake	210	582	718
Micheweni	92	501	317
Mkoani	37	460	391
Wete	92	492	518
Jumla	**1,078**	**3,859**	**3,359**

***Kiambatisho namba 13.1*: Wataalamu wa Fani za Afya Waliopo, Mahitaji halisi na Upungufu**

Kada	**Waliopo**	**Mahitaji halisi**	**Upungufu**
Specialist Doctors	17	109	92
Medical Doctor	18	55	37
Assistant Medical Officer	52	65	13
Clinical Officer	142	361	219
NURSES	305	941	636
LABORATORY ALL	276	412	136
MEDICAL IMAGING ALL	18	44	26
PHYSIOTHERAPHY	7	22	15
PHARMACY ALL	160	200	40
DENTAL	28	88	60
ENVIRONMENTAL HEALTH OFFICERS	155	246	91

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya kwa lengo la kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha uliopita 2010/2011 pamoja na muelekeo wa Bajeti na Malengo ya Wizara kwa mwaka mpya wa fedha 2011/2012.

Mhe.Spika, aidha kwa niaba ya Kamati napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa afya kuhusu mapendekezo ya bajeti ya wizara yake

Mhe. Spika, pia napenda nimshukuru Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya kwa kuwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 na muelekeo wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/12.

Mhe. Spika, nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao wakati wa kuijadili na kuichambua kwa kina Bajeti ya Wizara ya Afya na hatimae kuweza kutoa mapendekezo pamoja na kuishauri Serikali.Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hijja Hassan Hijja - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
4. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
6. Mhe. Saleh Nassor Juma - Mjumbe
7. Mhe.Nassor Salim Ali - Mjumbe
8. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
9. Ndg. Talib Enzi Talib - Katibu
10. Ndg.Shemsa Maabad Mohamed - Katibu

Mhe. Spika, kamati ilipokea maelezo ya taarifa ya utekeklezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2011/2012 ya Wizara ya Afya tarehe 9/06/2011 na kujadili yafuatayo:-

1. Muundo wa Wizara katika taasisi zake zinazojumuisha Idara ya sera, Mipango na Utafiti,Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Kinga, Idara ya Tiba, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mkemia Mkuu wa

Serikali, Mfamasia Mkuu wa Serikali, Idara ya Bohari Kuu ya Dawa, Maabara ya Afya ya Jamii Pemba, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Bodi ya Wauguzi na Bodi ya Huduma za Hospitali Binafsi.

2. Utekelezaji wa malengo makuu ya wizara kwa mwaka 2010/2011 na maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.
3. Utekelezaji wa miradi mbali mbali ya wizara katika mwaka 2010/2011 na malengo ya uendelezaji wa miradi hiyo katika mwaka 2011/2012.
4. Aidha, kamati ilipitia vifungu na kasma za Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Wizara ya Wfya kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kupendekeza kufanyika baadhi ya marekebisho katika makadirio ya mapato baada ya kujadili vianzio vyengine vya mapato vya wizara ambavyo havikuainishwa, kama vile makusanyo yatokanayo na michangio ya maegesho ya magari, baskeli, ada ya operesheni ya uzazi na kadhalika. Hivyo, kwa ujumla marekebisho ya makadirio ya mapato hayo ni shilingi 537,000,000 badala shilingi 52,000,000 zilizoainishwa awali.

Mhe. Spika, maoni ya Kamati na ushauri kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2010/2011 na muelekeo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, mfumo mzima wa utoaji wa huduma za afya nchini unahitaji sera imara pamoja na sheria zinazotekelezwa ipasavyo. Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaipongeza Wizara ya Afya kuona umuhimu wa kufanya mapitio makubwa ya Sera ya Afya ya mwaka 1999. Kwa mwaka mpya wa fedha Waheshimiwa Wajumbe tutarajie kuwa na sera mpya ya afya ambayo itatoa wigo mpana zaidi wa utekelezaji wa mikakati na malengo ya wizara pamoja na mabadiliko yanayotokea.

Mhe. Spika, aidha kamati yangu inaunga mkono Wizara ya Afya katika juhudi za kuimarisha nguvu kazi ikiwemo mafunzo katika kada mbali mbali za afya pamoja na kuajiri wafanyakazi wapya katika vituo na hospitali zetu.
Mhe. Spika, hatua hiyo itasaidia kuondokana na tatizo kubwa la uhaba wa wafanyakazi katika sekta ya afya. Ingawa kuna taarifa kuwa baadhi yao walioajiriwa kwa upande wa Pemba hawakuonesha hamu ya kufanya kazi huko kutokana na madai kuwa bado wizara haikuimarisha miundombinu ya makaazi kwa waajiriwa. Hivyo, kamati inaishauri wizara kufikiria kuanzisha miradi ya miundombinu ya makaazi kwa wafanyakazi wake ili kuweza kuilinda nguvu kazi mpya katika sekta ya afya.

Mhe.Spika, ushirikishaji wananchi katika utoaji wa huduma ni jambo muhimu, kamati yangu inaipongeza wizara kwa kuweza kutaarisha Mpango wa Mkakati wa Afya ya Jamii(*Community Health Strategy*) ambapo kamati kiongozi za afya za shehia zitaundwa ili kutumika kama kiungo baina ya wafanyakazi wa afya na wananchi.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MOJA

Mhe. Spika, kamati yangu imefurahishwa sana na mpango wa serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012, kuanzisha mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tunaikumbusha wizara kuwa, bado inachangamoto kubwa ya kukishughulikia chumba cha wagonjwa mahatuti *ICU* na kile cha upasuaji ili viweze kufikia viwango. Sehemu hizi zinakabiliwa na matatizo mengi na ya msingi hali ambayo kamati imeona inahatarisha maisha ya watu wetu kutokana na umuhimu wa sehemu hizo.

Ingawa wizara na serikali kwa ujumla imesema kuwa inaelewa hali hiyo, lakini kamati imeona kuwa hilo ni tatizo kubwa na ni la muda mrefu ambapo hakuna dalili za ushughulikiwaji kutokana na kuwa serikali inaendelea kusubiria washirika wa maendeleo. Kamati ilitegemea angalau wizara katika bajeti hii ingelionesha nia ya kuanza kuchangia ili kuinusuru *ICU* kwa hatua za dharura na wahisani wakiona ili wapate moyo wa kuchangia zaidi lakini sivyo hali ilivyo.

Mhe. Spika, katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa kuna baadhi ya wagonjwa katika sehemu za huduma za wagonjwa wa sukari wanamiliki vifaa vya upimaji sukari kinyume na utaratibu na huwa wanavitumia kwa kuwatumia wangojwa wenzao kwa malipo ya juu. Mhe. Spika, hili linaendelea kufanyika kutokana na madai kuwa hospitalini hapo hakuna kifaa hicho.

Kamati yangu inaiomba wizara kufatilia kwa karibu suala hili ili iweze kuwaondolea usumbufu wagonjwa hao. Kamati pia inaendelea kukemea kuwepo kwa lugha mbaya zinazotolewa na baadhi ya wauguzi dhidi ya wagonjwa hasa katika sehemu za wazazi. Kuna haja kwa wizara kuandaa vikao maalum kila muda ili kuwakumbusha wauguzi hao maadili ya kazi zao ili kuijengea heshima fani hiyo.

Aidha Mhe. Spika, licha ya wizara kuwa na lengo la jumla la kuanzisha mchakato wa kuzipandisha daraja hospitali za vijiji na Wilaya ikiwemo Kivunge, Makunduchi, Micheweni, Vitongoji na Wete. Kuna umuhimu wa hospitali hizo kujiwekea malengo mahsusi ili kamati husika iweze kufuatilia utekelezaji wake kwa ajili ya manufaa ya wananchi katika sekta hiyo ya afya.

Mhe.Spika, ukiachilia mbali Hospitali ya Magonjwa ya Akili ya Kidongo Chekundu hakuna hospitali iliyojiwekea malengo katika kipindi cha bajeti kilichopita cha 2010/2011. Hili ni tatizo katika kufuatia utekelezaji .

BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI

Mhe. Spika, kamati inapongeza kazi zinazotekelezwa na Bodi hii. Aidha, hatua ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi huandaa kanuni ya kushajihisha wananchi kutumia chumvi zenye maadini joto. Hicho ni kilio cha muda mrefu la kushangaza Mhe. Spika, kumekuwa na ucheleweshaji wa kutolewa kwa kanuni hizo.

Mhe. Spika, kamati yangu imebaini kuwa hakuna sheria inayowabana wadau wanaozalisha chumvi isiyo salama. Asilimia 58 ya wananchi wanatumia chumvi isiyo salama ni tatizo kubwa la kiafya.

Mhe. Spika, wizara imekamilisha rasimu ya Sheria ya Lishe kipindi kirefu sasa na kuiwasilisha katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunamuomba Mwanasheria Mkuu atueleze tatizo liko wapi, ili haraka hatua zichukuliwe na wizara iweze kuwa na sheria hiyo. Aidha, kamati inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa inaanzisha sheria itakayohakikisha usalama wa Bodi ya Chakula katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

MPANGO WA DAMU SALAMA

Mhe. Spika, wizara imeanzisha mpango wa uchangiaji wa damu salama katika maabara maalum iliyoko Sebleni kwa lengo la kuondoa usumbufu wa kutafuta jamaa wa mgonjwa kumchangia damu wakati inapohitajika. Pia kuwezesha kuwepo damu wakati wowote ikiwa tayari imechunguzwa na inakubalika kutumika kwa wagonjwa hiyo ni hatua ya mafanikio.

Kamati imebaini kuwa hakuna mchango wowote kutoka serikali kuu wa kuimarisha mpango huo. Serikali imewaachia washirika wa maendeleo pekee ni tatizo. Mhe. Spika, hilo ni lazima serikali ichangie program muhimu kama hizi. Mpango huu uingizwe katika miradi ya maendeleo. Aidha, kuna haja kwa serikali kuangalia suala la bima kwa matibabu katika hospitali za umma na binafsi ili kusaidia kufikia lengo la Mpango wa Damu Salama kuweza kujitegemea.

Mhe. Spika, kuna malalamiko ya muda mrefu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja dhidi ya baadhi ya watendaji kutoza wananchi huduma ya damu kwa malipo ya juu kinyume na utaratibu. Kamati yangu inaisisitiza wizara kufuatilia

kwa karibu vitendo hivyo na atakayebainika kuwajibishwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapatiwa huduma hiyo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Aidha, kamati inatoa rai kuwekewa majina katika beji maalum maafisa na wauguzi ambazo watapaswa kuzivaa ili kusaidia kuweza kuwagundua wanaofanya ubadhirifu huo.

KITENGO CHA TAKWIMU, MIENENDO MARADHI NA UTAFITI

Mhe. Spika, kamati inakipongeza kitengo hiki kwa ufanisi kwani kimeweza kukusanya taarifa za hospitali zote kutoka kila Wilaya na kuziingiza katika mpango wa "*data base",* kukamilisha mpango wa kuzieneza taarifa hizo pamoja na muongozo wa sera na mpango mkakati wa mfumo wa taarifa za afya.

Mhe. Spika, licha ya mafanikio hayo, Kitengo cha Tawimu kina changamoto ambazo wizara ioine umuhimu wa kushughulia mara moja. Kamati imeona kuwa kina upungufu mkubwa wa wataalamu wenye fani za kuweka kumbukumbu za taarifa za afya, aliyepo ni mmoja tu na ni muajiriwa wa ofisi ya mtakwimu, hivyo anatumilia mabosi wawili kwa wakati mmoja.

Jengine Mhe. Spika, ni usugu wa hospitali za binafsi kutoa taarifa za afya kwa ujumla, matokeo yake taarifa za serikali pekee huweza kuwa na mapungufu na kupelekea kuchelewa kukamilisha uandaaji wa mipango ya maendeleo katika sekta ya afya. Kamati yangu inashauri Bodi ya Hospitali binafsi kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo hospitali hizo katika upatikanaji wa taarifa za tawimu sahihi.

MAABARA YA MKEMIA MKUU

Mhe. Spika, kwa kweli kamati yangu imepata moyo kuona kuwa miongoni mwa miradi minne mipya ya wizara, katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali. Hali ya ofisi za maabara hii pamoja na vifaa Mhe. Spika, haisemeki inasikitisha. Kamati ilihudhunishwa hadi kuona baadhi ya watendaji katika maabara hii wakitokwa na machozi. Kwa kweli Mhe. Spika, maabara hii imeachwa mno kama haina mwenyewe.

Mfano mdogo Mhe. Spika, Kamati ilikikuta chombo kimoja cha kupimia *Alkohol* ambacho kimerithiwa tangu miaka ya 1934. Tulipohoji, tuliarifiwa kuwa kwa wakati uliopo hakifai lakini kinaendea kutumika. Hiyo ndio hali halisi ya maabara hiyo Mhe. Spika hali ambayo ilipelea asilimia 80 ya malengo yake kutofikiwa.

Mhe. Spika tunaiomba serikali kuithamini Maabara ya Mkemia Mkuu ili iweze kutekeleza majukumu yake vyenginevyo, wataalamu katika kada hizo mahsusi wataendelea kutukimbia.

MRADI WA KUZUIA MAAMBUKIZO YA UKIMWI

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inapongeza juhudi za washirika wa maendeleo katika kuendeleza mapambano ya kuzuia maambukizo ya ukimwi Zanzibar. Taarifa mbali mbali za takwimu zinaeleza kuwa bado kuna ongezeko la maambukizo ya virusi vya ukimwi. Elimu zaidi inahitajika kwa jamii ili Zanzibar iweze kukabiliana vyema na janga la ukimwi. Aidha, kuna haja kwa wizara kuhakikisha kuwa inaendeleza miradi itakayosaidia katika mapambano ya kuzuia maambukizi dhidi ya ukimwi .

Mhe Spika, taarifa za tafiti mbali mbali ndogo ndogo zilizofanywa na taasisi zisizokuwa za serikali, ikiwemo ZAPHA+, zimeeleza baadhi ya vichocheo vya maambukizi ya ukimwi Zanzibar, kuwa ni pamoja na hali ya kuendelea kuwepo kwa unyanyapaa katika utoaji wa huduma za afya na uvujaji wa siri za walioathirika, ambazo hudaiwa kufanywa na baadhi ya wahudumu katika sekta ya afya. Kamati yangu inaitahadharisha wizara juu ya hali hiyo ambayo kwa kweli inaweza kuchangia maambukizo zaidi ya virusi vya ukimwi nchini.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa ujumla kumekuwepo na maeneo ya mafanikio katika bajeti ya 2010/2011, pamoja na changamoto zinazohitaji kuchukuliwa hatua ambazo kamati yangu imeziainisha awali. Lakini, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii hairidhiki na ufinyu wa bajeti iliyopewa wizara ya afya kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Makisio yaliyopangwa ni chini ya robo ya makisio halisi yaliyoombwa.

Mhe. Spika tujiulize kweli serikali imedhamiria kutoa kipaumbele katika kuimarisha sekta ya afya? Asilimia 80 ya bajeti ya wizara inategemea wahisani, ni dhahiri kuwa bajeti hiyo haina uhalisia katika utekelezaji wake, tusije tukawasakama roho watendaji.

Mhe. Spika, kinachooneka, mambo mengi yamekuwa *centralized* wizara ya fedha na kufanya wizara hiyo iwe na bajeti nono na nzito. Hilo Mhe. Spika, wajumbe wataliona wakati ukifika wa bajeti ya wizara ya fedha. Kamati yangu inaishauri serikali ili iweze kufikia adhma ya kutoa kipaumbele katika sekta ya

afya kama ilivyoahidi, kuna haja ya kupunguza vifungu kutoka wizara ya fedha na ipeleke katika maeneo muhimu ya afya ambayo bado yanahitaji msukumo na sio kuwategemea wahisaini katika kiwango tulichofikia katika wizara ya afya.

Jengine Mhe. Spika, Kamati yangu inaungana na maoni ya kamati ya wenyeviti wa kamati kuwa serikali ni kubwa, hali ambayo imepelekea kuongezeka kwa gharama za kulipa ngazi ya utawala katika serikali kuu. Wizara, Kurugenzi, Kamisheni ni nyingi mno, tuwe na wizara kidogo zenye kutoa huduma mbali mbali kwa ufanisi na kwa mujibu wa uwezo wa uchumi tulionao. Hili linaweza kupunguza morali ya watendaji wengine hasa wa ngazi ya chini.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii tena, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia dakika hizo 15 japo hazinitoshi, lakini kwa heshima na taathima nitazikubali hivyo hivyo.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukiwa hai na kutupa pumzi na kuweza kupumua vizuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ataendelea zaidi kutupa afya njema.

Namshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu na Wakurugenzi wake wote wa Wizara ya Afya kwa kitabu chao kizuri sana, chenye muelekeo mzuri na mwelekeo wa sera ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, sera ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake ina maeneo mawili makubwa. Eneo la kwanza kuondoa malaria na eneo la pili ni kulikuza jina la Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, niingie katika suala lenyewe hasa katika ukurasa wa 21 kuhusu suala la malaria. Kwa kweli Mhe. Waziri niseme umejitahidi sana, ni asilimia ndogo sana ambayo sasa hivi inajitokeza kuwa mtu ni mgonjwa wa malaria. Japo wameambiwa wakenda hospitali wasiseme kuwa wana malaria, lakini hiyo tukubali kuwa jitihada zao ni nzuri sana humsikii mtu kusema kuwa ana malaria, isipokuwa anasema anaumwa na homa za kawaida tu.

Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 25, niende mbio mbio ni kuhusu programu ya kuondoa kichocho na minyoo. Mimi nishahidi katika eneo langu

la Jimbo la Kitope, tatizo hili ni sugu sana. Lakini kwa mashirikiano mazuri sana katika kitengo hiki, napenda niwasifu sana kitengo hiki baada ya kwenda pale na kunipa maelekezo mazuri, ni jinsi gani programu ambayo wameiandaa ili kutokomeza kabisa haya masuala ya kichocho. Mimi mwenyewe nimeridhika na niko pamoja na wao. Nimewaambia kadiri mukiona kuwa muda wa kutiwa fedha unakawia basi mimi niko tayari kuwasaidia njia ya kwenda kule kuondosha suala hili, kwa sababu tayari linaleta matatizo makubwa sana Mhe. Spika, matatizo yake ni makubwa sana. Utanifanya *population* ya Jimbo la Kitope nikose watoto sasa hivi kutokana na tatizo hili. Kwa hivyo, naiomba sana wizara hii iweze kufanya jitihada hizi haraka sana na hiyo programu Mhe. Waziri iweze kukamilika haraka sana.

Mhe. Spika, nije kwenye mabusha. Mhe. Spika, mimi mwenyewe nimefanya zoezi zuri sana katika jimbo langu, lakini sikupata msaada wowote katika wizara hii. Nishahidi tosha kama wapo wenyewe huko juu basi watakuwa shahidi kwa suala hili. Mimi nimejitahidi sana katika Jimbo la Kitope ili kuondosha haya mabusha kwa asilimia 50 mpaka 60. Kwa hivyo, nimeona hapa kuwa kumbe na wizara ina programu maalum, hivyo naomba nipate msaada wa Mhe. Waziri kwa sababu niko pamoja na wao kupigana na maradhi haya ili tuyaondoshe mara moja.

Mhe. Spika, niseme kwa makusudi, kama tulivyoeleza kwenye suala la kichocho kuwa wana programu maalum, basi na yale mabusha hebu kuwe na programu maalum ambayo inajiandaa kwa makusudi. Mhe. Spika, siku zote tunaitangaza tu kwenye vitabu lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo, hili tuseme ukweli. Kila siku programu hii ipo lakini utekelezaji wake hauoneshi vizuri.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 29 suala la macho. Siku zote sisi huwa tunasema, juzi moja tulisema hapa kuhusu waha maTX wetu wakija hapa hawajui Kiingereza. Mimi nilikuwa shahidi tosha juzi, Mchina hajui Kiingereza wala kutumia mashine za macho hajui, nilimuondoa mgonjwa wangu taratibu baada ya kusikia kule anafundishwa, mimi nilimuondoa mgonjwa wangu nikasema hakuna kufundishwa kwenye mwili bwana, isipokuwa mafundisho ni kwenye karatasi tu.

Nikamwambia twende zetu mgonjwa wangu. Kila anayeingia mule nilikaa kumuhesabia masaa, alipokuja alikuwa yuko *serious* Mwenyezi Mungu amjaalie awe salama huyo. Kwa sababu Mchina yule hajui Kiingereza, hajui Kiswahili na wala hajui hata ule ububu. Hili tukikuambieni hamkubali, juzi tuliwaambia mkatukatalia kata kata hapa, sasa na hili nikatalieni, nimelishuhudia mwenyewe hili, wala sikutaka ushahidi wa mtu. Kwa kweli

Mhe. Spika, tuwafikirie wenzetu kutokana na hali ilivyo. Ni kweli utaniambia kwamba ni TX mzuri, lakini sasa uTX wake kwenye mwili wa binadamu.

Mhe. Spika, kuna jamaa mmoja simtaji, aliniambia mheshimiwa ungetupigia simu tungekuambia kwanza minya usimlete mgonjwa wako, kwa sababu kwanza hatujaona uzoefu wake wa kazi ukoje. Kwa hivyo, hili suala liangalieni tena kwa umahiri kabisa.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 41 huduma katika kliniki maalum. Hapa kuna mambo mengi yametajwa lakini kuna hii ripoti sijaisikia ya matatizo ya kina mama ya *cancer* ya matiti, sijui inaitwaje hii nadhani saratani ya matiti. Mhe. Spika, programu hii ilikwishaje, nilitegemea humu kwenye kitabu itakuwemo lakini sioni, kama imo sawa basi mimi nafurahika nayo kuwa kiwemo hichi kitu na kiweze kufanyiwa utafiti haraka sana, kama imo sawa na kama ni masihara basi twende nayo hivyo hivyo. Lakini mimi nina imani hiyo kuwa lipo suala hilo kwa sababu kina mama wengi wanapata matatizo hayo na hakuna huduma endelevu ya kufanyiwa kwa maradhi hayo.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu matatizo ya kisukari. Mimi rai yangu kwa kuwa vitengo vingi viko karibu pale kwenye hospitali yenyewe, kuna sehemu za wazi pale, sisi hatutaki bustani bwana, tunachotaka lile eneo tupewe ili tujenge hospitali yetu ya wagonjwa wa sukari. Wagonjwa wa sukari wamo wengi wana chama. Kwa hivyo, naomba kwa makusudi kwa sababu kitengo cha sukari kwa Wizara ya Afya kimetupwa, hakishughulikiwi kabisa. Mimi naona tuwape eneo lile la bustani na pia watu wa macho, kwa sababu lile ni eneo kubwa. Siku hizi unatakiwa ukijenga uende juu, sio uende kwa upana. Kwa hivyo, panatosha pale lile eneo kwa watu wa macho na sukari, kwa sababu lile eneo la macho ni dogo sana siku za upasuaji wanafika kwenda kukodi au kuazima katika wodi nyengine, kwa kweli suala hili halipendezi na sisi tunaelekea kutaka hospitali yetu itambulikane kuwa ni ya rufaa.

Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 43 kifungu cha 6(11)(3) kuhusu habari ya mikakati ya Wizara Afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuelekea katika rufaa. Namuunga mkono Mhe. Mwenyekiti, kuwa hatujawa tayari, kwa sababu leo tukiangalia ile hospitali yenyewe ya Mnazi Mmoja kuisema kuwa ni ya rufaa kwa kweli tunaionea. Tukiingia katika chumba cha upasuaji basi zile nguo hazifai hata kidogo ni mbovu. Wazee wamesema mgeni njoo mwenyeji apone, wakija wataalamu ma-*specialist* wa magonjwa makubwa wanakuja na zana zao, wakiondoka tunaridhi sisi, hatimaye tunakuwa hatuna, hili suala ni lazima tuseme ukweli Mhe. Spika. Fungu waliotiliwa hili ni dogo sana, halitoshi hata kidogo, tunafanya mzaha tu. Fungu hili ni sawa sawa na timu ya mpira tu imetosha. Leo Wizara Afya ni wizara kubwa, wizara okozi, maana

yake inaokoa uhai wa binadamu. Kwa sababu nimeshashuhudia binadamu anatiwa *theater* hatimaye anarudi mzima, huwezi kuamini si ameokolewa huyo. Lakini leo kule *theater* hata zile nyuzi hakuna, halafu tunasema ni ya rufaa. Tufuteni jina la rufaa, kwa sababu halijaendana na wakati wa rufaa kabisa, ukweli tuuseme. Fungu hilo halifai ni ndogo kabisa.

Juzi mheshimiwa wangu mtaalamu Mhe. Haji Omar Kheir alisema anaongeza asilimia 25, lakini leo *specialist* ana laki tatu, hizo laki tatu pamoja na hiyo inakuwa ni ngapi, inakuwa ni 25, haya ni TX huyo. Wenzetu Tanzania Bara sasa hivi wana *point five.* Sasa kuna mambo mengine Mhe. Spika, hebu tuangalieni tusifanye mzaha, niliwaambia kuna wizara nyengine ni lazima tuzipe nafasi kubwa katika mishahara yao.

Mhe. Waziri alisema kuwa sasa tunatafuta madaktari bingwa. Je utampata kweli kwa shilingi laki tatu na ishirini na tano, humpati hata siku moja mheshimiwa usijidanganye babu yangu Juma, mimi nakupenda sana. Lakini kwa pesa hiyo utapata tabu bure huna.

Mhe. Spika, ukenda katika *ICU*, ukiingia pale na mwenyewe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais yupo tulikutana siku moja hospitali. Mwenyezi Mungu alitujaalia tulipofika hospitali umeme ukazimwa vuu! Usiku. Sasa tunatafutana Mhe. Makamo kapenya wapi na mimi nimepenya wapi, ulizimika kabisa. Kwa kweli kile chumba cha *ICU* kinaitwa tu jina hili la *ICU*, lakini mimi nashangaa sana kwa sababu *ICU* za wenzetu, kwa mfano kama mimi nimekwenda *ICU* ya Dar es Salaam ukiingia ubaridi mzuri. Lakini hapa kwetu mule *ICU* muna mapangaboi tutamuuwa huyo mgonjwa. Halafu kuna chumba maalum. Zamani kulikuwa kuna kama kompyuta ambazo ni za kumuangalia mtu ni jinsi gani *temperature* inavyokwenda, wataalamu wenyewe watanisaidia, wanaita *monitor* sijui.

Mhe. Spika, zamani daktari anakaa kwenye kile chumba anaangalia kitanda nambari ngapi, mgonjwa *temperature* yake inakwenda vipi na monitor yake inakwenda vizuri. Lakini sasa ananyanyuka aende kule arudi, Mhe. Spika, twende na wakati bwana, hii hospitali tunataka kuielekeza kwenye rufaa. Kwa hivyo, mimi naomba sana kwa makusudi kuwa fungu hili narudia tena bado, mimi nitashindwa kuunga mkono kama fungu hili halikuongezwa, ni dogo sana babu Juma tunampa mzigo mzito, kila siku babu yangu ana konda na hospitali ile na ndio mnamuona kaweka tama yule pale. Hana fedha Mhe. Spika, fedha mnamtilia kidogo hizi.

Mhe. Spika, wanajitahidi na miradi yao ile ya kukusanya mabaskeli na magari, sasa la kusikitisha na hili fungu analitaka Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na

Mipango ya Maendeleo. Mimi ningeomba Mhe. Spika, fungu hili waachiwe wenyewe kwa sababu wanaziba siri, kwa fungu hili la kukusanya vitu pale baskeli na gari zinawasaidia. Lakini leo limeandikwa humu fungu hili linakwenda katika serikali kuu. Mhe. Spika, wapewe wenyewe mara moja, warudishiwe ili waweze kutusaidia ndipo tutakapopata mambo mazuri.

Vile vile niwashukuru sana serikali kuu imetutengenezea *lift*, hii *lift* kila siku tunaipigia kelele. Sasa imetengenezwa *lift* ya kwanza tumalize na ya pili, vyenginevyo vyovyote tutaibebesha mzigo mzito na tutashindwa, baadae itakuja kuharibika ile na itakuwa ndio yale yale sifuri tu, tunarudi nyuma.

La mwisho Mhe. Spika, kwa kumalizia niseme kuwa, kuna tatizo ambalo namshukuru sana Mhe. Waziri Mohammed Aboud Mohammed amelifuatilia vizuri sana, suala la pale chuoni. Mhe. Spika, suala hili hatua iliyofikia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ikamilishe ile hatua waweze kukamilisha ili angalau ionekane serikali sasa lengo lake, ikichukua kitu ina mategemeo ya kuweza kufanya kitu tulichokikusudia.

Mhe. Spika, naona umeshawasha taa hapo kwenye *mike* yako. Kwa hivyo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni. Namshukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa kutumia dakika 15 vizuri. Sasa naahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 06/07/2011, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 06/07/2011 saa 3:00 za asubuhi)